# Nipashe

Jumanne Machi 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579869

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Waziri aagiza waliolipwa fedha korosho kuanikwa

UKURASA 3




UKURASA 13

# Maalim Seif aitikisa CUF

• **Ni** baada ya kutimkia ACT- Wazalendo, bendera zashushwa kila kona, umati wamfuata 'makao mapya'...*Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kujiunga na chama cha ACT-Wazalendo. Kushoto ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Nassor Ahmed Mazrui. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge mwingine upinzani matatani



UKURASA 2



UKURASA 2

## Askari polisi mbaroni kupiga dereva, abiria


FiveStar
write more.....

Come meet us at
paperworld
Middle East Exhibition

When?
18th - 20th Mar 2019

Where?
Dubai, UAE

Booth No?
S3 C45

Venue?
Dubai International Convention & Exhibition Centre



PART OF MASUMIN GROUP OF COMPANIES

21512302

# Maalim Seif aitikisa CUF

**Na Waandishi Wetu**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Maalim Seif Sharif Hamad, amekitikisa chama hicho baada ya kujivua uanachama na kujiunga na Chama cha ACT-Wazalendo.

Maalim Self aliyewahi kushika nafasi za juu katika uongozi serikalini, alitangaza uamuzi huo jana, jijini Dar es Salaam, muda mfupi baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kubariki uamuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa kumtambua Prof. Lipumba kuwa Mwenyekiti wa CUF.

Mara tu baada ya mwanasiasa huyo kutangaza uamuzi huo mbele ya waandishi wa habari, bendera za CUF zilionekana zikishushwa katika ofisi mbalimbali za CUF nchini. Visiwani Zanzibar, kunakoaminika kuwa ngome kuu ya CUF, ofisi ya makao makuu ya chama hicho iliyoko Mtendeni, ilifungwa, huku bendera za chama hicho pia zikishushwa muda mfupi baada ya Maalim Seif kutangaza uamuzi wa kujiunga na ACT-Wazalendo.

Hali kama hiyo ilionekana mjini Tanga ambako uongozi wa CUF Wilaya ya Tanga uliagiza kushusha bendera chama hicho na kupandisha za ACT-Wazalendo katika ofisi zao zote wilayani humo.

Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Tanga, Rashid Jumbe, alisema jana kuwa uongozi wao umeamua ofisi za wilaya na kata zote 27 wilayani mwake washushe bendera za chama hicho na kupandisha za ACT-Wazalendo.

Alidai tayari agizo hilo limeshatekelezwa na kuanzia leo, kila aliyekuwa kiongozi wa CUF atakuwa na jukumu la kupokea wanachama wa CUF na kuwapa kadi za ACT-Wazalendo.

"Zoezi la leo (jana) ni kushusha bendera zote za CUF wilaya nzima na kesho (leo) ni kazi ya kupokea wanachama wa CUF kwenye ofisi na matawi yote na kuchora nembo za ACT na kufuta za CUF, Jumbe alisema.

Baadhi ya wanachama wa CUF

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli, akitoa mkono wa pole kwa Mbunge wa Viti Maalumu wa Geita, Vicky Kamata mtoto wa marehemu mama Paulina Kasama Selemani ambaye ni dada wa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo (kulia), kwenye misa ya kumuombea marehemu iliyofanyika katika kanisa la Mtakatifu Petro jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mbunge mwingine upinzani matatani

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Kilombero (Chadema), Peter Lijualikali, ameingia matatani baada ya kudaiwa kumkashfu Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Ndugai amelalamika kuwa mbunge huyo alimkashfu alipozungumza na waandishi wa habari juzi, hivyo anafikiria hatua stahiki za kumchukulia.

Lijualikali anasubiri adhabu yake kutoka kwa Spika Ndugai kutokana na maelezo aliyoyatoa juzi dhidi ya kiongozi huo wa Bunge yaliyodaiwa kujaa tuhuma na kejeli.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa cha Bunge, maelezo yaliyotolewa na mbunge huyo yamesheheni tuhuma zenye kejeli na dharau dhidi ya Spika na ofisi yake.

"Maelezo hayo aliyatoa wakati akizungumza na waandishi wa habari juzi, Spika Ndugai anatafakari hatua za kinidhamu za kumchukulia Lijuakali," ilisema taarifa hiyo.

Alhamisi iliyopita, Bunge lilitoa taarifa kuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, Joshua Nassari, amepoteza sifa za kuwa

INAENDELEA UK. 8

# Askari polisi waliowapiga dereva, abiria mbaroni

**Na Mary Geofrey**

JESHI la Polisi linawashikilia askari wake wawili wa Kikosi cha Usalama Barabarani kwa tuhuma za kufanya makosa ya kuwashambulia kwa matusi na kipigo dereva wa gari na abiria wake.

Tukio hilo lilianza kusambazwa juzi kwenye mitandao ya kijamii kupitia video fupi inayowaonyesha watu wawili wenye sare za Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani, wakiwatukana matusi na kuwapiga dereva na abiria wake wakati walipokuwa wakishuka kwenye gari.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, alitoa agizo la kukamatwa kwa askari hao juzi, akieleza kuwa wamekosa uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa mafunzo na uchoraji picha za usalama barabarani yanayotolewa na Kampuni ya Mafuta ya Puma kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini, Masauni alisema kitendo kilichofanywa na askari wake hakikubaliki ndiyo maana wamewachukulia hatua dhidi yao.

Masauni alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya madereva kubambikwa makosa au askari kufanya vitendo vilivyo kinyume cha mwenendo mwema wa jeshi hilo, na walipoona tukio hilo, watachukulia hatua dhidi ya askari hao mara moja.

Naibu waziri huyo alisema askari polisi wanaotuhumiwa kufanya tukio hilo wanashikiliwa na jeshi hilo, wakati wakisubiri taratibu za kisheria.

Alisema vitendo vinavyolalamikiwa na wananchi dhidi ya Jeshi la Polisi ni pamoja na askari wake kupokea rushwa, lugha chafu kwa madereva na kuwashambulia.

"Jana (juzi) kuna video ambayo ilikuwa ikisambaa kwenye mitandao ya kijamii ikiwaonyesha askari wakimtukana dereva pamoja na abiria waliokuwamo," Masauni alisema.

"Na si hivyo tu, ilifika hatua hadi kumpiga. Baada ya tukio hili, nilimwagiza Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani achukue hatua kwa suala hili.

"Jana (juzi) nilipewa taarifa wamekamatwa askari waliofanya kitendo kile na wamewekwa ndani na sasa wanasubiri kufikishwa kwenye vyombo vya sheria."

Alisema watuhumiwa wanashikiliwa kwenye Kituo Kikuu cha Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, huku akiwataka wananchi kutoa taarifa pindi wanapoona kuna vitendo viovu vinafanywa na askari polisi. Alisisitiza kuwa ikitokea uongozi wa jeshi hilo unatetea au kutochukua hatua stahiki, mlalamikaji awataarifu viongozi wa juu wa wizara.

"Ninawaasa askari wote kuwa serikali iko makini na haitaruhusu mwananchi yeyote aonewe na vyombo vya dola. Pia hatutaruhusu mwananchi au taasisi yoyote imuonee askari kwa sababu yoyote ile," Masauni alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
18 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 26-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam kuelekea Ifakara**, gari hilo lenye namba za usajili: **T 881 AUX / T 137 CHN**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 20 |
| **Upana** | - | mita | 3.20 |
| **Kimo** | - | mita | 4.80 |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Ifakara** Kupitia Mikumi, gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215123902



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
18 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 26-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Mbagala kuelekea Dar Port** , gari hilo lenye namba za usajili: **T 653 DFA / ZE 1194**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 27.90 |
| **Upana** | - | mita | 2.84 |
| **Kimo** | - | mita | 4.80 |

3. Njia itakayotumika: **Mbagala hadi Dar Port** Kupitia Kilwa Road / Nelson Mandela Road, Gari Litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215123902

CRDB BANK
The bank that listens

INDEPENDENT NON EXECUTIVE DIRECTOR

CRDB Bank Plc is a leading, private commercial bank in Tanzania. Established in 1996, the Bank has grown and prospered over the years to become the most innovative and trusted Bank in the country. The Bank reached an important milestone when it was listed on the Dar es Salaam Stock Exchange on 17th of June, 2009. CRDB Bank owns three subsidiary companies - CRDB Microfinance Services Company Limited, CRDB Bank Burundi S.A. and CRDB Insurance Broker Company Limited.

The Board of Directors of CRDB Bank Plc would like to invite applications from suitable candidates for the position of Independent Non Executive Director.

**Duties and Responsibilities**

As a member of the Board of Directors, the Independent Non Executive Director will perform the following primary duties and responsibilities with other Board Members:

- To determine the Bank's vision, mission and values, continuously monitor and evaluate its strategy and ensure the Bank survives and thrives.
- To govern the Bank by broad policies and objectives, as formulated and agreed with the Managing Director.
- To assess the performance and effectiveness of the Board as a whole, and that of individual Directors and Board Chairman.
- To select and appoint the Managing Director of the Bank, review and evaluate his/her performance regularly and offer administrative guidance.
- To select and appoint the Director of Internal Audit, who shall report directly to the Board of Directors, and review his/her performance regularly.
- To oversee the Risk Management function within the Bank and its subsidiaries, and the effective management of investor relations.
- To appoint direct reports to the Managing Director.
- To regularly attend Board and other important meetings, corporate events and participate effectively and with commitment in Board assignments.
- To keep well-informed about Bank matters, be well-prepared for meetings and actively participate in annual evaluation and planning activities.
- To build a collegial working relationship with other members of the Board.

**Requirements**

- Experience in Legal, Insurance, ICT and FinTech.
- Expertise in Management, Banking including Credit experience.
- No criminal record.
- No involvement as a member of the Management or Board of Directors with a banking institution whose registration or license has been revoked or cancelled or which has gone into liquidation.
- Clean credit record, including that of related parties.
- No history of bankruptcy.
- Multi-skilled candidates with legal knowledge and experienced practitioner in fintech and insurance will have an added advantage.

**Mode of Application**

Qualified and experienced candidates are requested to apply with the following:

- An application letter detailing your suitability for the position.
- A comprehensive Curriculum Vitae (CV).
- Certified copies of relevant academic and professional certificates and awards.
- Certified copies of your current Passport (last two pages).
- Three recent passport size photographs.
- Letters from 3 referees.
- Declaration of indebtedness to Banks.

**PLEASE NOTE**

- The applicant should not be a shareholder of CRDB Bank PLC, an employee of a shareholder or have a relationship to the Management or the Board.
- Only successful candidates will be contacted.
- Upcountry candidates will be required to meet their own travel and accommodation costs for any interviews.

Interested candidates are invited to send their application in hard and soft copies to:

**COMPANY SECRETARY**
**CRDB BANK PLC**
**P. O. Box 268**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Email: john.rugambo@crdbbank.com**

**The deadline for the application is close of business on 26th March, 2019.**

215110902

# Waliolipwa fedha korosho kuanikwa

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameagiza kubandikwa kwa majina ya wakulima wote waliolipwa fedha za korosho ikiwa hatua ya kuondokana na taarifa potofu zinazotolewa na baadhi yao kuwa hawajalipwa.

Amesema baadhi ya wakulima wamekuwa wakidai kuwa hawajalipwa fedha kutokana na kuuza korosho wakati si kweli na kwamba watu wa namna hiyo wanaichafua serikali. Hasunga alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwenye kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

"Nashangaa sana kila mkulima akiulizwa anasema hajalipwa jambo hili si kweli. Nadhani wanafanya hivi kukwepa madeni wanayodaiana huko vijijini. Sasa naitaka timu ya wataalamu wa Operesheni Korosho kuhakikisha majina yote ya wakulima waliolipwa yanabandikwa kwenye ofisi za vijiji," alisema.

Katika kutekeleza hilo, aliwataka wataalamu hao kubandika majina ya watu wote waliolipwa na kiasi cha fedha walizolipwa.

"Mpaka sasa tani 222,684 zimekwishakusanywa na hadi Machi 14, mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 596.9 kati ya Sh. bilioni 722 zilikuwa zimeshalipwa kwa wakulima, lakini nashangaa wakulima wanasema hawajalipwa, hii si sawa," alisema Hasunga.

Waziri Hasunga pia alisema serikali imejipanga hadi Machi 31, mwaka huu, kuwalipa wakulima wote waliobaki kwa kuwa uhakiki umekamilika kwa kiasi kikubwa.

Alisema serikali inapaswa kuungwa mkono kwa uamuzi mgumu iliochukua kwenye korosho kwa kuamua kuwalipa wakulima Sh. 3,300 kwa kila kilo.

Kadhalika, Hasunga alielezea kufurahishwa na mkoa wa Mtwara ambao unazalisha karibu nusu ya korosho zote nchini lakini una idadi ndogo ya wafanyabiashara wa korosho wanaokiuka sheria, maarufu kama 'kangomba' kulinganisha na Lindi yenye idadi kubwa.

"Nashangaa sana mkoa wa Mtwara una kangomba 10, lakini ndio wazalishaji wakubwa wa korosho huku mkoa wa Lindi ambao unafuatia kwa uzalishaji wa korosho ukiwa na idadi kubwa ya kangomba ambao wako zaidi ya 400," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, alimpongeza Waziri Hasunga kwa kuanzisha usajili wa wakulima nchini.

"Nakupongeza sana waziri kwa hili lakini hakikisha unalisimamia kwa weledi ili liwe na matokeo chanya na wakulima kutambulika kote nchini kwa kuwa kufanya hivyo serikali itakuwa na uwezo wa kuwahudumia kwa ufasaha," alisema.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, wakiongozwa na Dk. Ishengoma wameanza ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Mtwara kukagua miradi ya maendeleo katika sekta za kilimo, mifugo na maji.

# Mkakati wa CCM kuchukua majimbo, ngome za upinzani

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kiliambulia majimbo manne kati ya 10 ya Mkoa wa Dar es Salaam katika Uchaguzi Mkuu uliopita, sita yakichukuliwa na wabunge kutoka vyama vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Tayari chama tawala kimefanikiwa kuyarejesha majimbo mengine matatu ya Kinondoni, Ukonga na Temeke baada ya waliokuwa wabunge wake kujiuzulu uanachama wao kwenye vyama vya upinzani na kuhamia CCM ambako walipewa tena nafasi ya kuwania ubunge.

Wakati vyama mbalimbali vya siasa nchini vikijipanga kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu ujao, Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Dar es Salaam, umezindua kampeni ya 'Dar es Salaam ya Kijani' yenye lengo la kuirudisha chama tawala mitaa na majimbo yaliyokwenda upinzani.

Kampeni hiyo inalenga kuweka mkakati kwa kuanzia ngazi za jumuiya zote za mkoa huo kujipanga kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Agosti, mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika Chuo Kikuu Kishirikishi cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Dar es Salaam, Mussa Kilakala, alisema wanaamini kampeni hiyo itachochea ustawi zaidi wa CCM katika Mkoa wa Dar es Salaam.

"Leo (jana) tunazindua kampeni yetu ya Dar es Salaam ya Kijani kuelekea serikali za mitaa mwaka huu. Ni kampeni kabambe kwa ajili ya kuirejeshea CCM mitaa iliyopotea katika uchaguzi uliopita ambayo itatusaidia kupata ushindi mkubwa kimkoa katika Uchaguzi Mkuu mwakani kwenye udiwani, ubunge na urais.

"Sote ni mashuhuda kwamba katika uchaguzi uliopita wa 2014 wa Serikali za Mitaa na ule mkuu wa 2015, tulipoteza baadhi ya mitaa, kata na majimbo yaliyokuwa yakishikiliwa na CCM.

"Na sababu za kupoteza huko zinajulikana, sina haja ya kuzirejea sasa. Hivyo, sisi vijana wa CCM tunatambua kuwa ndiyo damu na roho ya chama chetu, na kwamba tunao wajibu wa asili wa kusafisha njia katika kutimiza malengo ya uwapo wa vyama vya siasa kikatiba ya kushika dola," Kilakala alisema.

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# PM awafunda maofisa habari

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka maofisa habari, uhusiano na mawasiliano serikalini kujitathmini kuhusu walivyotekeleza wajibu wao na kutafakari njia bora ya kuyatangaza na kuyatetea mafanikio ya mageuzi yanayoendelea nchini.

Pia, aliwataka kuhakikisha wanatumia vizuri taaluma zao na nyenzo wanazopatiwa kusema mambo yanayofanywa kwenye sekta zote ili kuepuka upotoshaji kwa wapinga maendeleo.

Aliyasema hayo jana, katika ufunguzi wa kikao kazi cha 15 cha maofisa hao, kinachofanyika jijini Mwanza na kuhudhuriwa na maofisa hao wapatao 400.

Aliwataka maofisa hao kuueleza umma masuala yanayofanywa na serikali hususan katika kipindi hiki ambacho serikali inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021), wenye kuweka msisitizo kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda.

"Mkumbuke kuwa kazi ya utoaji taarifa kwa wananchi kwa sasa si utashi binafsi wa mtoa habari, bali kufanywa kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi. Mathalan Sheria mpya ya Haki ya Kupata Taarifa Na. 12 ya mwaka 2016, yenye kuzitaka mamlaka za umma kuwapa wananchi taarifa zinazowahusu," Waziri Mkuu alisema.

Alisema sheria hiyo, inaendana na sheria nyingine ya kumlinda mwananchi asilishwe taarifa za uongo, uchochezi na uzushi yaani Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari Na. 12 ya mwaka 2016.

Alisema lengo la katiba na sheria hizo mbili, ni kuwahakikishia wananchi haki ya kupata habari zilizothibitishwa kwa maana ya usahihi na kwa wakati. "Sababu hizo, ndizo zilizofanya niguswe sana na kaulimbiu yenu isemayo: "Utoaji habari sahihi na kwa wakati ni chachu katika kuifikia Tanzania ya kipato cha kati".

Aidha, Waziri Mkuu alipongeza kazi zinazofanywa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (hususan Idara yake ya Habari - MAELEZO) na timu za habari za viongozi wakuu kama mawaziri, wakuu wa mikoa na watendaji wengine.

Alisema ameguswa na baadhi ya mada zitakazojadiliwa katika kikao kazi hicho, ikiwamo ya namna ya kushughulikia habari za uongo, kutunga, kughushi na namna kada yao inavyoweza kusaidia kukidhibiti kichochoro hicho haramu katika habari.

Aliwataka viongozi na watendaji wote wa taasisi za umma, kuanzia sasa washirikiane na maofisa wa habari kwenye maeneo yao kuhakikisha habari muhimu kwa wananchi hazizuiwi kwa urasimu kama hazijazuiwa kisheria. Habari zitolewe kwa haraka na kwa njia anuai za kisasa.

Alimwagiza Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, afuatilie uzinduzi wa tovuti za halmashauri walioufanya jijini Dodoma Machi 27, 2017, kama zinafanya kazi ipasavyo. Alisema lengo la tovuti hizo ni kuiongezea serikali uwezo wa kuwapatia wananchi habari na taarifa kwa haraka kuzingatia wako katika kipindi muhimu cha mageuzi katika historia ya nchi na mambo mengi yanafanyika serikalini ya kiuchumi na kijamii, lakini hayafikishwi kwa wananchi.

"Kuhusu hili, naiagiza Wizara ya Habari kufanya tathmini ya mara kwa mara na kuniletea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu yenu na matakwa haya ya kisheria miongoni mwa wizara, taasisi za umma na sekretarieti za mikoa na halmashauri mbalimbali nchini."

Waziri Mkuu ametaja mapinduzi makubwa yaliyofanyika kwenye kila sekta nchini ikiwamo elimu; afya; nishati; mifugo; viwanda; barabara; viwanja vya ndege; uchukuzi wa anga; uchukuzi wa reli; uchukuzi wa majini; madini; sanaa za filamu na muziki; utalii na michezo mbalimbali na kuwataka maofisa hao kutangaza mageuzi hayo.




Balozi wa Uswisi nchini, Florence Tinguely, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu wiki ya kuadhimisha lugha na utamaduni wa Kifaransa katika nchi zinazoongea lugha hiyo, ambapo imehusisha balozi 13 wanaowakilisha nchi zao hapa nchini. Wengine kutoka kushoto ni Balozi wa Ubelgiji, Peter Van Acker, Balozi wa Ufaransa, Frédéric Clavier na Balozi wa Morocco, Adid Benryane. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Wagoma kupinga bajaj kubeba abiria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMO wa madereva na makondakta wa daladala umesababisha kero kwa wakazi wa Jiji la Mbeya baada ya kukosa huduma ya usafiri ya kuwafikisha sehemu mbalimbali.

Mgomo huo ulianza jana, ukihusisha madereva wa daladala wanaoipinga pikipiki za magurudumu matatu (bajaj), kutoa huduma kwenye barabara kuu na njia nyingine ambazo zimeainishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra), kwa ajili ya usafiri wa daladala.

Wakizungumza na Nipashe jana, baada ya kuanza mgomo huo, baadhi ya madereva wa daladala walisema kuwa wameamua kusitisha huduma ya usafiri katikati ya Jiji la Mbeya kutokana na hatua ya serikali kushindwa kuziondoa Bajaj kwenye barabara kuu.

Mmoja wa madereva hao, Innocent Dawala, alisema kuwa kitendo cha serikali kushindwa kuziondoa Bajaj kwenye njia zinazotumiwa na daladala kinasababisha biashara yao kuwa ngumu kwa vile wanalazimika kunyang'anyana abiria.

"Serikali iliamua kuondoa Hiace ambazo zinabeba abiria 15, wamiliki wakaamua kukopa na kununua Coaster ambazo sisi madereva tunaziendesha tukitumia mafuta mengi kutoka stend kuu hadi Igawilo, lakini ndani tunabeba abiria wachache ambao hawawezi kurudisha gharama zetu," Dawala alisema na kuongeza:

"Lakini njiani tunaongozana na Bajaj nyingi ambazo pia zinabeba abiria na kuwapeleka huko huko tunakoenda sisi, sasa tunajiuliza kama waliamua kuondoa Hiace za abiria 15 kisha wanaruhusu Bajaj za abiria wanne hii ndio kuboresha usafiri wa Jiji la Mbeya?" Alihoji Dawala.

Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria (Chakua), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Stanford Mwambogela, alisema mgomo huo unaathiri haki za abiria na kwamba mamlaka zinapaswa kuzingatia sheria za nchi katika sekta ya usafirishaji.

Alisema kuwa tatizo kubwa linaloathiri sekta ya usafiri hasa wa abiria jijini Mbeya ni kuingizwa kwa maslahi ya kisiasa ambayo ndio kiini cha mgomo huo.

Ofisa Mfawidhi wa Sumatra, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Daud, alikiri kuwa katika Jiji la Mbeya, pikipiki na bajaj zimezuiliwa kutoa huduma ya usafiri kwenye barabara kuu na badala yake zinatakiwa kwenda pembezoni mwa jiji.

Alisema kuwa mamlaka yake katika kuboresha usafiri katikati ya jiji imekuwa ikipinga na kuyaondoa mabasi madogo yenye uwezo wa kubeba abiria 15 na badala yake kuhamasisha na kuruhusu mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria kuanzia 25 hivyo kitendo cha bajaj zinazobeba abiria watatu hadi wanne kutoa huduma katikati ya jiji ni kinyume cha utaratibu.

# Mabalozi nchi za Kifaransa wakutana Dar

**Na Salome Kitomari**

MABALOZI wanaowakilisha nchi 14 nchini zinazozungumza Kifaransa duniani, wamekutana jijini Dar es Salaam kujadili mchango wa lugha hiyo katika maendeleo ya kiuchumi na kiutamaduni.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, mabalozi hao walisema kuanzia jana ilikuwa maadhimisho ya Wiki ya Lugha ya Kifaransa ambayo yatakwenda sambamba na shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo michezo.

Kiongozi wa Mabalozi hao, Abid Benryane, kutoka Morocco, alisema katika maadhimisho hayo kutakuwa na maonyesho ya picha, video, programu maalum, michezo mbalimbali ya kuonyesha namna gani lugha inaweza kuwaunganisha watu na kutumika kuleta maendeleo.

Alisema lugha ya Kifaransa ni ya tano duniani kwa kuzungumzwa na kwa sasa ina zaidi ya wazungumzaji milioni 300 duniani kote na ifikapo mwaka 2050 wanatarajiwa kufikia milioni 700.

Alisema lugha hiyo ni rasmi kwa nchi 32 na mashirika ya kimataifa kama Umoja wa Mataifa (UN), Nato, Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki (IOC) na Umoja wa Afrika (AU).

"Ni lugha ya kufundishia na kujifunzia kwa zaidi ya watu milioni 80 katika nchi 36 na lugha ya nne kwenye mtandao na biashara. Asilimia 59 ya wazungumzaji wa lugha hii wanaishi Afrika na inatarajiwa watafikia asilimia 80 mwaka 2050," alisema na kuongeza:

"Mwaka 2018 nchi zinazozungumza Kifaransa zilichangia asilimia 8.4 ya pato la taifa duniani na kwamba lugha hiyo inafungua milango ya ajira kwenye biashara hasa kwa Afrika na ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Naye Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema kwa Tanzania, Kifaransa kinazungumzwa na zaidi ya watu milioni 1.5 na kinatumika kwenye shule mbalimbali, hivyo kuongeza idadi ya Watanzania wanaojua lugha hiyo.

"Tanzania imepakana na nchi nne wanachama wa nchi zinazozungumza Kifaransa ambazo ni Rwanda, Burundi, Congo na Msumbuji. Mkoa wa Kigoma asilimia sita ya wakazi wake ni kutoka nchi hizo na kwa wastani wa nchi ni asilimia mbili," alisema na kuongeza:

"Kupitia Bahari ya Hindi, Tanzania inaunganishwa na Madagascar, Mauritius, Shelisheli na Comoro. Pia zipo fursa mbalimbali za Watanzania wa aina zote kujifunza lugha na kuitumia kwa maendeleo ya kiuchumi kwa kuwa kwa kutumia intaneti wamejifunza na kusoma mambo mbalimbali ikiwamo kupata fursa za ndani na nje."

# Wauzaji viumbepori wamwangukia JPM

**Na Romana Mallya**

WASAFIRISHAJI nje ya nchi viumbepori hai wamemwomba Rais John Magufuli awasaidie ili biashara hiyo iliyositishwa miaka mitatu iliyopita, irejee kwa sababu hawasafirishi wanyama bali viumbepori.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Chama cha Wasafirishaji Viumbepori Hai Nje ya Nchi (TWEA), Adam Waryoba, alisema mwaka 2016 serikali ilisitisha ghafla ukamataji na usafirishaji nje ya nchi viumbe hao.

Alisema wakati wa tamko hilo lililotolewa na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Prof. Jumanne Maghembe, walikuwa tayari wameshalipa serikalini vibali vya usafirishaji.

"Miaka mitatu ya sitisho imeisha Machi 16, mwaka huu, mchakato wa biashara kwa mwaka unaofuata huanza Oktoba na Novemba mwaka uliotanguli, lakini wizara kupitia Mamlaka ya Wanyamapori (Tawa) Februari Mosi, mwaka huu, ilitangaza leseni za biashara za mwaka huu, bila kutangaza leseni tunazofanyia biashara," alisema.

Alisema wizara haijatamka lolote kuhusu wao kuanza biashara hiyo baada ya kipindi cha sitisho kuisha.

"Waziri wa sasa wa wizara hiyo, Dk. Hamis Kigwangalla, Mei 21, mwaka jana, alilieleza Bunge kuwa serikali itaturudishia Sh. milioni 173.3 tulizo lipa lakini hadi sasa hawajafanya hivyo na hatujajua hatima ni nini," alisema Waryoba.

Alisema biashara hiyo wanayoifanya inawahusu viumbepori hai ambao ni vyura, wadudu, mijusi, ndege na tumbili.

Kwa mujibu wa katibu mkuu huyo, baada ya kulipa serikali fedha hizo, waliendelea na shughuli za ukamataji wa viumbepori hai na wakati sitisho hilo linatoka, walikuwa kwenye maandalizi ya kusafirisha.

"Ndiio maana tunamuomba Rais Magufuli atusaidie kwa sababu fedha tumelipa, viumbepori tulikamata, leseni zetu zilizotoka kabla ya kusitishwa biashara hii zilikuwa 454. Tunamwomba Rais atusaidie tuendelee na biashara hii kuliko kuendelea kupata hasara na tuko tayari kukutana naye," alisema.

Alisema biashara ya viumbepori hai ilianza kabla ya uhuru ambapo ilifanywa na wazungu kwa wanyama.

"Baada ya uhuru iliainishwa vyema kwa sharia ya uhifadhi wanyamapori ya mwaka 1974 na kufanywa kuwa ya Watanzania wazawa," alisema.

Waryoba alisema mwaka 2012 leseni za wanyama ziliondolewa kwenye biashara kwa kuwa wanapatikana kwenye hifadhi ambako utalii unafanyika.

Alisema serikali ilibakiza leseni za vyura, wadudu, mijusi, nyoka, ndege, tumbili na nyani.

"Mgawo wa biashara ya viumbepori vyote ni kwa aina zile zilizopatikana maeneo ya wazi ambako wananchi wanaishi na kufanya shughuli za kiuchumi.

Alisema tangu wakati huo hadi sasa ukamataji wa viumbepori hai inafanyika kwenye mikoa isiyozidi minane kati ya 31 iliyopo ambapo ni sawa na asilimia 26.

Mfanyabiashara wa viumbepori hai, Deodata Nsimeta, alisema sitisho hilo limemwathiri kwa sababu alikopa fedha, alikusanya viumbepori ambao waziri aliwaeleza watakwenda kuwachukua lakini hadi sasa hawajafanya hivyo.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, akisalimiana na wanafunzi ambao ni mabalozi wa usalama barabarani kutoka Shule ya Msingi Bunge, baada ya kuzindua Programu ya Usalama Barabarani 2019 na Shindano la Uchoraji kwa shule za msingi, inayoendeshwa na kampuni ya Puma Energy Tanzania Ltd, jijini Dar es Salaam jana. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy, Dominic Dhanah. **PICHA: JOHN BADI**

## Ukarabati uwanja ndege wafikia pazuri

**Na Hamisi Nasiri,** NACHINGWEA

KAZI ya ukarabati wa mradi wa kiwanja cha ndege kilichopo wilayani Nachingwea, mkoani Lindi wenye thamani ya Sh. milioni 943 umefikia asilimia 75.

Mkandarasi wa mradi huo ambaye ni Kampuni ya Makapo Construction Ltd., amefikia hatua ya G-15.

Utekelezaji wa ukarabati wa kiwanja hicho ni miongoni mwa mpango mkakati wa serikali katika kuboresha viwanja vya ndege nchini ili kuongeza thamani na tija kwenye usafiri wa anga nchini.

Injinia Mkuu wa ujenzi huo, Helifuraha Hema, alisema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa waandishi wa habari waliotembelea kiwanja hicho kuangalia maendeleo ya ujenzi.

Alisema serikali imetoa Sh. milioni 943 kwa ajili ya kufanya

INAENDELEA UK.8

## TFS yahimiza utunzaji misitu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania(TFS) umewahimiza Watanzania kuendelea kutunza misitu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho na kusisitiza changamoto zilizopo zitatuliwe kwa majadiliano na hatimaye misitu ibaki salama.

Meneja wa Rasilimali za Misitu, Dk. Masota Abel, alisema hayo juzi kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, baada ya kumalizika kwa kikao cha majadiliano kati ya maofisa wa TFS na ujumbe wa watu 15 kutoka Ethiopia ambao walikuja kujifunza namna nzuri ya utunzaji misitu.

Waethiopia hao wametoka katika taasisi mbalimbali zinazohusika na utunzaji misitu na utafiti katika nchi yao na walipata fursa ya kwenda katika maeneo mbalimbali katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Iringa na Dar es Salaam.

Dk. Abel alisema ni vyema Watanzania wakahakikisha wanatunza misitu iliyopo na kufafanua wageni hao kutoka Ethiopia wamefurahishwa na TFS inavyotunza misitu, hivyo kuwaomba Watanzania kuwa sehemu ya kila mmoja kwa nafasi yake kuitunza kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

"Ujumbe wangu kwa Watanzania watunze misitu. Tuitunze kwa kufuata taratibu zinazostahili na hata kama kuna changamoto zingine tutumie nafasi za majadiliano kutafuta ufumbuzi na hatimaye ibaki salama. Tuache kuvamia misitu na kuikata, tuache kufanya shughuli za kilimo maeneo ya hifadhi na misitu kwa ujumla.

"Tunapaswa kufahamu misitu tuliyo nayo nchini ni keki ya taifa, hivyo lazima tuitunze na ilete tija kwa ajili ya kizazi kilichopo sasa na kijacho. Kwetu TFS tutaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha misitu inabaki salama, lakini wakati huo huo wananchi nao wanalo jukumu kama hilo," alisema.

Kuhusu changamoto kubwa ambayo TFS inakabiliana nayo, Dk. Abel alisema ni ongezeko la watu ambalo linasababisha ukosefu wa nishati mbadala ya miti ambayo itakidhi mahitaji, jambo ambalo linasababisha misitu kuvamiwa na kuharibiwa.

Pia alisema ongezeko la watu limesababisha kuwe na mahitaji makubwa ya ardhi, hivyo wengi kuvamia maeneo ya misitu yaliyohifadhiwa. Pia alisema mabadiliko ya tabianchi nayo yanachoche watu kuvamia misitu kwa lengo la kutafuta ardhi yenye rutuba kwa shughuli za kilimo.

Kuhusu kwa nini Waethiopia hao wameichagua Tanzania, Dk. Abel alisema nchi hii inasifika kwa utunzaji wa mazingira, hivyo wameona ni sehemu sahihi ya kujifunza kuhusu uhifadhi wa misitu.

"Wageni wetu wamekiri na kukubali kazi nzuri ambayo inafanywa na serikali yetu kupitia TFS katika kutunza misitu. Wameeleza namna kile ambacho wamejifunza watakavyokwenda kwao kuweka mikakati itakayowawezesha kuitunza misitu yao. Ethiopa misitu yao imeendelea kuharibiwa.

Tunaweza kusema hawana misitu tena. Kwao eneo kubwa limebaki kuwa jangwa ndiyo maana wanasema hata asali yao wanafuga katika mabanda na hiyo inasababisha asali kutoka Tanzania inabaki kuwa bora na ya asili kuliko ya kwao," alisema.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua muhimu zichukuliwe kukomesha vitendo vichafu dhidi ya sifa Jeshi la Polisi

**KATIKA** siku za karibuni kumekuwa na taarifa ambazo zinaharibu taswira ya Jeshi la Polisi nchini kutokana na baadhi ya askari wake kujihusisha na vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili ya chombo hicho.

Taarifa ambazo zimetolewa hivi karibuni, si mpya bali zimethibitisha tuhuma kwamba baadhi ya askari wa jeshi hilo hujihusisha na rushwa, ujambazi na unyang'anyi wa kutumia silaha, uonevu dhidi ya raia ikiwamo vipigo na kuwabambikia makosa wananchi kama vile kesi za mauaji au kuwashikisha dawa za kulevya.

Kutokana na kuwapo kwa madai hayo, viongozi wa ngazi za juu serikalini akiwamo Rais John Magufuli, wameshatoa onyo hadharani na kuwataka wanaojihusisha na vitendo hivyo waache mara moja. Kama wahenga wasemavyo pafukapo moshi kuna moto, vitendo hivyo sasa si siri tena bali ni bayana baada ya kubainika kuwa polisi mkoani Tabora walimbambikia mfanyabiashara mmoja kesi ya mauaji.

Jambo hilo ambalo linaweza kugharimu maisha ya mtu kutokana na hukumu yake kama atatiwa hatiani, liliibuka baada ya mtuhumiwa huyo kuandika barua kupitia gazeti moja akiomba Rais Magufuli aingilie kati kutokana na jambo hilo. Mtu huyo hivi sasa yuko huru baada ya serikali kupitia vyombo vyake kufuatilia na kubaini ukweli ndani yake.

Licha ya hatua hizo kuchukuliwa na mhusika kuokoka dhidi ya janga lililokuwa likimkabili, Jeshi la Polisi lilikiri kuwa baadhi ya askari wake wamekuwa na mtindo huo wa kuwabambikia kesi raia tukio la Tabora likiwa kielelezo cha wazi.

Hilo likiwa halijapoa, limeibuka lingine ndani ya jeshi hilo baada ya askari wawili wa Kikosi cha Usalama Barabarani kuingia matatani kwa tuhuma za kuwashambulia kwa matusi na kipigo dereva wa gari na abiria wake.

Tukio hilo la aibu kwa jeshi hilo, lilianza kusambazwa juzi kwenye mitandao ya kijamii kupitia video fupi inayowaonyesha watu wawili wenye sare za polisi wa Usalama Barabarani, wakiwatukana matusi na kuwapiga dereva na abiria wake walipokuwa wakishuka kwenye gari.

Kutokana na tukio hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, aliagiza kukamatwa kwa askari hao juzi, huku akieleza kuwa wamekosa uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Katika kuonyesha kukasirishwa na kitendo hicho, Masauni alisema kitendo kilichofanywa na askari hao hakikubaliki ndiyo maana wamechukuliwa hatua, huku akibainisha kuwa kumekuwa na malalamiko dhidi ya jeshi hilo hasa kikosi cha usalama barabarani kuwabambikia madereva makosa au askari kufanya vitendo vilivyo kinyume cha mwenendo mwema wa jeshi hilo.


Malalamiko, tuhuma na vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya askari wasio waadilifu, hususan kumbambikia mfanyabiashara kesi ya mauaji na kupiga dereva na abiria, vimelifedhehesha kwa kiasi kikubwa Jeshi la Polisi.

Tunasema hivyo kwa sababu kaulimbiu ya jeshi hilo ni 'usalama wa raia na mali zao' lakini kutokana na vitendo hivyo, imeonyesha kwamba wananchi usalama wao umewekwa rehani, hivyo sehemu kubwa ya raia wameanza kukosa imani dhidi ya chombo hicho.

Ni vyema viongozi waliopewa dhamana juu ya uongozi na ustawi wa jeshi hilo, wakafanya kazi ya ziada ikiwamo kulisafisha kwa kuwaondoa wasio waaminifu na wale ambao wanachafua taswira ya chombo hicho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Motisha ndio chachu ya ufaulu kuongezeka

**MOTISHA** ina maana nyingi katika hamasa ya mwanadamu, katika mtazamo wa kusukuma kasi yake kutamani na kupenda kitu fulani.

Kuna ushahidi mwingi kwamba katika eneo na mazingira ya aina yoyote yale, mtu anapopata msukumo wa motisha, basi anasimamia katika kasi na mwamko mkubwa wa kuwajibika kikazi au shughuli aliyo nayo na daima mabadiliko hushuhudiwa.

Motisha inaweza kupatikana katika sura nyingi; ama kwa maneno, pesa na zawaida ya aina nyingine popote, ambayo inaugusa utashi binafsi wa mtu.

Hilo ndilo mtu akirudia katika mustakabali wa maana hiyo ya motisha katika masomo shuleni ambako wamejaa wanafunzi wa umri mdogo, basi kila inapotolewa motisha hizo, inawasaidia sana walimu na wanafunzi kubadilika kielimu.

Ukizungumzia motisha kwa wanafunzi, hii inawasaidia wanafunzi kujituma kusoma na kufanikisha hata ufaulu kuongezeka kila mwaka.

Motisha inapotolewa kwa wanafunzi, unawapa matarajio ambayo ndani ya utashi wake wa uanafunzi, mhusika huyo anaguswa nayo.

Mara nyingi tu tumekuwa tukiona baadhi ya shule zinafanya vizuri katika mitihani yao na katika orodha zinazotajwa kufikia mafanikio hayo, motisha kwa walimu na wanafunzi ina nafasi yake.

Motisha zinapotolewa na wamiliki wa shule au viongozi wa maeneo jirani, wazazi na walezi wanaohusika moja kwa moja au wako jirani na mustakbali huo, wote kwa pamoja wanaguswa iwe kwa kuiga kushiriki moja kwa moja.

Inasikitisha sana tunapoona baadhi ya wazazi, wanashindwa hata kuwapa watoto wao motisha na pesa wanapokuwa nazo, pindi wanapofanikisha taaluma.

Katika baadhi ya maeneo, pesa zilizopo hasa katika jamii zinazokumbatia aina fulani za tamaduni, si cha kushangaza kuona kiasi chote cha pesa kinaingizwa katika shughuli za utamaduni wa ngoma.

**Tukipanua maana ni kwamba hata viongozi wa serikali ya mtaa, wakiwamo madiwani na wengineo wanapaswa kujenga utamaduni wa kutoa motisha kwa wanafunzi na walimu wa kata zao.**

Hapo hapo, pia inasikitisha kumuona mzazi anashindwa kumpa mtoto wake zawadi, pindi anapofanya vizuri masomoni, lakini pesa anazokuwa nazo anazipeleka ngomani kwa mambo yasiyo na tija kwa mwenendo wa maisha yake.

Katika hilo, kuna busara zote zinazopaswa kuelekezwa kwa walimu kupewa haki hiyo kutokana na kutoa mchango mkubwa katika sekta ya elimu.

Tukipanua maana ni kwamba hata viongozi wa serikali ya mtaa, wakiwamo madiwani na wengineo wanapaswa kujenga utamaduni wa kutoa motisha kwa wanafunzi na walimu wa kata zao.

Kutolewa motisha hizo kuna maana kubwa katika saikolojia ya mwalimu, kuelekea kupatikana matokeo mazuri shuleni.

Matokeo mazuri, siku zote ni zao la motisha na juhudi za moja kwa moja kwa anayefundisha na anayefundishwa.

Pia, nikienda mbali zaidi, juhudi hizo za moja kwa moja zinapatikana katika sura ya uwajibikaji wa pande hizo mbili; mwalimu na mwanafunzi.

Wanafunzi wanapofanya mitihani, wakafaulu na wakapewa motisha stahiki, daima itasaidia kuboresha sekta ya elimu katika eneo tajwa.

Tumekuwa tukiona shule zinafanya vibaya, uongozi unakutana na kujadili nini kifanyike. Baada ya kugundua kufanyika, ndio hapo motisha zinaanza kutolewa kwa wanafunzi husika.

Motisha tumekuwa tukiziona katika sura ya madaftari, pesa taslimu na wengine kupewa punguzo la ada na hata kusoma bure.

Sasa tukiifanya katika mtazamo wa kanuni, ni jukumu la wazazi kuhakikisha wanawapa watoto motisha na sio kutegemea wafadhili au viongozi wengine.

# BARUA & MJADALA

## 'Supermarket' ziboreshwe

***Mhariri***

*NITOE pongezi katika sehemu nyingi katika mji wetu kuwa na maboresho katika mifumo yetu ya manunuzi, hasa nikiona katika maeneo tofauti kuna maduka ya kisasa, maarufu kama 'supermarket.'*

*Hoja yangu kuu iko jijini Dar es Salaam, ambako kumetanuka kwa kiasi kikubwa, kwa wakazi lukuki, hali inayofanya hata mahitaji ya kila siku ya wakazi wake yana mengi sana.*

*Hivyo, niseme maboresho hayo ya kuwa na 'supermarket' nyingi ni mageuzi makubwa katika historia nchini, ambayo katika sura ya pili ya kimaendeleo mbali na kuboresha mfumo wa manunuzi, ni kwamba inarahisishia serikali mazingira ya kukusanya kodi yake.*

*Makusanyo bora ya kodi hizo, ndiko ambako Rais Dk. John Magufuli, anakoangazia, kwa kuwa inajulikana kwamba kodi ndio msingi wa serikali yoyote duniani.*

*Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alishasema kwamba serikali yoyote ile ambayo ni dhaifu, sifa yake kuu iko katika udhaifu wa kukusanya kodi.*

*Niseme, mbali na hayo maduka ya kisasa makubwa yanayojulikana hapa jijini, yapo mengine mengi madogo maarufu kama 'mini supermarket' ambayo mengi nikiingia katika huduma zake hazijafikia viwango vikubwa, hivyo rai yangu ni kwamba katika kwenda katika dunia hii ya ushindani, wahusika hao wanahitaji kujiimarisha.*


*Pia, ushauri huo nausogeza katika masoko makubwa ambako ndiko kunapatikana bidhaa nyingi za vyakula, ambavyo kimsingi ndio msingi wa maisha ya umma uliko, kwamba unatulisha.*

*Huko kuboreshwe, kwa kuwa masoko ya Dar es Salaam, hali ya uchafu ni mbaya zaidi.*

***Abudi Shabani, Chanika, Dar es Salaam***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Jamani, tuwe makini na haya ya zebaki katika samaki

**Na Salome Kitomari**

**HIVI** karibuni habari iliyogonga vichwa vya habari, ni samaki tani 11 wenye thamani ya Sh. bilioni 66 wenye sumu waliokamatwa jijini Dar es Salaam, kabla ya kuingia sokoni, wakiwa wametokea nchini China.

Samaki hao walikamatwa wakiwa kwenye kontena lenye urefu wa futi 40, lililoingizwa nchini kwa njia zinazodaiwa za panya na baada ya kupimwa, walibainika kuwa na kiasi kikubwa cha sumu ya zebaki, ambayo kwa mwili wa binadamu ni sumu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, anasema madhara ya sumu zilizobainika katika samaki hao, husababisha baadhi ya magonjwa kama saratani, matatizo ya mfumo wa uzazi, kuzaliwa watoto wenye upungufu wa akili na kusababisha vifo.

Kukamatwa kwa shehena hiyo na aina ya sumu iliyokamatwa, imenifanya nikumbuke kinachoendelea kwenye maeneo ya wachimbaji wadogowadogo ambako zebaki hutumika pasipo kujali madhara yake.

Zebaki hutumika kusafishia (kuchenjua) madini ya dhahabu na bila kujali madhara ya kiafya, baadhi ya wananchi wanatumia bila kinga yoyote kwa kuwa wanatafute kipato.

Mfano ambao umeshaelezwa sana na kuandikwa ni mkoani Geita, ambako wananchi hasa kinamama huenda na watoto wadogo kwenye maeneo ya wachimbaji, kwa ajili ya kuchenjua dhahabu ili kujipatia fedha na madhara wanayoyapata huwa ni makubwa.

**Imethibitishwa kuwa, sumu hiyo ni mbaya ikiingia kwenye mwili wa binadamu, kwa uthibitisho wa samaki waliokamatwa hivi karibuni ni wazi kuwa inapaswa kuchukua hatua katika kudhibiti matumizi ya plastiki.**

Katika taarifa ya mwaka juzi iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Kimataifa, utafiti uliofanyika mkoani Geita ulionyesha madhara wanayoyapata wachenjuaji wa dhahabu ambao hufanya kazi hiyo bila kinga yoyote, yaani hushika zebaki kwa mikono. Licha ya utafiti huo, lakini hata leo bado katika mkoa huo na mingine, wananchi wanachenjua dhahabu kwa kutumia mikono na moja kwa moja inakwenda kwenye miili yao na kuwa na madhara ya muda mrefu.

Kwa uthibitisho kuwa zebaki ikiingia kwenye mwili wa binadamu ina madhara ya magonjwa ambayo waziri ameyataja, basi Tanzania itakuwa moja ya nchi ambayo wananchi wake wengi wana madhara yanayotokana na matumizi ya kemikali hizo; kuchenjua dhahabu kwa ujira mdogo sana.

Lazima, tujiulize sumu hiyo ilipenyaje kwenye mnofu wa samaki, ni wazi kuwa ni kupitia chakula anachokula samaki na maji, kwa kuwa shughuli za kuchenjua dhahabu hufanyika wakati mwingine kwenye mikondo ya maji ambayo hutumiwa na binadamu na viumbe wengine, mwishowe huingia kwenye mfumo wa binadamu.

Mwezi uliopita, Ubalozi wa Ufaransa uliandaa mjadala wa jinsi takataka za nailoni zinavyochafua mazingira ya nchi kavu na bahari, na katika mjadala wataalamu walieleza utafiti uliofanywa katika Ziwa Victoria kwa samaki kukutwa na vipande vya plastiki kwenye minofu, ambavyo moja kwa moja huenda kwenye mwili wa binadamu anapokula samaki.

Mmoja wa wataalamu alieleza kuwa utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), mkoani Morogoro, ulibaini kati ya samaki 40 walipimwa asilimia 20, walikutwa na vipande vya plastiki kwenye matumbo yao.

Kwa upande wa bahari, nako kuna kiwango kikubwa cha uchafuzi wa mazingira kwa pastiki ambazo huishi kwa zaidi ya miaka 500 kusambaa kutokana na kutupwa ovyo, jambo ambalo huleta madhara kwenye mwili wa binadamu na mazingira kwa ujumla.

Kwa msingi huo, kwamba samaki wenye sumu ya zebaki wamekamatwa nchini, maana yake inapaswa kuimarisha mifumo yetu kwa kuwa haijulikani ni samaki kiasi gani waliingizwa au wameshaingizwa nchini kwa njia za panya na kwenda kwa walaji moja kwa moja.

Ni vyema hatua za kudhibiti sumu zote ambazo moja kwa moja zina madhara kwa afya za wananchi, mfano kwenye migodi sumu hiyo inatumika kwa uwazi pasipo kificho na vimelea vya simu hupenya kwenye mwili wa binadamu, kwa namna nyingi.

Imethibitishwa kuwa, sumu hiyo ni mbaya ikiingia kwenye mwili wa binadamu, kwa uthibitisho wa samaki waliokamatwa hivi karibuni ni wazi kuwa inapaswa kuchukua hatua katika kudhibiti matumizi ya plastiki.

Mapambano ya matumizi ya plastiki kwa kiasi kikubwa imefanikiwa Zanzibar na Kenya, ambazo ni marufuku kutumia nailoni nyepesi na ukikamatwa utachukuliwa hatua za kisheria na utawajibika kulipa faini kubwa.

Hapa Tanzania Bara, hakuna mafanikio ya moja kwa moja katika suala hilo.

Kama imeshathibitishwa kuwa zebaki ni sumu yenye madhara kwa binadamu, matarajio ya wengi ni kuwa kukabiliana nazo ni lazima hatua zichukuliwe kuanzia ngazi zote na eneo kubwa ni eneo la uchumbuaji wa madini, hasa kwa wachimbaji wadogo.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Maalim Seif aitikisa CUF

INATOKA UK. 2

wilayani hapa pia walionekana wakichana na wengine kuchoma moto kadi za uanachama wa chama hicho muda mfupi baada ya Maalim Seif kutangaza kukihama CUF. Jumbe aliahidi kuzungumza na waandishi wa habari jijini hapa leo ili kutoa idadi kamili ya wanachama wa CUF walioamua kumfuata Maalim Seif ACT-Wazalendo.

**SABABU ZA KUHAMA**

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema ameamua kuondoka CUF kwa kuwa hana tena muda wa kulumbana.

"Natangaza kwamba mambo ya malumbano yamekwisha, sasa ni mapambano ya kujenga siasa, malumbano hatuna haja nayo tena," Maalim Seif alisema na kuongeza:

"Ninakiri kwamba nimetumia muda mrefu sana kuijenga CUF, na ni kweli nyumba ukiizoea, kuihama ni tabu, lakini tukumbuke kwamba hata wakati mwingine tunazaa watoto tunaowapenda lakini Mwenyezi Mungu anawachukua na maisha yanaendelea."

Maalim Seif alisema kuwa kabla ya kufikia uamuzi huo wa kutimkia ACT, alitembelea baadhi ya vyama na kuwauliza kama vilikuwa tayari kumpokea.

"Kabla ya kuchukua maamuzi haya, tulitembelea baadhi ya vyama ili kuwaambia ikitokea sisi tumehama CUF, wako tayari kutukaribisha na kwa masharti gani, kuna mmoja alituambia kwamba yuko tayari kutukaribisha, lakini masharti je, tunaweza?

"Baada ya hapo tulikaa na kuchambua, tukaona kwamba ACT-Wazalendo masharti yao siyo magumu na tulisoma katiba yao, tukaona kwamba inatufaa.

"Sasa malumbano yamekwisha, sasa hivi ni kujenga, kama wanataka kuchukua ofisi na mali zao waende wakachukue, lakini ofisi nyingi za CUF ni za watu binafsi, walituazima majengo, sasa ni uamuzi wa wenye majengo na si letu tena," Maalim Seif alisema.

Mwanasiasa huyo mzoefu alisema yuko tayari kuwa mwanachama wa kawaida ndani ya ACT na haangalii nafasi aliyokuwa nayo ndani ya CUF.

"Sisi tumetafuta mahali ambapo tunaamini tutaendeleza mapambano ya siasa, hatuangalii vyeo, niko tayari kuwa mwanachama wa kawaida mradi mapambano ya kisiasa yaendelee.

"Wale wanaohama vyama na kutaka vyeo hawana nia ya kupambana kisiasa. Kwetu sisi kuhama na nyazifa zetu haina shida.

"Kauli yangu kwa wanachama wa CUF na Watanzania wote, kwamba wakati ni sasa wa kushusha tanga na kupandisha tanga, safari iendelee, mzigo wa CUF tumeutupa, hatuna habari tena na chama hicho, mambo yamekwisha na sasa ni kusonga mbele.

**HATIMA WABUNGE CUF**

Alipoulizwa kuhusu hatima ya wabunge wanaotokana na chama cha CUF wanaomuunga mkono, Maalim Seif alisema wataendelea kuwa wanachama wa chama hicho.

"Wabunge wataendelea kuwa wanachama wa CUF, tumewaachia wao isipokuwa wakiamua kujiunga na ACT-Wazalendo ni wao, kama wataamua kubaki hukohuko pia ni sawa, sisi hatuna uamuzi juu yao," Maalim Seif alisema.

Aliongeza kuwa yuko tayari kushirikiana na vyama vingine katika kuendeleza mapambano ya kisiasa nchini.

"Tuko tayari kushirikiana na vyama vyote makini, kama ni Ukawa (Umoja wa Katiba ya Wananchi) au hata kama utabadilika, mradi ni vyama makini, tutashirikiana navyo," Maalim Seif alisema.

CUF imekuwa katika mgogoro wa uongozi tangu mwaka 2015, Prof. Lipumba alipoandika barua ya kujiuzulu nafasi ya uenyekiti wa chama hicho akieleza kutofurahia uamuzi wa Ukawa kumpa nafasi Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa kuuwakilisha kusaka kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu uliopita.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa uchumi alirejea kwenye chama hicho baada ya uchaguzi huo na kutangaza kutengua barua ya kujiuzulu kwake, huku uamuzi wake ukipata baraka za Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini. Ukawa uliundwa na vyama vinne ambavyo ni Chadema, CUF, NCCR – Mageuzi na NLD.

**MAALIM SEIF NI NANI?**

Seif Sharif Hamad, maarufu kama Maalim Seif, alizaliwa OKtoba 22, 1943) na sehemu kubwa ya maisha yake amekuwa mwanasiasa ndani ya CCM na CUF. Yafuatayo ni matukio yake ya kumbukumbu;-

- Mwaka 1950 hadi 1957 alisoma Shule ya Msingi Undowe na baadaye Wete Wavulana.
- Mwaka 1958 alijiunga na elimu ya sekondari katika Shule ya King George VI Memorial, Zanzibar na kumaliza kidato cha nne mwaka 1961. Aliendelea na masomo ya kidati cha tano na cha sita katika shule hiyo mwaka 1962 hadi 1963.
- Mwaka 1964 hadi 1972, alifanya kazi ya ualimu katika shule mbalimbali za sekondari.
- 1972 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa masomo ya shahada ya kwanza ya Sayansi Jamii katika masuala ya Sayansi ya Siasa, Utawala na Uhusiano wa Kimataifa.
- Alitumikia nafasi ya Waziri wa Elimu katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) mwaka 1977 hadi 1980.
- Ni mmoja wa waanzilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na alikuwa mjumbe mwaka 1980 hadi 1989 na Mbunge mwaka 1977. Pia alikuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM mwaka 1977 hadi 1987.
- Mkuu wa Idara ya Uchumi na Mipango ya CCM mwaka 1982 hadi 1987.
- Waziri Kiongozi wa SMZ kuanzia Februari 6, 1984 hadi Januari 22, 1988. Baada ya kuondolewa katika nafasi ya Waziri Kiongozi, alifukuzwa uanachama wa CCM.
- Mei 1989 hadi Novemba, 1991 aliwekwa kizuizini.
- Mwaka 1992 wakati kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, Maalim Seif na wanachama wengine waliokuwa CCM walianzisha Chama cha Wananchi (CUF).
- Mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 na 2015 aligombea urais wa Zanzibar kupitia CUF na safari zote akishika nafasi ya pili nyuma ya wagombea wa CCM, Dk. Salmin Amour Juma, Amani Abeid Karume na Dk. Ali Mohamed Shein.
- Mwaka 2010 hadi 2015 alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar baada ya muafaka wa kumaliza mpasuko wa kisiasa uliokuwa umevikumba visiwa hivyo.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya (DAR), Rahma Suleiman (ZANZIBAR) na Dege Masoli (TANGA).***

## Mbunge mwingine upinzani matatani

INATOKA UK. 2

mbunge kutokana na kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Bunge.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Spika Ndugai amemwandikia barua Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, kumwarifu kuwa Jimbo la Arumeru Mashariki liko wazi.

Taarifa ya Bunge ilibainisha kuwa Jimbo la Arumeru Mashariki linaloongozwa na Nassari aliyedhaminiwa na (Chadema) liko wazi kutokana na Mbunge huyo kupoteza sifa. Vilevile taarifa hiyo ilisema Nassari amepoteza sifa hiyo kwa kutohudhuria mfululizo mikutano ambayo ni mkutano wa 12 wa Septemba 4 hadi 14, mwaka 2018, mkutano wa 13 wa Novemba 6 hadi 16 na mkutano mwaka 2018.

Pia taarifa hiyo ilisema Nassari hakuhudhuria mkutano wa 14 uliofanyika kuanzia Januari 29 hadi Februari 9, mwaka huu.

"Uamuzi huu wa Spika umezingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 71 (1) (c). Ibara hii inaeleza kuwa, 'Mbunge atakoma kuwa Mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge ikiwa atakosa kuhudhuria vikao vya mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Spika," ilisema.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Ibara hiyo imefafanua katika Kanuni ya 146 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari 2016.

"Kanuni hiyo inaeleza kuwa, 'Kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati zake ni wajibu wa kwanza wa Mbunge, Mbunge yeyote atakayeshindwa kuhudhuria mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ruhusa ya Spika iliyotolewa kwa maandishi, atapoteza ubunge wake na Spika ataiarifu NEC," ilisema.

## Mkakati wa CCM kuchukua majimbo

INATOKA UK. 3

Alisema CCM inahitaji ushindi mkubwa kwa kuweka mikakati ya awali kwa kuwahusisha wanachama wa chama hicho kwa ngazi zote.

"Kampeni yetu hii itashuka katika wilaya, kata na matawi yote katika mkoa wetu ili kuwa na ufahamu wa pamoja na kuhakikisha kila kijana wa UVCCM anawajibika ipasavyo kuhakikisha falsafa ya Dar es Salaam ya kijani, yaani Dar es Salaam ya CCM inaenea kwa wanachama na wananchi ili ikifika wakati wa uchaguzi, tuvune wapigakura wa kutosha," alisema.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa UVCCM, Raymond Mwangwala, alisema ameridhishwa na kasi kubwa inayofanywa na vijana wa Dar es Salaam kuhakikisha chama kinapata heshima katika uchaguzi.

"Leo ninachokiona hapa, hii ndiyo UVCCM ninayoijua na sina shaka na uongozi wa mkoa kwa kuwa unafanya kazi kubwa na nzuri, ninachoweza kusema kwenu ninawaomba sana vijana tukilinde chama na kuhakikisha tunapata ushindi katika uchaguzi.

"Na ikiwezekana waachieni (upinzani) asimilia mbili tu ya mitaa na pindi ikibidi hata hakikisheni tunachukua asilimia zote 100. Vijana tushikamane na tulinde heshima ya chama chetu," Mwangwala alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
18 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 26-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dodoma kuelekea Dar-Es-Salaam**, gari hilo lenye namba za usajili: **T 324 CZS / T 387 DHQ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.84** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Dodoma hadi Dar-Es-Salaam** Kupitia Morogoro, gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215123902


## Ukarabati uwanja

INATOKA UK.5

ukarabati wa kiwanja ndege cha Wilaya ya Nachingwea ikiwa ni miongoni mwa mkakati wa kuboresha viwanja vyote vya ndege nchini ili kuboresha usafiri wa anga nchini.

Alisema shughuli za ukarabati na matengenezo ya kiwanja hicho zimefikia asilimia 75 hadi sasa.

Hema alisema serikali imeipa kandarasi ya ukarabati wa kiwanja hicho kampuni ya ujenzi ya Makapo ambayo inajenga kwa kasi kuhakikisha unakamilika ndani ya wakati.

Alisema awali walianza na kazi ya kusafisha uwanja na baadaye kuchimba na kuweka sawa udongo katika viwango vinavyotakiwa kitaaluma kwenye viwanja vya ndege nchini.

Hema alisema kiwanja hicho kupitia ukarabati huo kwa sasa kitakuwa na viwango bora vya viwanja vya ndege utakaokuwa na urefu wa mita 1,800 sawa na kilomita 1.8.

"Tunaihakikisha serikali Kampuni ya Makapo itahakikisha inamaliza mradi huo ndani ya wakati kwa kuwa tumekuwa tukifanya kazi saa zote ili kukamilisha ujenzi huu kama serikali inavyotaka na kutuagiza," Hema alisema.

## HABARI KITAIFA

# TPA yatenga mil. 50/- kusaidia maendeleo

**Na Dege Masoli,** TANGA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imetenga Sh. milioni 50 kwa Mkoa wa Tanga kuchangia shughuli za kijamii katika miji inayozunguka bandari ikiwa ni mpango wa bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deodatus Kakoko, alisema fedha hizo ni mpango wa kuchangia kupitia asilimia za mapato yake utakaotolewa katika maeneo muhimu ya kijamii kama elimu na afya.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi mabati 379 ya Shule ya Ufundi ya Tanga iliyofanyika mwishoni mwa wiki shuleni hapo, Kakoko alisema pamoja na bati hizo, Mamlaka hiyo itachangia huduma za afya Wilaya ya Pangani.

Alisema uchangiaji huo ni utekelezaji wa sera ya Bodi ya Mamlaka hiyo na pia jamii inayoishi katika maeneo hususani yaliyozungukwa na Bandari na nchi nzima itanufaika na mpango huo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TPA, Ignas Rubaratuka, alisema lengo la uchangiaji huo ni kuboresha mazingira ya shule hiyo pamoja na makazi ya walimu ili kuinua kiwango cha elimu.

Awali Mkuu wa shule hiyo, Andrew Mwakanyamale, alieleza changamoto wanazokabiliana nazo kuwa ni uchakavu wa nyumba za walimu, majengo ya shule, kantini, shule ya awali na kutokuwa na uzio jambo linalohatarisha usalama wa wanafunzi na mali za shule.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, alipongeza mpango wa mamlaka hiyo kusaidia shughuli za kijamii na kwamba Tanga umewafikia wakati mwafaka.

Mwilapwa alieleza umuhimu wa mpango wa mamlaka hiyo kuwa uchangiaji huo utarahisisha pia utekelezaji wa sera ya elimu bure na hivyo kufikia lengo la kila mtoto kusoma.

# TRA yawashtukia wafanyabiashara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

> **Kuna barua nyingi tayari ofisini kwangu na ninapokea idadi ya kuanzia barua nane hadi 10 kwa siku kutoka kwa wafanyabiashara za kuacha biashara zao.**

BAADHI ya wafanyabiashara wilayani hapo, mkoani Shinyanga, wameanza kuandika barua za kuomba kuacha kufanyabiashara, kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), huku wengi wakiingia katika mfumo mpya wa vitambulisho vya wajasiriamali vya biashara ndogo ndogo.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Meneja wa TRA Mkoa Maalumu wa Kikodi Kahama, Faustine Kayambo, wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake kuwa kwa wale ambao hawana sifa ya kupata vitambulisho ni bora wakaendelee kufanyabiashara zao na kulipa kodi ya serikali.

Alisema mpaka sasa ni zaidi ya wafanyabiashara 100 ambao wameandika barua za kuomba kuacha biashara, kati ya hao mamlaka yake iliwatembelea wawili kujiridhisha na kuwakuta na bidhaa zenye thamani kubwa ambazo haziwafanyi kuingizwa katika mfumo wa kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali.

"Kuna barua nyingi tayari ofisini kwangu na ninapokea idadi ya kuanzia barua nane hadi 10 kwa siku kutoka kwa wafanyabiashara za kuacha biashara zao, na ofisi yangu imebaini kuwa wengi wao wanakuwa na nia ya kukwepa kulipa kodi na kujiunga na vitambulisho vya wajasiriamali," Kayamba alisema.

Aliongeza: "Mpaka sasa Mamlaka imefanya msako kujiridhisha na hali hiyo na tuliwabaini wafanyabiashara wawili ambao wana vitambulisho vya wajasiriamali wadogo na tulifanikiwa kuwakamata na kuwanyang'anya na kuvirudisha kwa Mkuu wa Wilaya Anamringi Macha.

Alieleza kuwa walioandika barua za kuacha biashara majina yao yote yameorodheshwa na wanakadiriwa kuwa zaidi ya wafanyabiashara 80 hadi 100 na Mamlaka yake itawatembelea ikiwa ni pamoja na kuangalia kama wana madeni ya kodi katika siku za nyuma.

Hata hivyo, Kayambo alitoa wito kwa wanaostahili kulipa kodi ni bora wakaendelee kulipa kwa wakati na kama mitaji yao itakuwa imeyumba wanaweza kufika katika ofisi yake kwa lengo la kukadiriwa kodi upya huku akiwa katika uangalizi.

Pia alisema wenye mauzo chini ya shilingi milioni nne kwa mwaka, wanatakiwa kuendelea kuvitumia vitambulisho ambavyo vinatolewa na serikali ili kuepuka usumbufu baadaye.

Katika hatua nyingine, Kayambo alitoa onyo kwa wafanyabiashara ambao hawatoi risiti na ambao hawachukui risiti kuwa atawachukulia hatua za kisheria kwa kuwapiga faini ya shilingi milioni tatu hadi Sh. milioni 4.5 kwa ambaye hatoi risiti na Sh. 300,000 hadi Sh. milioni 1.5 kwa mteja ambaye atakuwa hajaomba risiti.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akihutubia watumishi wa ofisi yake wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi, mjini Morogoro. **NA MPIGAPIGA WETU**

# Mhagama asisitiza ubunifu kwa wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amewataka watumishi wa ofisi hiyo kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na ubunifu ili kuleta tija na utendaji wenye maendeleo nchini.

"Naamini mkutano huu unalenga kugusa maeneo yote ya utendaji kazi ikiwamo kubainisha changamoto, fursa na jinsi ya kujipanga ili kuongeza tija na ufanisi katika maeneo yetu ya kazi," Mhagama alisema.

Alisema hayo wakati akifungua mkutano wa wafanyakazi mjini Morogoro, juzi.

Aliwaeleza watumishi kuutumia mkutano huo kama chombo muhimu cha kuendelea kujadili na kuweka maazimio yanayotekelezeka kwa kuzingatia umuhimu wa chombo hicho kilichopo kisheria katika kusaidia watumishi wa umma.

"Tumieni mabaraza haya kama eneo muhimu la kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kuboresha mazingira ya kazi ili kuendelea kuwa na weledi katika kutekeleza majukumu ya ujenzi wa taifa."

Alisema matumizi sahihi ya mkutano huo ni kuona namna utavyosaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili idara, vitengo pamoja na taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo na kuwa na maoni, ushauri na mapendekezo yanayotekelezeka ili kufikia malengo waliojiwekea kwa mwaka wa fedha ujao 2019/2020.

Waziri Mhagama pia alipongeza utendaji wa watumishi wa ofisi yake hususan Idara ya Kazi inayoshughulikia masuala ya vibali vya kazi na kuendelea kuboresha mifumo na mazingira wezeshi ili kuendelea kulinda mazingira ya kazi na ajira nchini.

"Pamoja na idara zote kuendelea kufanya vyema, kipekee naipongeza Idara ya Kazi kwa mabadiliko mapya ya kiutendaji kwa kuzingatia ilikuwa idara inayotupa shida hususani upande wa vibali vya ajira, tunashukuru kwa mageuzi makubwa yaliyofanyika kwa kuwa na usimamizi mzuri na kulinda mazingira ya ajira na kuleta manufaa nchini," Mhagama alisema.

Aliwapongeza watendaji wa ofisi kwa ujumla kwa nafasi zao kwa kuwapo na mafanikio makubwa ya kiutendaji pamoja na mchango wa kila mtumishi katika utoaji wa huduma bora bila upendeleo kwa wananchi wote kwa haki na usawa.

Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Andrew Massawe, aliahidi kuendelea kusimamia maagizo na ushauri wa waziri kwa watumishi wa ofisi yake ili kuleta matokeo chanya yanayotarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika kuboresha mazingira ya utendaji kwa watumishi ikiwamo kuendelea kupambana na rushwa mahali pa kazi na kuzingatia haki na usawa kwa watumishi wote.

Alieleza kuwa uwapo wa mabaraza hayo ni kwa mujibu wa sheria na agizo Na. 1 la mwaka 1970 ambalo linaelekeza utaratibu wa kuundwa kwa mabaraza katika taasisi na ofisi za umma kwa kuzingatia sheria mbalimbali za kimataifa ikiwamo zile za Shirika la Kazi Dunia (ILO).

"Kwa kuzingatia lengo la kuanzishwa kwa mabaraza haya ni pamoja na kuona utekelezaji wa bajeti za ofisi zetu pamoja na kutoa mapendekezo katika kuboresha utekelezaji wa bajeti zetu za kila mwaka," Massawe alisisitiza.

# NHC kujenga nyumba 30,000 za bei nafuu

**Na Steven William,** MUHEZA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limepanga kujenga nyumba 30,000 za bei nafuu katika mikoa yote nchini kwa lengo la kuboresha makazi ya nyumba bora kwa watu watakaozinunua.

**NHC inajenga nyumba kwa bei nafuu na hiyo ni Ilani ya CCM chini ya Rais John Magufuli.**

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema hayo baada ya kutembelea nyumba 20 mpya zinazojengwa na NHC katika eneo la Kibanda ambazo 10 zimenunuliwa na halmashauri na 10 zingine za makazi.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii, wilayani Muheza, alisema kuwa serikali kupitia NHC imepanga kujenga nyumba hizo 30,000 kwa awamu.

Alisema kuwa NHC inajenga nyumba kwa bei nafuu na kwamba hiyo ni Ilani ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Rais John Magufuli.

Lukuvi aliagiza kuhakikisha miundombinu inajengwa katika maeneo ya miradi hiyo ya NHC kama maji na umeme ili watu watakaponunua nyumba hizo kuwe na huduma hizo.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, NHC imejenga nyumba 20 za makazi ya gharama nafuu.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Shabani Shekilindi, alisema kuwa miradi kama hiyo inakwenda vizuri.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (kulia), akitoa maelekezo kwa viongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), alipotembelea kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba zinazojengwa na shirika hilo katika eneo la Chatur Kijiji cha Kibanda wilayani Muheza jana, alipoambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Katikati ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Shabani Shekilindi na kushoto ni Naibu Waziri Anjelina Mabula. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Chanzo ongezeko mimba za wanafunzi chatajwa

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

UPANGAJI wa vyumba mitaani kwenye makazi ya watu kwa wanafunzi wa kike wilayani Kishapu, umedaiwa kuchangia ongezeko la mimba za wanafunzi na kusababisha kufukuzwa shule.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Shadrack Kengese, alitoa tahadhari hiyo wakati alipotembelea Shule ya Sekondari ya Mangu, iliyopo wilayani humo na kukuta idadi ndogo ya wanafunzi wa kike ambao wanaishi bweni, huku wengi wakiwa wamepanga vyumba kwenye makazi ya watu.

Alisema hajafurahishwa na idadi hiyo ndogo ya wanafunzi wa kike kukaa bweni wakati serikali ilitenga fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo ili kumaliza tatizo la mimba shuleni wilayani humo, lakini hali imekuwa tofauti kwa wanafunzi kuendelea kupanga nje.

"Upangaji huu wa mageto mitaani kwenye makazi ya watu ni moja ya sababu kubwa ambayo inachangia kuendelea kuwapo kwa mimba shuleni wilayani Kishapu, hivyo naombeni sana wanafunzi wa kike mje muishi hapa shuleni mahali salama," alisema Kengese.

"Nimefuatilia ili kujua sababu zipi zinakwamisha wanafunzi kuja kuishi shuleni kwenye mabweni, nikagundua ni wazazi ndiyo wanawazuia kwa sababu ambazo hazina mashiko kabisa, wakidai watakosa wasaidizi wa kazi za nyumbani ikiwamo kilimo," alisema.

Awali Mkuu wa Shule hiyo, Agness Mhando, akisoma taarifa ya shule, alisema changamoto hiyo ya wanafunzi wa kike kutokaa bweni, imesababisha mwaka jana kuwapo na wanafunzi wanane waliokuwa na ujauzito na mwaka huu tayari wanafunzi wengine watatu wa kidato cha kwanza wamefukuzwa shule sababu ya ujauzito.

Nao baadhi ya wanafunzi wakike wanaosoma shule hiyo akiwamo Aogenia Pesambili, walikiri kuishi nje ya shule na kukumbana na vishawishi vingi vya kutongozwa na wanaume, na kujikuta wengine wakiingia kwenye uhusiano na kuambulia ujauzito.

# NEMC yaitaka Tanesco kuweka mifumo ya tahadhari

**Na George Tarimo,** KIHANSI

WAJUMBE wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC), waliotembelea mradi wa kuzalisha umeme wa Kihansi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Profesa Esnat Chaggu, wameliagiza Shirika la Umeme nchini (Tanesco) kuweka mifumo ya tahadhari ya majanga ikiwamo rasmi ya utoaji taarifa kwa wananchi wanaoishi kwenye mwelekeo wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme.

Mkurugenzi wa Bodi ya NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema kutokana na uwapo wa vijiji kwenye mwelekeo wa maji ya mabwawa ya kuzalisha umeme, ipo hatari ya vijiji hivyo kukumbwa na mafuriko kama yatatokea majanga ya asili ikiwamo tetemeko la ardhi na kusababisha kubomoka kwa mabwawa na kutaka kuwapo kwa mifumo ya utoaji taarifa kwa wananchi.

Dk. Gwamaka alisema kuwa vituo vyao huwa vinafuatiliwa (GCC) kwa kuangalia maji kwa kila kituo mfano kwa siku Kidatu wanaangalia kiwango cha maji.

Naye Kaimu Meneja wa Tanesco Kihansi, Mhandisi Yona Mwasajone, alisema zipo tahadhari zinazochukuliwa na Tanesco kwenye bwawa hilo ambalo huzalisha kiasi cha megawati 180 za umeme wa gridi ya taifa akizitaja baadhi kuwa ni kuhakikisha bwawa halijai kupita kiasi huku pia akiahidi kufanyia kazi ushauri huo.

Mhandisi Yona alisema kuwa kufuatilia kila siku ni jambo muhimu kwa sababu inasaidia iwapo kutatokea tatizo kujua jinsi ya kukabiliana nalo mapema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Profesa Chaggu, amelishauri shirika hilo kushirikiana na wananchi kununua mabasi ya wanafunzi katika Shule ya Msingi Kihansi ili kutatua kero ya kutembea umbali mrefu na uhusiano na ujirani mwema na jamii.

Prof. Chaggu alisema, wanatakiwa kuungana na wananchi kwa kuwa eneo hilo ni maarufu kwa kilimo cha mpunga ni vizuri wakachangia sehemu ya mauzo kununua mabasi mawili au matatu kwa ajili ya wanafunzi hasa nyakati za mvua.

## Wafugaji wachekelea maamuzi ya serikali

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeagiza kurejeshwa kwa ng'ombe 550 za wafugaji wa kijiji cha Kimotorok, wilayani Simanjiro, iliyokuwa inashikiliwa na askari wa Pori la Akiba la Mkungunero.

Agizo hili lilitolewa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Elisante ole Gabriel, wakati akizungumza na wakazi wa eneo hilo, mwishoni mwa wiki.

Hata hivyo, alisema wafugaji wanapaswa kutambua kuwa wanatekeleza haki na wajibu wao bila kuvunja sheria za nchi lakini wasionewe.

Alisema wafugaji wanapaswa kuheshimu maeneo ya hifadhi kwa kutovunja sheria na kuingiza mifugo.

"Hatutegemei wafugaji nchini kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwa mifugo yao kukamatwa, ila wafuate maelekezo ya serikali kwa kuheshimu maeneo ya hifadhi," alisema.

Meneja wa Pori la Akiba la Mkungunero, Khadija Marongo, alisema ng'ombe 447 na punda 10 walikamatwa na askari wao baada ya kuingia ndani ya eneo lao.

Diwani wa Kata ya Loiborsiret, Ezekiel Lesenga (Mardad), aliishukuru serikali kwa kurejesha mifugo hiyo kwa wafugaji wa kijiji hicho kilichopo kwenye kata yake.

Alisema serikali imekuwa ikiwajali wafugaji hivyo kupitia nafasi hiyo wanaishukuru kwa kurejesha mifugo hiyo.

Aliongeza kuwa wafugaji hawapendi kuvunja utaratibu uliowekwa na serikali, hivyo watajitahidi kutokiuka mipaka iliyowekwa baina yao na majirani wao waliowazunguka.

Lesenga alisema hali ilikuwa ngumu kwa baadhi ya wafugaji ambao ng'ombe wao walikamatwa kwa kuwa kuna ambao walikuwa wananyonyesha ndama wao.

"Ndama nyingi ziliathirika kwa sababu zilikuwa zinategemea kunywa maziwa ya ng'ombe, lakini kutokana na mifugo hiyo kukamatwa waliteseka na njaa," alisema.

Mifugo hiyo ilishikiliwa kwa siku 10 na wamiliki wake walitarajiwa kufikishwa Mahakama ya Wilaya ya Kondoa.

# Huduma afya ya kinywa, meno kuwafikia 47,000

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHAMA cha wataalamu wa afya ya kinywa na meno, kinatarajia kutoa huduma ya usafi wa kinywa kwa watu 4,000 mkoani hapa na 47,000 nchi nzima hadi kufikia kesho.

Makamu wa Rais wa chama hicho, Deogratias Kilasara, alisema hayo jijini hapa juzi, baada ya matembezi ya uhamasishaji wa afya ya kinywa na meno kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku hiyo yatakayofanyika kesho.

Alieleza mwaka jana walitoa huduma za elimu ya afya, ushauri na matibabu kwa watu 38,000 na walipewa tuzo ya kimataifa ya "Most Educative Award" inayotolewa na Shirikisho la Vyama vya Afya na Kinywa na Meno Duniani (FDI).

Alisema kabla ya kufikia siku ya kilele watatoa huduma hiyo katika shule za zenye watu wenye uhitaji maalumu ndani ya Jiji la Arusha pamoja na kwenye Kituo cha Afya Themi.

Aliongeza kuwa kupitia utafiti uliofanywa na FDI, unaonyesha magonjwa ya fizi na kutoboka meno huwapata watu katika ya umri wa miaka 10 hadi 45, na kati ya wagonjwa hao, wanane wanakabiliwa na ugonjwa wa fizi.

**Wataalamu waliripoti magonjwa hayo kuwa na visababishi mtambuka na magonjwa mengine yasiyo ya kuambukiza (NCD).**

Alisema wataalamu waliripoti magonjwa hayo kuwa na visababishi mtambuka na magonjwa mengine yasiyo ya kuambukiza (NCD).

Aliongeza magonjwa ambayo siyo ya kuambukiza ni kama vile saratani, kisukari na magonjwa ya moyo.

Aidha, alisema kwa upande wa visababishi vya magonjwa mtambuka ni kama utumiaji wa sigara, tumbaku na ugoro, unywaji wa pombe kupita kiasi, ulaji wa vyakula hatarishi na kutokufanya mazoezi ya mwili.

Alisema magonjwa hayo yanaweza kuzuilika kwa usafishaji sahihi wa kinywa, kusafisha meno mara mbili kwa kutwa, kutumia dawa ya meno yenye madini ya floride na kumuona daktari angalau mara moja kwa mwaka.

Hata hivyo, alishauri kinga ni bora kuliko tiba kutokana na gharama za matibabu kuwa kubwa, hivyo aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kuliko kusubiri hadi tatizo linapokuwa kubwa.

Kwa upande wake, mgeni rasmi katika tukio la matembezi hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, aliwapongeza wataalamu wa shirikisho hilo kwa kuandaa matembezi hayo.

Alisema uhamasishaji kwa wanajamii ili wapate elimu ya kutunza usafi wa kinywa ni suala muhimu.

Alisema kwa kipindi cha miaka mingi, afya ya kinywa na meno imekuwa haipewi kipaumbele kutokana na wananchi wengi kuwa na uelewa mdogo wa kutokufahamu mahusiano ya magonjwa ya kinywa na meno na magonjwa mengine.

Aliongeza kwa mujibu wa taarifa za kiafya duniani zinaonyesha ongezeko la magonjwa ya saratani, watu 24 wanapoteza maisha kwa siku huko nchini Marekani.

Kwa hapa nchini, Kwitega, alisema ugonjwa wa saratani za kinywa unashika nafasi ya nne miongoni mwa magonjwa ambayo yanawaathiri Watanzania pamoja na magonjwa ya saratani ya shingo ya uzazi, saratani ya matiti na saratani ya ngozi.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Zuwena Omary (kulia), akizungumza na wakurugenzi watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Tamim Kambona (kushoto) na Yefred Myenzi, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Naibu Waziri Manyanya ataka matumizi teknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, amezitaka taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo kubuni vifaa vya teknolojia zinazoendana na soko ili watumiaji wajikwamue kiuchumi na kujiendeleza zaidi.

Alisema hayo wakati alipotembelea Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (Temdo) jijini hapa mwishoni mwa wiki, akiwa ameambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Alisema taasisi hizo zinatakiwa kuwa wabunifu katika kubuni vifaa vya teknolojia ambavyo vitawezesha kubadilisha maisha ya wananchi na mwisho wa siku kuongeza pato la serikali.

"Mnatakiwa kila wakati mje na ubunifu mpya wa teknolojia za mitambo ya kisasa inayoendana na hali ya sasa kwa kuwa mnategemewa sana katika kuzalisha mitambo ambayo itamkomboa mwananchi na kuinua kipato chake na kuondokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili," alisema.

Alisema serikali itaendelea kutoa fedha kusaidia taasisi hizo kubuni teknolojia mbalimbali kwa lengo la kunufaisha wananchi na serikali kwa ujumla.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Suleiman Saddiq, alisema kinachotakiwa zaidi katika taasisi hizo ni kuwapo kwa usimamizi mzuri na wataalamu wanaoweza kutengeneza mashine zilizo bora na kuziendesha wenyewe.

Alisema umefika wakati sasa wa taasisi hizo kufanya shughuli zao kibiashara na kuzalisha ili wapate mapato ya ndani, fedha ambazo zitawasaidia endapo fedha tarajiwa zitachelewa.

Naye Kaimu Meneja Ushauri Viwandani katika taasisi hiyo, Alexander Komba, alisema wataendelea kubuni teknolojia mbalimbali ili waweze kutimiza ndoto zao walizojiwekea.

Alisema pamoja na kuwa muda mrefu walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya raslimali fedha na mashine, serikali kwa sasa imewatatulia changamoto hiyo kwa kuwapatia fedha ambazo zimesaidia kuongeza uzalishaji.

# Askofu aonya wanaojiandaa kuvamia eneo la kanisa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, ametoa tahadhari kwa kikundi cha watu wachache kinachojiandaa kuvamia ardhi katika eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stephano Moshi (SMMUCo) kuachana na dhamira hiyo ovu.

Alikuwa akizungumza jana na wanavijiji pamoja na wanaushirika ambao ni waumini wa dhehebu hilo katika ibada mbili tofauti zilizofanyika Sharika za Hosiana na Nshara za Jimbo la Hai la Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT.

Eneo linalodaiwa kwamba kuna kikundi cha watu wachache wanaojiandaa kuvamia ekari 50 za ardhi, lilitolewa na Vyama vya Ushirika vya Nshara na Uduru kwa Dayosisi ya Kaskazini kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

"Nimesikia kwamba kuna maneno ya watu wachache au kikundi cha watu wachache ambao wanataka kuingia kwenye lile eneo, labda nichukue nafasi hii tu kuwaeleza wajue kwamba lile eneo limeshawekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Mungu, na mtu yeyote ambaye anaelewa na ni mwamini wa dini yeyote, anaelewa kitu ambacho kimeshawekwa wakfu, huwa kimetengwa kwa kazi ya Mungu.

**Kwa hiyo ilikuwa tu ni tahadhari yangu kwa yeyote ambaye amejaribiwa kwa njia moja au nyingine kutaka kuingia katika hilo eneo, aache mara moja.**

"Kwa hiyo ilikuwa tu ni tahadhari yangu kwa yeyote ambaye amejaribiwa kwa njia moja au nyingine kutaka kuingia katika hilo eneo, aache mara moja. Nimeshukuru kwamba washarika na wanakijiji wa hapa Nshara ambao ndio walitoa ardhi hii kwa hiari yao kwa kanisa, wanaelewa na bado msimamo wao ni huo huo kwamba walishatoa ardhi hii kwa ajili ya kazi ya Mungu ambayo ni kwa maendeleo, siyo ya kanisa tu, bali kwa maendeleo ya jamii nzima."

Askofu Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, amewasihi waumini wa dhehebu hilo kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya Rais Dk. John Magufuli katika kudumisha na kuboresha elimu nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Shoo, baada ya eneo hilo kutengwa, kanisa liliweka wakfu na kujenga mnara wa msalaba na kisha kuweka jengo moja mahali ambapo hivi sasa wanataka kujenga ghala kubwa ambalo litatumika kuanza kukusanya vifaa na kwamba kazi ya ujenzi huo itaanza mara moja mwezi huu.

Zaidi ameeleza: "Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutambua mchango wa kanisa na umuhimu wa elimu kwa maendeleo endelevu ya jamii yetu, walitupa hati miliki ya ile ardhi ambayo iko pale Makuru. Na pia napenda kuishukuru serikali yetu kwamba ilitupa kibali cha kubadilisha matumizi ya ardhi ile kutoka ardhi ya kilimo na kuifanya iwe kwa ajili ya makusudi ya elimu."

Licha ya tahadhari hiyo, Askofu Dk. Shoo ameeleza kuwa Dayosisi ya Kaskazini kwa pamoja imeamua kazi ya ujenzi wa chuo kikuu hicho ianze mwezi Machi mwaka huu na kwamba sasa anayofuraha na shukrani kwa Mungu kwamba wanayo fedha ya kutosha kuanza sehemu kubwa ya majengo katika eneo lile.

Akifafanua zaidi kuhusu kikundi hicho cha watu wachache kutaka kuvamia ardhi hiyo, Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Nshara, Rodrick Mlay alisema, "Huu upepo unaozunguka kuhusu maeneo ya kanisa, unatupa changamoto na changamoto tunayoipata ni hiyo roho ya watu kutaka kuvamia maeneo ya kanisa kwa ushawishi ambao utawapelekea kuingia mahali pagumu, kwa sababu maeneo yale yametengwa, yamewekwa wakfu na kanisa lilipewa kwa utaratibu kabisa."



Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akizungumza na wananchi wilayani kwake katika moja ya ziara zake za kutatua changamoto zinazowakabili. **PICHA: JAMES LANKA**

# Uchangiaji damu KCMC washuka

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HALI ya uchangiaji wa damu katika Benki ya Damu Salama inayohudumia mikoa ya Kanda ya Kaskazini iliyopo Hospitali ya Rufani ya KCMC hairidhishi, kutokana na rekodi zake kuonyesha wachangiaji wamepungua kutoka watu 10 kwa siku hadi kufikia watatu.

Kushuka kwa rekodi hiyo ya wachangiaji wa damu salama, kunatoa picha halisi sasa kwamba kuna hitajika uhamasishaji wa hali ya juu kwa wananchi kujitokeza kutoa damu kwa ajili ya kusaidia wenye uhitaji hasa wagonjwa wa Cycosell, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, mama wajawazito na waathirika wa ajali.

Akizungumza jana, wakati wa uchangiaji wa damu uliofanywa na waumini wa Kanisa la wa Adventisa Wasabato lililopo Majengo, Manispaa ya Moshi, Mtaalamu wa Ushauri Nasaha wa Benki ya Damu Salama na msimamizi wa zoezi hilo, Penina Swai, alisema bado wana upungufu wa damu ingawa sio mkubwa sana.

"Kwa jamii, mwamko bado ni mdogo, uko chini sana kwa sababu kwa pale kituoni kwetu tunategemea angalau tupate wachangiaji watano mpaka 10 kwa siku, lakini kwa sasa tunapata wachangiaji mmoja mpaka watatu kwa siku na kuna siku hatupati wachangiaji kabisa," alieleza Swai.

Hospitali za rufani za mikoa kama Mawenzi (Kilimanjaro), Mount Meru (Arusha), Bombo (Tanga) na Hospitali Teule ya Misheni Hydom (Manyara) na Hospitali ya Taifa ya Rufani ya Magonjwa ya Kifua Kikuu (Kibong'oto) zinategemea kupata damu katika benki hiyo.

Mtaalamu huyo ameeleza, kwa kuwa kuchangia damu ni tendo la hiari na ni tendo la upendo, wanawaomba watu wajitokeze kwa wingi kuchangia damu kwa ajili ya mahitaji ambayo ni makubwa zaidi kwa wahitaji waliopo katika hospitali zilizopo mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga.

Amefafanua kuwa katika kituo chao, hali ya damu upatikanaji wake kwa sasa hivi sio mkubwa wala mdogo, ni wa wastani. Amesema watu wanajitokeza ingawa sio kwa kiasi kikubwa ambacho wanategemea jamii ijitokeze kuchangia damu.

# Jaji ataka watumishi kushughulikia malalamiko

**Na Mwandishi wetu,** MOSHI

KAIMU Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Moshi, Partricia Fikirini, amewataka watumishi wa mahakama kushughulikia malalamiko ya wateja ambayo yapo ndani ya uwezo wao ili kuwa na matokeo mazuri.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa watumishi wa mahakama za mkoa wa Kilimanjaro, yaliyoadaliwa na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika-Misa Tan, kwa kushirikiana na Taasisi ya Kijerumani ya Friedrich Ebert Stiftung.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kuboresha upatikanaji wa taarifa mahakamani.

Mafunzo hayo yanahusu huduma kwa wateja, upatikanaji wa taarifa na maadili kwa utumishi wa umma.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa ni hitaji la watumishi wa mahakama kwa muda mrefu kutokana na ukweli kuwa wanahudumia watu wa aina mbalimbali na wanahitaji huduma nzuri ili kupunguza au kumaliza malalamiko.

"Mafunzo haya ni msingi wa mabadiliko kwa kilio cha muda mrefu kwa wateja wetu kutoridhishwa na huduma za mahakama. Natarajia yatazingatiwa na kusaidia kuleta mabadiliko katika kuwahudumia wateja," alisema Jaji Fikirini.

Aidha, aliwataka watumishi hao kuunda kikosi kazi cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mafunzo hayo ya jinsi wanavyowahudumia wateja wanaofika mahakamani, ili kupunguza malalamiko ambayo yanatoa taswira isiyo sahihi kwa mahakama.

Akimkaribisha Jaji Mfawidhi Kanda ya Moshi, Patricia Fikirini, kufungua mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (Misa Tan), Salome Kitomari, alisema mafunzo hayo yamejumuisha watumishi 36 wa mahakama za mkoa huo.

Alisema watumishi hao kuwa ni pamoja na Mahakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakimu wa Mahakama za Wilaya, Mwanzo pamoja na watunza kumbukumbu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema washiriki hao walifundishwa nini maana ya uhuru wa kujieleza (mambo muhimu na misingi yake), huduma kwa wateja na ujuzi wa mawasiliano kwa watumishi wa umma.

Kadhalika, alisema washiriki watajifunza mifano ya utekelezaji wa uhuru wa kujieleza, Tanzania, Afrika na duniani, matakwa ya kisheria ya uhuru wa upatikanaji wa taarifa, muundo wa vyombo/taasisi za umma na upatikanaji wa taarifa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 19, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA? UTURUKI KINARA WA UPASUAJI PUA



## Dodoma Sekondari yawaita wahitimu kuchanga mil. 200/- za uzio wa shule

Ukurasa 19



# Mila zinavyotesa watoto Shinyanga kuozeshwa, mimba na kuacha shule

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Waandishi wanapotosha Kiswahili chetu

"KIMYA kimya si ujinga ni maneno kupeleleza." Umwonapo mtu katulia tuli, usidhani ni mjinga bali anachunguza mambo. Twakumbushwa umuhimu wa kuchunguza mambo, kabla ya kufanya uamuzi.

Toleo la Machi 10, 2019 niliandika makala yenye kichwa: "Kazi isiyofuatiliwa haiongoki." Paragrafu ya nne iliyomhusu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi ilisomeka:

"Kama kuna tuzo (kitu anachopewa mtu kama zawadi baada ya kufanya jambo zuri; tunu) Mnyalukolo (ndugu yangu) huyo anastahiki. Ingawa mimi si Mhehe, natambua kuwa Watanzania wote ni ndugu."

Makala ile ilimfanya mwalimu na rafiki yangu, Mohamed Sharif wa Tanga, anitumie ujumbe ufuatao kuhusu neno 'tuzo,' akielezea maana yake kwa kirefu kama ifuatavyo:

"Tuzo, tuza, tuliza. Atuzwa mtu kwa maana ya kutulizwa. Katika ngoma pande zote kuimbana au watani, unaozidiwa 'humtuza' kwa kumpa kitu asiendelee. 'Wanamtuza.' Vilevile akigandisha mtu atuzwa. Mtoto akileta kero huambiwa, 'Wee! Mwana wee! Hebu jituze."

"Tunzo, tunza, tazama, angalia. Anayetunzwa mtu anapopendeza. Anapofurahisha, anaposhinda ili aendele. Wanasema, 'mcheza kwao hutunzwa.'Apewa tunzo."

"Sufufu ni wingi wa safu. Tumezoea kusema 'pangeni safu.' Mkishapanga mwaulizwa: 'Ziko ngapi?' Ziko kumi. Safu ni mstari mmoja; mingi ni sufufu."

Tukosoe makosa ya magazeti ya michezo yanavyotumia maneno tofauti na maana yake. 'Ndege ya... balaa." Neno 'balaa' nimejitahidi kueleza maana yake, lakini bado lapotoshwa na magazeti ya michezo.

'Balaa' pia 'baa' ni janga lililoenea katika jamii au kwa mtu. Jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; kisirani, nuksi; jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku, beluwa.

Mwandishi angeeleza 'balaa' ya ndege ya... ikoje: Kwamba kila akipanda ndege yake hushindwa kuruka? Huugua ghafla anapokuwa ndani yake? Abiria mwingine anayekuwa ndani ya ndege hiyo, hufia ndani inapokuwa angani au balaa la namna gani? Kama ina balaa kwa nini mmiliki huyo anaendelea kuitumia?

Pia, nimeshuhudia magazetini yakitumika maneno kama 'shobo; kitaa na buana." Ni maneno yanayonikanganya.

Haya ni baadhi ya maneno ya mitaani yatumiwayo kila mara na magazeti ya michezo nchini. Matokeo ya matumizi yasiyokuwamo kwenye msamiati wa Kiswahili, twashindwa kuandika maneno sahihi ya Kiswahili.

Ndicho kile kilichosemwa na wahenga kuwa (ashaakum) 'Kuchamba kwingi mwisho huondoka na mavi.' Ni methali inayotumiwa kurejea mfano wa jambo linaloonyesha dalili fulani, zilizopuuzwa kisha likaishia kuharibika.

Tusiyadharau mambo madogo; huweza yakawa makubwa kama Kiswahili kinavyopotoshwa kwa matumizi ya maneno ya mitaani. Tunawafunza nini wenzetu?

Baadhi ya maneno ya mitaani yatumiwayo sana na magazeti ya michezo: '... aliamsha dude...' Maana sahihi ya 'dude' ni kitu kikubwa kisichojulikana; dubwana. Lakabu (jina analopewa mtu zaidi ya jina lake) ya kuonyesha dharau kwa mtu mwingine.

Maana ya 'amsha' ni toa mtu usingizini; inua mtu aliyekuwa nyuma kimawazo na kiuchumi; zindua. 'Dude' ni kitu kikubwa kisichojulikana; dubwana; mtu anayedharauliwa. Kuandikwa "...aliamsha dude..." maana yake nini?

Maneno ya mitaani, yanatufanya tushindwe kujua maana sahihi ya maneno ya Kiswahili au kuyaandika na kuyatamka tofauti na maudhui (wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) yake hata twashindwa kuandika sentensi zinazoeleweka! Ni yaleyale ya (ashaakum) "kuchamba kwingi ..."

"... ila kama zitaangaliwa rekodi ya mechi zao sita zilizopita za timu hizo katika ligi ili kutoa mbabe, basi ushindi lazima uende kwa vijana wa Alliance, madogo hao wametisha."

Mwandishi kaandika "... ushindi lazima uende kwa vijana wa Alliance ..." lakini matokeo halisi hao walioabashiriwa ushindi ndio waliofungwa na timu iliyodharauliwa na mwandishi.

Maneno matatu ya " ... madogo hao wametisha" yanishangaza sana. Kwa nini mwandishi hakuandika 'vijana hao wanatisha' na badala yake akawapa jina la dharau? 'dogo' (si rasmi), ni mtu mwenye umbo dogo, sio kuwa kubwa; katiti, saghiri; siokuwa nyingi; chache, haba.

"Uchaguzi huo ulioghubikwa ..." Kwa kadiri ya ufahamu wangu, neno 'ghubika' si Kiswahili. Badala yake mwandishi angetumia neno 'gubika' lenye maana ya kufunika kabisa bila kuacha sehemu. 'Gubigubi' ni namna ya kujifunika mwili mzima mpaka usoni.

'Gubiko' ni zawadi anazopewa mtawala wa jadi kwa kuruhusu msafara kupumzika nchini mwake. 'Gubia' ni kitendo cha kunywa maji kwa mfululizo.

Soma jinsi sentensi zinavyoandikwa na waandishi wetu wa leo: "Ebu tulia, kumbuka mashambulizi 'flani' makali katika mchezo wa Namungo dhidi ya Yanga katika dakika za 29...kipa akiupa mpira kasi kwa shuti flani la mbali."

Sentensi hii haileti maana, kwani haieleweki! Aidha 'flani' si Kiswahili. Neno hilo limerudiwa mara mbili, kuthibitisha mwandishi hajui kuandika neno hilo kwa usahihi! 'Fulani' (si flani) hutumika kuwakilisha jina la mtu au kitu; -enye kutotajwa kwa jina.

"...(timu ya soka) noma! Wabeba ndoo ya..." Kilichoshindaniwa ni 'ndoo' au kombe? 'Ndoo' ni chombo cha bati au plastiki cha kuhifadhia vitu vya majimaji.

Pia, ni chombo kidogo kama vile cha buyu kilichofungwa kamba cha kutekea maji katika kisima kirefu; zela. 'Kombe' ina maana nyingi, lakini kwa muktadha huu ni kitu cha thamani kinachotolewa kama kielelezo cha ushindi katika mchezo kama vile kandanda.

**Methali: Ubishi chanzo cha mateso.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI



Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Ahmed Msangi. **PICHA: MTANDAO**

# Ulinzi na usalama ni wajibu wako, nami

MAKUZI ya mwanadamu yanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo majanga na matatizo mengi yaliyogawanyika katika makundi mbalimbali.

Wakati mwingine, inaaminika binadamu huwa ndiye kisababishi cha kutenda au kutotoa taarifa za haraka, ili kero au changamoto zinazomkabili ziweze kutatuliwa. Miongoni mwa kero na changamoto hizo, ni uhalifu.

Hilo ni tatizo linalosababishwa na mwanadamu ndani ya jamii na kusababisha madhara kwa watu, jamii na taifa kwa ujumla. Ni tatizo linalojenga hofu kwa watu na jamii, jambo linaloifanya jamii kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, kwa hofu ya kutendewa uhalifu.

Wananchi wanapaswa kutambua kuwa, suala la kuzuia uhalifu ni jukumu la kila mtu ndani ya jamii. Ili jamii iweze kuepuka madhara ya vitendo vya uhalifu, wananchi hawana budi kushirikiana na Jeshi la Polisi, katika kutekeleza mkakati wa ulinzi jirani unaowawezesha wananchi kujilinda wenyewe, kwa kupeana taarifa zitakazosaidia kuweka makazi yao katika hali ya amani na usalama.

Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Ahmed Msangi, anasema mpango wa ulinzi jirani, ni moja ya mikakati ya kuzuia uhalifu inayotekelezwa na Polisi, kupitia Kamisheni ya Polisi Jamii, lengo ni kuimarisha usalama wa raia na mali zao waliko.

Hali iliyoko ni kwamba, mkakati huo wa ulinzi jirani unasaidia kuondoa kero za uhalifu wa wizi wa vitu vidogo majumbani na hata wizi wa kuvunja nyumba, pale wahusika wanapokuwa hawapo.

Pia, ni mkakati unaohamasisha watu kujenga utamaduni wa kupeana taarifa na jirani zao, kuwaangalizia mazingira ya nyumba yao, ili wahalifu wasitumie fursa ya wao kutokuwapo na kutekeleza azima yao ya kutenda uhalifu.

"Jamii inapaswa kuelewa kwamba mpango wa ulinzi jirani si wa Jeshi la Polisi, bali ni wa jamii nzima ambayo inachukia uhalifu, hivyo wanaamua kuanzisha mtandao wao wa ulinzi kwa lengo la kujihakikishia usalama wao na mali zao," anasema DCP Msangi.

Mkakati wa ulinzi jirani, ni mpango shirikishi wa ulinzi ndani ya jamii, unaojumuisha watu na nyumba jirani, kwa ajili ya kuimarisha usalama, kwa kutengeneza mtandao wa mawasiliano baina yao, kupashana taarifa za vitendo vya uhalifu, lengo ni kutafuta ufumbuzi, ili waweze kuwa salama.

Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi, wana jukumu la kufanya mpango huo wa ulinzi jirani kuwa endelevu. Kufanya hivyo, kunaelezwa kutasaidia upatikanaji taarifa za vitendo vya uhalifu vinavyotokea majumbani, ikiwamo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Ni ukweli usio na shaka kuwa, wananchi wanapoamua kuchukua hatua ya kujihakikishia usalama wao na mali zao bila ya kuvunja sheria, vitendo vya uhalifu hupungua ndani ya jamii, kwa kuwa wahalifu wanatoka katika jamii yao.

Wengi wao ni watoto na jirani zao, jamaa, hivyo ni rahisi kuwabaini, kuwafichua na kuwachukulia hatua za kisheria na kuacha tabia ya kulindana.

Jukumu la Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa mkakati huu wa ulinzi jirani, ni kuchangia utaalamu na ushauri kwa vikundi hivyo vya ulinzi, juu ya masuala ya ulinzi na usalama, kwa kutumia askari kata ambaye ndiye mtaalamu wa usalama katika kata na ana jukumu la kuhakikisha kero za kiusalama zinatatuliwa kwa wakati.

Jamii mbalimbali zinapaswa kujiunga na kushirikiana katika kupanga mipango na mikakati ya kujihakikishia ulinzi na usalama, kama wanavyopanga mipango mingine ya kijamii ndani ya jamii zao, ili kujihakikishia huduma mbalimbali katika jamii.

Ushirikiano huo wa wananchi wenyewe na Jeshi la Polisi, ndio msingi wa kufanikiwa kwa mpango mkakati wa ulinzi jirani.

Viongozi wa serikali ya mtaa na shehia kwa Zanzibar, kijiji pamoja na kitongoji, wao kama viongozi wa wananchi wenye wajibu wa kuhakikisha katika maeneo yao, kunakuwapo na hali ya amani na utulivu katika maeneo yao, wanawajibika kuwahamasisha wananchi suala zima la kuanzisha vikundi vya ulinzi jirani ili kuepukana na vitendo vya uhalifu.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

ELIMU

# Matumizi haya ya Kiswahili yanaangukia katika makosa

## • Tujipange matumizi ya neno ‘kama’

**NA LOTHA LOYEWO, ARUSHA**

SI mara ya kwanza kuwaona au kuwasikia, wataalamu wa Kiswahili, lugha yetu adhimu, wakiendelea kuelekeza matumizi sahihi ya baadhi ya maneno ya Kiswahili au hata sentensi zake katika vyombo vya habari.

Suala hilo ni la kupongezwa sana na linafaa kuendelezwa, pindi nafasi inapopatikana katika vyombo habari, ili lugha hiyo - Kiswahili izidi kuenziwa.

Licha ya juhudi hizo, kuna ambalo limekuwa gumu kuachwa katika matumizi ya wataalamu wa lugha na hata wazungumzaji wa kawaida.

Neno ‘kama’ limekuwa likitumika katika muktadha tofauti. Mara utamsikia mzungumzaji wa lugha, akitamka: “Mimi kama baba; kama mama; mimi kama diwani; mimi kama waziri.”

Tatizo hilo ni kubwa sana katika lugha, ingawa neno ‘kama’ ni pana. Kuna wakati inachukua nafasi ya kifananishi cha dhana ya sawasawa na inatumika kuonyesha msisitizo wa kitu au jambo, mathalan ‘amependeza kama nini,’ kwa maana ya amependeza sana. Pia ‘kama’ hutumika kuonyesha makisio.

Lengo la makala hii ni kujikita katika maana ya neno ‘kama’ katika nafasi ya kifananishi inavyotumiwa na watumiaji na wazungumzaji wa Kiswahili katika muktadha mbalimbali.

Je, ni sahihi kujifananisha wakati wewe ndiye? Kwa mantiki hiyo, ukisema kuwa ‘mimi kama mtangazaji’ inabeba ujumbe wewe sio mtangazaji, ila unajifananisha tu na mtangazaji.

Ukisema ‘ninatangaza mpira kama Mpenja,’ maana yake unajifananisha tu na Mpenja na kamwe huwezi kuwa Mpenja. Watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili, kupitia sanaa zao za lugha, wamekuwa wakiwasilisha ujumbe katika mtazamo wa kujifananisha, wakati wanachomaanisha ndio kwenye uhalisia wa ujumbe.

Kwa matumizi hayo, neno ‘kama’ ni wazi kuwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), lina kazi na nafasi kubwa ya kuyaelekeza matumizi sahihi ya baadhi ya maneno yanayotumiwa ndivyo sivyo. Hiyo, binafsi naona ndio kazi kubwa iliyoko mezani mwa BAKITA.

Ni lazima matumizi holela ya lugha ya Kiswahili yadhibitiwe ingawa si kwa kiboko, ila kwa kutumia vyombo vya habari kama magazeti, redio, runinga na hata mitandao ya kijami, vikatoa maelekezo ya matumizi sahihi ya baadhi ya maneno.

Kutegemea vipindi vya lugha katika runinga na redio, haitoshi. Magazeti na mitandao ya kijamii, pamoja na redio zitumike kwa lengo la kuelimisha umma juu ya matumizi sahihi ya baadhi ya maneno.

Sioni haja ya kujifananisha na baba, mama, kiongozi, mwalimu, au mwanafunzi wakati ndiye. Itakuwa sahihi kujifananisha hivyo, kama siye mhusika halisi anayebeba wasifu huo.

Kwa mfano mtu akisema: “Mimi kama mwalimu wenu nitawafundisha vizuri,” ni kwamba anaeleweka kuwa yeye sio mwalimu wao, ila anajifananisha na mwalimu mhusika. Tayari inakuwa imeangukia katika upotoshaji.

Kusema “Mimi kama baba nimejitahidi kuyatekeleza majukumu yangu,” maana yake ni kwamba wewe sio baba ila unajifananisha tu na baba aliyepo.



Mwanafunzi Bahati kutoka Beijing, China, akiwasilisha utafiti unaohusu utalii ulivyo uti wa mgongo, katika maendeleo ya taifa, unaokamilisha mafunzo ya miezi minne ya lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Kampasi ya Vuga, Unguja.

> “Mimi baba yenu nimeyatekeleza majukumu yangu,” bado ni sahihi ili mradi tu neno kama lisiwepo katika sentensi hiyo. Mifano mingine ni: “Mimi diwani wenu nitawachimbia visima vya maji” na siyo “mimi kama diwani....”



Mkuu wa Idara ya Kiswahili kwa Wageni, katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Dk. Zainab Ali Iddi, akiwapongeza wanafunzi wa China, wanaojifunza Kiswahili chuoni hapo, baada ya kuwasilisha tafiti walizofanya kukamilisha mafunzo yao ya miezi minne. . **PICHA ZOTE: RAMADHANI ALI: MAELEZO, ZANZIBAR.**

Kwanini ujifananishe wakati wewe ni baba au mama, mwalimu au kiongozi? Mara nyingi lugha inatawaliwa na muktadha, mada ya mazungumzo na hata uhusiano baina ya wanaozungumza.

Kwa maana hiyo, muktadha au mada unaweza kubaini maana ya sentensi. Kwa mfano. inatosha tu kusema kwamba ‘Mimi nitawafundisha vizuri’ na itakuwa imekamilishwa na mazingira anayozungumzia, mada husika na uhusiano kati ya unaozungumza nao.

Kwa mfano, iwapo mtu anajijua kuwa hadhi na cheo chake ni mwalimu, kwa nini atamke tena “Mimi kama mwalimu wenu?” Pia, pasipo shaka unajijua wewe ni baba, kwa nini useme tena mimi kama baba?

Inatosha tu kusema: “Mimi nimeyatekeleza majukumu yangu,” kwa sababu unaozungumza nao wanakujua wewe ni nani au nafasi yako.

Ikumbukwe kuwa, kinachojaribiwa kufafanuliwa au kutolewa ufafanuzi, ni matumizi ya neno ‘kama’ kwa maana ya kifananishi.

Mtui akisema: “Mimi baba yenu nimeyatekeleza majukumu yangu,” bado ni sahihi ili mradi tu neno kama lisiwepo katika sentensi hiyo. Mifano mingine ni: “Mimi diwani wenu nitawachimbia visima vya maji” na siyo “mimi kama diwani....”

Pia, kuna mfano: “Mimi Waziri wa Nishati, nitahakikisha umeme utawashwa katika kila kijiji” na siyo “mimi kama waziri...”

Chonde walumbi wa lugha, ninawaasa turudi kwenye mstari kwa kuzingatia matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili, ili wanaotuiga waondoke na kiichocheemeka kwa ufasaha.

Ni jukumu la kila mwana lugha kuyatambua na kuyarekebisha makosa katika matumizi ya lugha. Kwa kufanya hivyo, kamwe lugha hii muhimu, yenye heshima na kukua kwa kasi, haiwezi kukosa mwelekeo.

Yapo matumizi mengi holela ya lugha ya Kiswahili yanayoibuka kila baada ya muda na hata kuwapo baadhi ya maneno yasiyo sahihi kuibuka kwa kulazimishwa tu kimatumizi.

Chonde tunaambiwa kupitia usemi: “Mjenga nchi ni mwananchi, pia mbomoa nchi ni mwananchi mwenyewe. Katika lugha, mjenga lugha ni mwanalugha na mbomoaji ni mwanalugha mwenyewe.” Tusiyaruhusu haya.

**• Mwandishi anapatikana kupitia simu: (+255) 0752631092 na baruapepe: lothalaizer@yahoo.com**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mila zinavyotesa watoto Shinyanga kuozeshwa, mimba na kuacha shule

## ■Serikali, NGO zashikia 'bango'
## ■Mabaraza watoto vijijini yaundwa
## ■Mikutano hadhara yaja na maagizo

HALMASHAURI ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, ni miongoni zinazokabiliwa na tatizo la wanafunzi kukatishwa masomo, kwa sababu ya ujauzito na wengine kuolewa ndoa za utotoni.

Takwimu za mwaka jana zinaonyesha, kuna wanafunzi 22 waliokatiswa masomo, kwa sababu ya ujauzito na wengine kuolewa ndoa za utotoni; shule ya msingi wako saba, sekondari 15.

Mwaka huu, takwimu zinaonyesha kuwapo na wanafunzi sita katika halmashauri hiyo, wameshafukuzwa shule kwa sababu ya ujauzito.

Kutokana na kushamiri hali hiyo, halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Agape, linalotetea haki za watoto mkoani Shinyanga, limeanza kuunda mabaraza ya watoto ngazi ya vijiji.

Lengo ni kusaidia utoaji taarifa za awali kuhusu matukio, ili yachukuliwe hatua haraka kabla ya madhara.

Ni mabaraza yanayoshirikisha kikundi cha watoto wasiozidi 40 wanasoma na wasio soma, wanaokutana na kujadili changamoto zinazowakabili dhidi ya matukio ya ukatili juu yao, ikiwamo haki ya elimu na wanaziwasilisha kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji na kuchukuliwa hatua haraka.

Aisha Omari, ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya Shinyanga Vijijini, anayesema mabaraza ya watoto ni muhimu katika mapambano ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, tatizo linaloendelea kuwa kero inayozima ndoto za wanafunzi.

Anasema, watoto wanapokutana, wanakuwa huru na wazi kuzungumzia changamoto zinazowakabili, kuliko wanapoeleza matatizo kwa watu wazima, wakuwa waoga.

"Lengo letu kubwa ni kupata taarifa mapema za matukio haya ya kikatili kwa watoto, kabla ya kuwaletea madhara.

"Mimba na ndoa hizi za utotoni zimekuwa zikishamiri kutokana na watoto kutosikilizwa shida zao na kufanyiwa utatuzi wa haraka, ambapo hujikuta wakirubunika na hatimaye kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na kuambulia ujauzito ama kuolewa," anasema Omari.

Anataja manufaa ya mikakati dhidi ya ukatili huo, ni kwamba serikali itachukua hatua haraka watuhumiwa wote, wakiwamo wazazi wasiotekeleza mahitaji ya watoto na wanaowaozesha utotoni.

Wasimamizi Agape

Ofisa Mradi wa Kutokomeza Mimba na Ndoa za Utotoni kutoka Agape, Mustapha Isabuda, anasema wameanza kuunda mabaraza hayo katika vijiji vya Shinyanga.

Anasema, muundo wa utendaji wa mabaraza hayo, yatakuwa na uongozi; mwenyekiti, makamu wake, katibu na mweka hazina na wajumbe sita, kutoka kundi la watoto 40.

"Shirika la Agape tumekuwa tukitekeleza mradi huu wa kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, lakini changamoto nyingine ambayo tunakumbana nayo ni usiri wa kupata taarifa mapema juu ya matukio hayo," anasema Isabuda.



Watoto wakiwa kwenye mkutano wa kuunda mabaraza yao ngazi ya vijiji katika Kata ya Didia, Halmashauri ya Shinyanga Vijijini. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**

> "Kupitia uundwaji wa mabaraza haya ya watoto tuna imani kabisa yataweza kuwajengea ujasiri watoto na kuweza kujitambua kwa kupinga vitendo hivyo vya kupewa ujauzito, pamoja na kuozeshwa ndoa za utotoni,"

Anaeleza dira aliyo nayo ni matarajio ya chachu ya mabadiliko katika kutokomeza mimba na ndoa za utotoni Shinyanga, ikianzia Shinyanga Vijijini.

Mwalimu & Mwanafunzi

Ntenga Ng'hehela, ni Mwalimu Mlezi kutoka Shule ya Msingi Bukumbi, anayeonyesha faraja ya matarajio, kwamba mabaraza hayo yatawasaidia walimu kupata taarifa za utoro wa wanafunzi na kuzishughulikia haraka, hali itakayosaidia kupunguza watoto kuacha shule na kuolewa.

"Wanafunzi hawa wa maeneo ya vijijini huwa wasiri sana na wana woga wa kuzungumza na walimu wao kuwaelezea matatizo yao.

"Lakini kupitia mabaraza haya ya watoto, kunaweza kuwa msaada mkubwa sana wa kupata taarifa mapema za mwanafunzi, kutaka kuozeshwa na kuzifanyia kazi mapema," anasema Ng'hehela.

Mwanafunzi Naomi Salumu, anayesoma darasa la saba, anataja sababu ya wao kukosa ujasiri wa kujieleza, ni kutokana na mfumo wa malezi ya kifamilia, akiutaja 'mfumo dume,' msichana hana sauti ndani ya familia na jamii.

Anasema malezi hayo yanachangia kumdumaza mtoto wa kike kuwa wa kukubali kila jambo, ikiwamo kukosa ushujaa wa kupinga maombi ya mwanaume, ambayo huwaacha wanaishia katika lindi la ujauzito, kukatishwa masomo na kuolewa.

"Watoto wa kike wa vijijini hatuna sauti kabisa ndani ya familia na jamii. Hata mzazi akiamua niache shule na kwenda kuolewa, siwezi kupinga kwa sababu wao wanaona mtoto wa kike ni wa kuolewa tu. Ndiyo maana, ndoa za utotoni zinaendelea kuwapo," anasema Naomi.

"Mwanafunzi akipewa ujauzito shuleni, huwezi kumuona mzazi anachukizwa na jambo hilo, zaidi ya kufurahia kuwa tayari mwanawe atafukuzwa shule na amepata fursa ya kumuozesha, ili apate mifugo hasa ng'ombe," anaeleza.

**VIONGOZI VIJIJINI**

Ofisa Mtendaji Kata ya Didia, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Jacksoni Majenga, anasema kwamba yalikoundwa mabaraza hayo ya watoto ngazi ya vijiji, ndiko kuliko kithiri matukio ya mimba na ndoa za utotoni, kutokana na wazazi kuyakumbatia.

Anasema, kati ya kila wanafunzi watatu wa shule za msingi walipewa ujauzito mwaka huu kwenye kata hiyo, mtuhumiwa mmoja ameshatajwa na kukamatwa, lakini wengine wamegoma kuwataja kutokana na wazazi kuwazuia kutaja.

"Hata huyu mtuhumiwa mmoja ambaye tumemkamata, tunahofia huenda hata asifungwe jela, kwa sababu ya wazazi kuharibu ushahidi kwa kumzuia mtoto wao kutokwenda mahakamani kutoa ushahidi au kumkana. Lengo tu wapate kumuozesha na kupata mifugo.

"Kupitia uundwaji wa mabaraza haya ya watoto tuna imani kabisa yataweza kuwajengea ujasiri watoto na kuweza kujitambua kwa kupinga vitendo hivyo vya kupewa ujauzito, pamoja na kuozeshwa ndoa za utotoni," anasema Majenga.

Anataja mbinu inayotumika katika mabaraza hayo, ni kupaza sauti za kutoa taarifa mapema, inayowapa nafasi viongozi kuchukua hatua haraka.

Masana Kayela ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mwanono, eneo ambalo wanafunzi wawili wamepewa ujauzito, anakiri wazazi kuwa chanzo cha matatizo.

Anafafanua sababu kuu, ni kuenzi mila na desturi zilizopitwa na wakati, za kumnyima hadhi msichana, akiahidi kuitisha mikutano ya hadhara kuonya tabia isiyofaa ya wazazi kuozesha wanafunzi na wanaume kuwanyemelea mabinti.

Shanwa Dutwa, ni mzazi anayekiri kuwapo mila hizo za kutopenda kusomesha wasichana na anabainisha, mzizi uliopo ni kasoro katika elimu hiyo.

Maria Mwaselela, ni wakili wa kujitegemea wa mjini Shinyanga, anayesema kesi za ndoa za utotoni ni vigumu kumtia hatiani mtuhumiwa, kutokana na mwanya wanaoutumia wazazi kupitia Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayoruhusu mtoto chini ya miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi au mahakama.



Meneja Mradi wa Kuzuia Mimba na Ndoa za Utotoni kutoka Shirika la Agape, mkoani Shinyanga, Mustapha Isabuda, akijadili jambo na watoto kuhusu mabaraza yao.

JIELIMISHE



Chombo kinachosafiri kwenda katika anga nyingine. **PICHA: MTANDAO**

# Safari ya ajabu angani yenye mafanikio

WAPENZI wawili nchini Iran, wamekamatwa baada ya kuchumbiana hadharani, huku watu wakiwashangilia.

KATIKA mpango wa kuanzisha safari za kibiashara kwenda anga za mbali, Shirika la Nasa, limejaribu chombo chake kitakachotumika kwa safari hizo kwa mafanikio.

'Crew Dragon' chombo cha kubeba watu kwenda anga za mbali kilichotengenezwa na Shirika la Kimarekani la 'SpaceX' kwa ajili ya Shirika la 'Nasa' kimerudi duniani kutoka kituo cha kimataifa cha anga.

Katika taarifa iliyotolewa na Nasa kuwa ni ya jaribio, chombo hicho kilichorushwa kwenda kituo cha kimataifa cha anga, kimerejea duniani na kutua katika bahari ya Atlantiki kilomita 450 kutoka jimbo la Florida.

Chombo hicho kiligusa anga la dunia saa moja na dakika 52 na kugusa uso wa bahari saa mbili na dakika 45 katika eneo hilo.

Nasa katika mpango wake wa kuanzisha safari za kibiashara, mnamo Machi 2 mwaka huu, ilirusha chombo kilichobuniwa kwa ajili ya kubeba watu kwenda kituo cha kimataifa cha anga.

Siku inayofauta, Machi 3, chombo hicho kiliwasili kituoni hapo na kukaa katika kituo hicho cha angani kwa muda wa siku sita.

Baada ya mafanikio hayo ya jaribio la safari iliyofanyika bila kuwa na watu jaribio la safari itakayokuwa na watu wawili, wanajimu wa Nasa kwenda kituo cha kimataifa cha anga, litafanyika mwezi Julai, mwaka huu.

Katika taarifa nyingine chombo cha shirika la Boeing kijulikanacho 'Starliner' kinatarajiwa kujaribu safari ya bila watu mwezi ujao na iwapo litafanikiwa katika jaribio hilo, itafanya jaribio litakalokuwa na watu, mwezi Agosti mwaka huu.

**Kwa mujibu wa TRT**

## JE, WAJUA?



Tiba ya pua ikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

# Uturuki kinara wa upasuaji pua

IWE Kirusi, Kiarabu ama Kichina au hata fizikia ya maumbo. Ubongo wa binadamu unaweza kujifunza kitu chochote kile, hata kiwe kigumu namna gani, tena kwa haraka.

RAIS wa Taasisi ya Upasuaji wa Pua barani Ulaya, Profesa Nazım Cerkes, ambaye kutaaluma ni daktari wa tiba, anasema Uturuki ni nchi inayoongoza duniani katika fani ya upasuaji wa uboreshaji wa mwonekano wa pua za watu.

Akiongea katika warsha ya kimataifa ya upasuaji na uboreshaji wa mwonekano wa pua inayorushwa moja kwa moja kupitia mtandao, iliyofanyika mwaka huu katika Hospitali ya Florence Nightingale Sisli, Cerkes alisema wamewaleta pamoja mabingwa kutoka sehemu zinazosifika kwa upasuaji wa pua, ili kubadilishana uzoefu kumeisaidia fani ya upasuaji wa pua nchini Uturuki.

Cerkes, anasema kwamba Uturuki iliwaalika madaktari bingwa 10 wa kimataifa wanaosifika katika fani ya uboreshaji wa mwonekano na upasuaji bandia.

Madaktari hao walifanya operesheni zilizotumika kama darasa kwa madaktari wengine wasiobobea katika eneo hilo. Vilevile baadhi ya operesheni zilirushwa moja kwa moja kupitia mtandao.

Cerkes, anaongeza kwamba, kutokana na ukweli asilimia 90 ya washiriki wa warsha hizo ni madaktari wa kigeni, hilo linaifanya Uturuki iongoze katika upande wa kuonyesha njia, kwa kuwa madaktari hao wa kigeni hutaka kujifunza njia mpya katika fani ya upasuaji wa uboreshaji wa mwonekano wa pua kutoka kwa madaktari wa Kituruki.

**TRT Swahili**



Meya Mbuzi. **PICHA: MTANDAO**

# Mbuzi achaguliwa kuwa meya

MBUZI anayeitwa 'Lincoln' amechaguliwa kuwa Meya wa Heshima wa manispaa moja iliyoko katika Jimbo la Vermont, nchini Marekani.

Mbuzi 'Lincoln' kutoka kijiji cha 'Fair Haven' kinachopatikana katika Jimbo la Vermont nchini Marekani, amechaguliwa kuwa meya wa heshima wa manispaa.

Kwa mujibu wa habari zilizotolewa na shirika la habari la Associated Press, kijiji hicho chenye idadi ya watu 2,500, wamemchagua mbuzi kumpa cheo cha meya wa heshima wa manispaa.

Mbuzi 'Lincoln' kwa mwaka mzima, atashiriki katika matukio yote muhimu kwa mujibu wa cheo chake.

Akielezea sababu za kufikia uamuzi huo, kiongozi wa kijiji hicho, Joe Gunter, aliwaambia wanahabari kuwa inatokana na kutokuwapo cheo hicho katika kijiji hicho, hivyo waliamua kumpa mbuzi huyo cheo cha rais wa heshima wa manispaa hiyo.

Gunter anatetea wazo hilo akisema lilikuwa muafaka kutokana na kuwawezesha kukusanya mapato kutoka kwa wamiliki wa wanyama ambao wangeshiriki uchaguzi. Katika uchaguzi huo, wanyama 16 walishiriki na zilikusanywa dola tano (Shilingi 11,500) ikiwa ni ada ya ushiriki wa kila mnyama.

Lincoln, mbuzi mwenye umri wa miaka mitatu, alipata kura 13 kati ya 53 zilizopigwa na kufanikiwa kuwa rais wa heshima wa manispaa. **TRT Swahili**

## UTAFITI

# Shinikizo damu linavyopopofusha

SHINIKIZO la juu la damu, ni miongoni mwa maradhi yanayoendelea kuwapata watu wengi nchini duniani kwa ujumla.

Kila siku, inaelezwa idadi ya watu wenye maradhi hayo ambayo yapo kwenye kundi la yasiyoambukiza yanaongezeka maradufu. Hiyo ni kwa mujibu wa tafiti mbalimbali.

Ugonjwa huo jinsi ulivyo, ni kwamba baada ya kuathiri mfumo wa damu, unasababisha madhara katika sehemu mbalimbali za mwili, yakiwamo macho.

Hiyo inaelezwa ni kwa vile huanzia kwenye mfumo wa damu, madhara yake kwenye macho uhusisha mishipa ya damu iliyo ndani ya jicho hususan sehemu ya ndani ya ukuta wa nyuma inayoitwa retina.

Kazi kubwa ya retina ni kupokea mwanga wenye taswira na kuubadilisha kwenye mfumo utakaowezesha kusafirishwa mpaka kwenye ubongo kwa ajili ya kutafsiriwa.

Shinikizo la juu la damu, linaelezwa linasababisha kuta za mishipa ya damu kutanuka, ikiwamo iliyoko kwenye retina (machoni) na kadri kuta za mishipa ya damu inavyotanuka ili kukabiliana na ongezeko la msukumo wa damu kutoka kwenye moyo, ndivyo inavyosababisha upenyo wa ndani ya mishipa ya damu kupungua.

Kupungua upenyo huo, kunapunguza kiwango cha damu kinachoweza kupita kwenye mishipa.



Upunguaji huo wa damu, husababisha kiasi kidogo cha damu kufikia kwenye retina na kukosekana, huku kwa kiwango kinachostahili cha damu ambayo hubeba virutubisho na hewa safi na kuipeleka kwenye chembe hai, hufanya uchukuaji wa uchafu kwa ajili ya kuusafirisha mpaka kwenye ogani ambazo hufanya kazi ya kuuondoa ushindikane.

Damu inavyopungua, huchangia ukosefu wa virutubisho kwenye chembe hai zinazounda retina, hivyo kusababisha ishindwa kufanya kazi yake ipasavyo. Matokeo yake, mgonjwa anashindwa kuona vizuri.

Sababu kubwa ya kutokea kwa athari za shinikizo la juu la damu kwenye macho, ni kupanda kwa shinikizo la damu.

Madhara hayo kwenye retina hutokea baada ya mgonjwa kuwa na shinikizo la juu la damu kwa muda mrefu, kwa miaka kadhaa.

**Kwa mujibu wa taarifa mtandao**



Mgonjwa akitibiwa macho. **PICHA: MTANDAO**

# ELIMU
## NA YASMINE PROTACE

NI shule kongwe, inayojulikana kwa wengi. Sasa ina umri unaotimu miaka 60. Ni mahali ambako pamezalisha majina makubwa ya nchi. Lakini hali yake ya leo ikoje? Hali si nzuri kiasi kwamba waliowahi kusoma hapo sasa wanaombwa kuikumbuka shule hiyo.

Ni shule inayokabiliwa na changamoto ya uzio, mahali iliko katikati ya Jiji la Dodoma.

Tayari uongozi wa shule unalalamika kwamba, kuna matatizo ya kibinadamu kama vile utoro, magari kupita ndani ya shule, baadhi ya watu wasiostahili wakiwamo wafanyabiashara wanaoendesha biashara zao katika eneo hilo.

Mbali na kutokuwapo uzio, Mwenyekiti wa Bodi wa Shule hiyo, Phillibert Bugenda, anataja changamoto nyingine ni mahitaji ya mabweni, maabara na vitanda.

Hilo ni tamko lake katika kikao cha kawaida kilichowakutanisha wazazi mwanzoni mwa mwezi huu, kuhusu kuchangia ujenzi wa uzio huo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo wa bodi, shule hiyo haina mipaka bayana kutokana na ukosefu wa uzio, hali inayowapa walimu mtihani wa kiusimamizi dhidi ya wanafunzi.

Anasema:"Kutokana na ukosefu wa uzio shule imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kuibiwa mali za shule."

Bugenda anataja matatizo mengine ni kuingiliwa na mifugo, kutoroka kwa baadhi ya wanafunzi, kushindwa kudhibiti uchelewaji wa wanafunzi, kuingiliwa na wafanyabiashara, pia wenye magari kugeuza maegesho yao na watu wenye matatizo ya akili kupageuza makazi yao.

Bugenda anasema, uwepo wa uzio, utaisaidia kuiepusha shule na changamoto tajwa, jambo analoamini litaleta mchakato tija kwa mchakato mzima wa ufundishaji shuleni.

Anataja faida kubwa ya uzio ni kuimarisha nidhamu ya wanafunzi, inayoangukia katika kuinua kiwango cha ufaulu shuleni.

**KAMPENI ZILIKOANZIA**

Mwenyekiti huyo anarejea mchakato wa ujenzi wa uzio ulianza mwaka 1978 bila ya mafanikio, japo zilitolewa fedha Shilingi 340,000 na Wizara ya Elimu.

Anafafanua: "Novemba 16 mwaka 1978, pesa hiyo ilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa uzio na Chama cha Ushirika na Ujenzi Dodoma, kilipewa jukumu la ujenzi kwa mkataba wenye namba Dd/ RDB/ 6/78/79/1/86 wa tarehe 5, Desemba 1978."

Anafafanua kuwa, kampuni hiyo haikufanikisha ujenzi huo licha ya kununua vifaa vyote vilivyohitajika kwa ajili ya mradi, kwa sababu ya kukosekana mipaka sahihi katika eneo la shule.

Bugenda anasema, ni hali iliyomlazimu aliyekuwa Mkuu wa Shule, kumwandikia Mkurugenzi wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) barua ya kudai ufafanuzi wa mipaka hiyo.

Mwenyekiti Bugenda, anasema tangu wakati huo kumekuwapo na mafanikio mbalimbali ya kupatikana mipaka ya mawe ya shule hiyo.

"Novemba 24, 2018, baada ya agizo la Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, katika mahafali ya kidato cha nne, Novemba 2, mwaka 2018, Halmashauri ya Jiji ilitoa ufafanuzi juu ya eneo la shule na mipaka," anasema.

Aidha, kibali na ramani ya ujenzi vimetolewa, kwa ajili ya mchakato na ujenzi kuanza na shule inafuatiliwa kwa karibu,



Baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma Shule ya Sekondari Dodoma, wakiwa katika mkutano wa kuchangia ujenzi wa ukuta. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE**

# JUHUDI ZILIZOKWAMA TANGU 1978
## Dodoma Sekondari yawaita wahitimu kuchanga mil. 200/- za uzio wa shule

- Kishindo cha Jafo chawezesha kazi kuanza
- Yalia tangu zama hizo mpaka haukujulikana
- Eneo shule lageuka kijiwe, njia ya magari

> Anasema bodi kupitia uongozi wa shule, hasa Kamati ya Ujenzi wa Uzio, imepanga kuwafikia wadau kwa nyakati tofauti, ili kuomba ushirika katika kupata kiwango cha fedha tajwa, kuufanikisha mradi.

huku uandaaji gharama za ujenzi wa uzio wa ukuta na kamati ya ujenzi ya uzio huo kwa ngazi ya shule imeshaundwa.

Bugenda anasema, kumeshafanyika makadirio ya gharama ya ujenzi, ambayo ni wastani wa zaidi ya shilingi milioni 200.

Anasema, ni ujenzi unaotarajiwa kuendana na mahitaji ya kisasa ya Jiji la Dodoma na msimamizi wake atakuwa, Mkurugenzi wa Jiji, kupitia Ofisi ya Mhandisi wa Jiji.

**VYANZO MAPATO**

Anataja vyanzo vya mapato vya kutekeleza mradi huo ni kupitia Kamati ya Ujenzi wa Uzio, inayoratibu kupata mapato kutoka kwa wadau wa shule, wizara na taasisi zake, watu waliosoma shule hiyo walioko ndani na nje ya nchi.

Wengine ni wadau wa elimu, wazazi na wanafunzi, mashirika ya umma, taasisi za fedha, wafanyabiashara wakubwa, kampuni za simu na watu wote watakaoguswa na mradi huo.

Anasema bodi kupitia uongozi wa shule, hasa Kamati ya Ujenzi wa Uzio, imepanga kuwafikia wadau kwa nyakati tofauti, ili kuomba ushirika katika kupata kiwango cha fedha tajwa, kuufanikisha mradi.

Anasema serikali kuu imewapatia shilingi bilioni 1.3, pesa zitakazotumika kununua vitanda, ujenzi wa mabweni mawili ya wasichana, ukarabati wa shule nzima na maabara.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi, kikao cha tarehe 2, mwezi huu, kilikutana na wazazi wenye watoto katika shule hiyo, ambao waliahidi kuchangia mradi huo wa ukuta wa shule.

Anasema katika kikao hicho, ahadi kutoka kwa wazazi ilikuwa shilingi milioni sita na pesa taslimu shilingi 730,000 zilikusanywa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi, tarehe 30, mwezi huu, wamepanga kukutana na watu waliosoma Dodoma Sekondari, kuchangia ujenzi wa ukuta huo.

Anasema ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kuwasomesha watoto bure na kuboresha miundombinu iliyochakaa katika shule.



Wazazi na walezi wakiwa katika mkutano wa ujenzi wa ukuta wa Dodoma Sekondari.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Serikali imefanya maboresho kadhaa katika sekta ya elimu, ikiwamo kutoa elimu bure na kuondoa walimu hewa. Je, yamesaidia kuongeza motisha ya kazi kwa walimu?

Wadau wanajadili?



**AMINATHA KYANDO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HAYO mazuri unayosema, sidhani kama yana uhusiano wowote na motisha ya kazi kwa walimu, kwa sababu hawanufaiki nayo hata kidogo. Unataka kuniambia kwamba baada ya kuondoa walimu hewa, mishahara yao wameongezewa hao waliopo kazini?


Je, serikali kutoa elimu bure walimu wananufaikaje? Labda kuna kitu kingine kizuri kilichofanywa na serikali ambacho hujakitaja na kinaweza kuwa motisha ya kazi kwa walimu hujakitaja, lakini hayo, sioni uhusiano wake na motisha kwa kazi ya ualimu.

Walimu wanataka maslahi yao yaboreshwe, wanataka mazingira mazuri ya kazi, nyumba za kuishi na mahitaji mengine ya muhimu. Sijajua iwapo serikali imeamua kuanzia kwenye elimu bure, ndipo baadaye iwaboreshee maisha au ni namna gani.

Hatua ya kutoa elimu bure ni nzuri, lakini bado inakabiliwa na changamoto nyingi, kwa kuwa kuna baadhi ya michango ambayo wazazi wanatakiwa kutoa kwa ajili ya watoto wao, lakini wengine wanakataa na kung'ang'ania tu kuwa serikali ilishatangaza elimu bure.

Mkanganyiko huo kwa namna moja au nyingine, unaweza kusababisha kukwamisha maendeleo ya elimu kwenye baadhi ya shule. Miaka ya nyuma, walimu walikuwa wanashirikiana vizuri na wazazi na kuwahamasisha wachangie chochote, ili kuwezesha walioamua kuandaa na kutunga maswali akiwa ametulia.

Sidhani kama hali hiyo ipo. Ninasema hivyo, kwa sababu hata hicho kidogo walichokuwa wakikipata hawana tena, wanapambana na wingi wa wanafunzi darasani, ambao kimsingi hawawezi kumfikia kila mwanafunzi na kujua matatizo yake kwa lengo la kumsaidia.



**THOMAS NGAWAIYA (MKURUGENZI WA TAASISI YA UTAWALA BORA NA MAENDELEO)**

TAASISI ya Utawala Bora na Maendeleo (Cegodeta), inaamini kwamba Serikali ya Awamu ya Tano, imefanya mambo makubwa katika sekta ya elimu na inaendelea kuyafanya mengine zaidi, ingawa changamoto hazikosekani.

Kwa mfano, hilo la kuondoa walimu hewa katika ajira limefanyika kwa spidi kubwa. Baada ya kumaliza kazi hiyo, iliahidi kuajiri wengine wapya ili kuziba nafasi za hao waliondolewa.

Lakini, bahati mbaya bado kumekuwapo na malalamiko kwamba walimu hawatoshi. Huu ni ujumbe tosha kuwa kasi ya kuajiri walimu wapya bado ni ndogo, hivyo niiombe na kuishauri serikali iongeze kasi ya kuajiri walimu wapya, pia kumaliza changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na walimu, ikiwamo ukosefu wa nyumba za kuishi na kutopandishwa vyeo.

Hizo ni sehemu ya motisha kwa kazi ya ualimu, kwa ajili ya kuwaongezea kasi ya kazi. Hivyo, serikali izifanyie kazi kwa spidi kubwa, ili walimu waliopo waendelee kuchapa kazi kwa bidii, kwa ajili ya kuwaandaa vizuri watoto waweze kutimiza ndoto za maisha yao ya baadaye, kwa kuzingatia kwamba kazi ya ualimu ni wito.

Vilevile wito wangu ni kwa wanafunzi wa msingi hadi kidato cha nne, kutumia vizuri fursa ya elimu bure.




**FREDRICK MASALA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HAPA nafuu ipo kwa serikali na wazazi, kwa maana kwamba serikali imefanikiwa kuondoa walimu hewa, hivyo zimerudi serikalini, pia kwa upande wa elimu bure, wazazi ndio waliopunguziwa mzigo wa ada, lakini walimu bado wanakabiliwa na changamoto nyingi za maisha.

Mfano mdogo, ni suala la masomo ya ziada ambayo walimu walikuwa wakifundisha wanafunzi na kujipatia chochote, hayo hayapo tena. Ikumbukwe kuwa, wanafunzi wanafundisha wanafunzi kwa asilimia 25 tu na asilimia nyingine 75 ni wanafunzi wenyewe kutafuta namna ya kupata vitu vya ziada, kwa ajili ya maendeleo yao kielimu.

Hivyo, ninaona bado kuna haja ya masomo ya ziada kwa wanafunzi shuleni kila upande unufaike, kwa kuwa ukiangalia kwa upande wa walimu, hata vitu vidogo walivyokuwa wakiuza shuleni, walishazuiwa miaka mingi.

Hali kama hiyo inawaweka katika mazingira magumu sana kimaisha. Cha msingi ambacho ninadhani kingefanyika kikilenga manufaa kwa walimu, ni kuwashirikisha katika maamuzi mbalimbali yanayohusu maslahi yao na elimu kwa ujumla, kwa sababu ninaamini wapo walimu wenye mawazo na maono mazuri kwa ajili ya kuboresha sekta hii muhimu.



**DK. AZAVELI LWAITAMA (MHADHIRI MWANDIMIZI MSTAAFU CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM)**

SITAKI kuzunguka sana katika maelezo yangu, ila nataka nikuambie kuwa motisha kwa walimu inaendana na kuajiri wengi, ili kupunguza kufundisha bila ya kupumzika na kulipwa mafao kama nauli ya kwenda likizo ndani ya muda, kuwapa nyumba za kuishi karibu na shule na kufundisha darasa lenye wanafunzi wasiozidi 45.

Pia, darasa liwe limesheheni vifaa vya kufundishia na motisha ni kuwapa walimu fursa ya kujiendeleza zaidi. Lingine, ni kufuta michango holela kwa wazazi mmoja mmoja, kwa wanafunzi kuanzia chekechea hadi kidato cha nne kwa shule za serikali na kuhakikisha fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi, inawekwa kwenye akaunti ya shule ya serikali, hata kama ruzuku hiyo ni ndogo haikidhi mahitaji.

Hayo ndio mambo ya msingi ambayo yakifanyika, ninaweza kusema yanaongeza motisha kwa walimu, lakini vinginevyo, bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji kutatuliwa, ili walimu waweze kufanya kazi yao bila manung'uniko ambayo tumekuwa tukiyasikia mara kwa mara.



**ROGERS KAITIRA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NI kweli serikali imefanya mambo makubwa kwenye elimu na tunawaona watoto wengi wanasoma sasa, mimi niipongeze kwa hilo na iendelee kufanya mengine zaidi, kwa sababu yapo mengi ambayo hayajaguswa sawasawa kuanzia ujenzi wa vyumba vya kutosha vya madarasa, shule kuwa na vitu vyote vinavyohitajika kwa ajili ya kujifunza na kufundishia.

Lakini kubwa zaidi ambalo ninaona linaweza kuwa, ni motisha kwa walimu ni kuboresha maslahi yao wasijisikie wanyonge. Ninaamini kwamba, hayo yakifanyika, nchi hii itakuwa sawa na kisima cha maarifa, kwani sekta ya elimu ni kichochea kikubwa cha maendeleo. Walimu ni msingi mkuu wa maendeleo ya taifa lolote duniani. Hivyo, wasionekane taaluma yao haithaminiwi.

Serikali imekuwa ikifanya jitihada kuinua elimu, lakini kwa bahati mbaya walimu wanaendelea kulalamika, hapa ina maana kuna jambo halijakaa sawa.

Nijuavyo ni kwamba, ualimu ni sekta pekee yenye watumishi wengi katika utumishi wa umma. Pamoja na wingi wao, bado wanahitaji kuhudumiwa ipasavyo, hasa kwa kuzingatia kwamba ndio wanaowandaa viongozi wa baadaye.





# Prof. Mbarawa apeleka neema ya maji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI 50,000 wa vijiji 16 vya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, wanatarajia kunufaika na mradi wa maji baada ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Profesa Makame Mbarawa kumwagiza Mhandisi wa Maji wa Halmashauri kusanifu michoro kwa ajili ya kutandaza mabomba.

Waziri Mbarawa alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kutembelea mradi huo ambao ulikuwa unasuasua kwa muda mrefu na hivyo kufifisha matumaini ya wananchi wa vijiji vilivyokuwa vinalengwa kunufaika.

Alitoa agizo la kuandaliwa michoro na kuandaa michoro kwa ajili ya kutandaza mabomba kwenda kwa wananchi baada ya wananchi kupaza sauti zao wakitaka kujua ni lini wataanza kunufaika na mradi huo ambao umetumia fedha nyingi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Matwiga, Tupyelesyeghe Mtawa, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakipewa matumaini na viongozi wa kisiasa kuwa mradi huo unaelekea kuanza kuwanufaisha lakini wanakuta hakuna kinachoendelea.

**Tunahangaika sana wananchi wa kata hii, ujio wako mheshimiwa waziri naamini utatusaidia kupata majibu, ni lini wanawake wa Kata ya Matwiga tutatuliwa ndoo kichwani?**

Alisema kwa muda mrefu wanawake wa kata hiyo wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji kwenye maeneo ambao mengine ni hatarishi kwa maisha yao, huku pia yakiwa hayafai kwa matumizi ya binadamu.

"Tunahangaika sana wananchi wa kata hii, ujio wako mheshimiwa waziri naamini utatusaidia kupata majibu, ni lini wanawake wa Kata ya Matwiga tutatuliwa ndoo kichwani?" Alihoji Mtawa.

Alisisitiza kuwa wananchi wa eneo hilo wanatumia maji ambayo wanachangia na wanyama hali ambayo inahatarisha afya zao huku pia akidai wanatumia muda mwingi kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Chunya, Noel Chiwanga, alisema changamoto ya maji katika Wilaya ya Chunya ni kubwa na hivyo wananchi wanapoona mradi wanaanza kupata matumaini mapya.

Alisema kwa muda mrefu mradi huo umewakatisha tamaa wananchi hao hali ambayo inakifanya chama hicho tawala kiwe na wakati mgumu katika kujibu maswali ya wananchi hao.

Chiwanga alisema kwa sasa wananchi wamechoka kupigwa danadana na sasa wanataka utekelezaji wa mradi huo ili wapate huduma na kwamba wao kama wasimamizi wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho ni lazima wasimamie kwa ukaribu ili kuwaondolea changamoto wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 98 na kwamba kilichobaki kwa sasa ni kutandaza mabomba kwenda kwenye makazi ya wananchi.

Alisema maelezo hayo ya wataalamu yanaanza kuleta matumaini ya wananchi kuanza kunufaika na mradi huo ambao umetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.1 tangu ulipoanza kutekelezwa.

"Hizi asilimia mbili zilizobaki ni za kuandaa mtawanyiko wa mabomba kwenda kwa wananchi pamoja na umaliziaji mdogomdogo, lakini ninaamini muda sio mrefu wananchi wataanza kunufaika," alisema Mahundi.

Kwa upande wake Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Chunya, Samwel Hechei, alisema mkandarasi wa kusanifu na kutandaza mabomba yupo tayari na kazi itaanza muda wowote.

Alisema mkandarasi huyo yuko tayari kufanya kazi hiyo kwa shilingi milioni 355 ikiwa ni pamoja na ongezeko la thamani (VAT) na hivyo akaahidi kuanza kazi mara moja.

Baada ya malalamiko ya wananchi hao na maelezo ya viongozi, Waziri Mbarawa alitoa maelekezo ya kuanza mara moja utekelezaji ili wananchi waanze kupata huduma baada ya miezi minne.

"Mradi kukamilika ni jambo moja, lakini wananchi kupata maji ni jambo jingine, sasa mhandisi wa maji wa wilaya, wiki ijayo wasiliana na mhandisi mshauri ili aandae michoro kwa ajili ya kuyatoa maji hapa na kuyapeleka vijijini," aliagiza Prof. Mbarawa.

Alimtaka mhandisi huyo kumpatia taarifa wiki ijayo baada ya shughuli hiyo kuanza kufanyika ili kurahisisha usimamizi na akasisitiza kuwa atakuwa anafuatilia.

## DC aagiza wajasiriamali wenye mafunzo

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

MKUU wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, John Palingo, ameiagiza ofisi ya Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo kuvipa kipaumbele wakati wa utoaji wa mikopo ya halmashauri kwa vikundi vya wajasiriamali vilivyopatiwa mafunzo maalumu ya uendeshaji wa biashara.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa mgeni rasmi kwenye Sherehe za Mradi wa Uwezeshaji Biashara (Sirolli) unaotekelezwa na Shirika la Heifer International kwa kushirikiana na Taasisi ya Sirolli ya nchini Marekani katika Wilaya ya Mbozi.

Alisema wananchi hao wamepata elimu ambayo itawasaidia kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati, hivyo ni vema wapewe kipaumbele kuliko wale ambao hawana mafunzo hayo.

Alilipongeza Shirika la Heifer kwa kufadhili mradi huo kwa madai kuwa utakuwa na manufaa kwa wananchi hao hasa wajasiriamali wadogo kwa madai kuwa watakuwa na uwezo wa kuendesha biashara zao kisasa na kuweza kukua kiuchumi.

"Elimu hii ni muhimu sana hasa wakati huu ambapo serikali ya awamu ya tano inasisitiza uchumi wa viwanda, sasa hawa wenzetu wametoa elimu ya bure kabisa kwa hawa wajasiriamali, sasa ni vema na sisi tukawapa kipaumbele kwenye utoaji wa mikopo," alisema Palingo.

Alisisitiza kuwa baada ya kukagua baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali walionufaika na mradi huo wanazalisha bidhaa nzuri na wanaendesha biashara zao kwa mbinu za kisasa zaidi.

Aliwashauri baadhi ya wazalishaji hao hasa wanaozalisha vyakula kuhakikisha wanaziona mamlaka zinazohusika ikiwamo Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Shirika la Viwango Tanzania TBS, ili zithibitishe ubora wa bidhaa hizo.



Baadhi ya vijana wakipakia mabati yasiyokuwa na viwango kwenye moja ya gari jijini Mbeya kwa ajili ya kwenda kuyaharibu baada ya maofisa wa Shirika la Viwango nchini (TBS), kubaini mabati hayo kuendelea kuuzwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wafanyabiashara wakaidi agizo la TBS

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kukamata zaidi ya mabati 2,000 ya migongo mipana yaliyotengenezwa chini ya kiwango jijini Mbeya na kuzuia yasiuzwe tena, wazalishaji na wafanyabiashara wamekaidi agizo hilo kwa kuendelea kuyasambaza kwa kuwauzia wananchi wa vijijini.

Hayo yalibainika juzi wakati wakaguzi ubora wa TBS kutoka makao makuu na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walipofanya ukaguzi kwenye viwanda vya kuzalisha bidhaa hiyo na kwenye maghala ya kuhifadhia ambapo walibaini mabati hayo yakiendelea kuuzwa.

Kufuatia hali hiyo shirika hilo liliamua kubeba mabati hayo na kwenda kuyahifadhi kwenye ghala maalumu kwa ajili ya kusubiria taratibu zikamilike ili kuyaharibu.

Wataalamu hao walibeba bati 2004 walizozikamata awali walipofanya ukaguzi kwenye viwanda viwili vya Dragon Mabati, Alaf limited na kwenye ghala la Kampuni yenye asili ya China ya Yalin International ambalo lilikutwa na mabati mengine zaidi ya 1,000 ambayo yalikuwa yameletwa baada ya msako wa awali.

Mkaguzi ubora mwandamizi wa TBS kutoka makao makuu, Mhandisi Donald Manyama, alisema walibaini kuwa bati hizo zenye migongo mipana za kiwango cha gage 30 zinaendelea kuuzwa maeneo ya vijijini walipofanya ukaguzi wa kushtukiza wilayani Rukwa.

Alisema baada ya kubaini hali hiyo waliamua kurudi Mbeya kwa ajili ya kuzihamisha kutoka kwenye maeneo ya viwanda na maghala walikozuia zisiuzwe na ndipo wakaamua kuzibeba na kwenda kuzihifadhi wenyewe.

Alisema shirika hilo lilibaini kuwa bati hizo zinaendelea kuzalishwa na kuuzwa baada ya kukagua katika ghala la Yalin na kukuta shehena mpya ya mabati zaidi ya 1,000 yakiwa yameingizwa kutoka jijini Dar es Salaam.

Ofisa Uhusiano wa TBS kutoka Makao Makuu, Roida Andusamile, aliwataka wananchi kuacha kununua bati hizo kwa madai kuwa zitawasababishia hasara kubwa kutokana na kuharibika baada ya muda mfupi.

Alisema aina hiyo ya bati kwa mujibu wa sheria haziruhusiwi kuzalishwa wala kuuzwa kwa wananchi na hivyo akawataka wazalishaji kuacha kukiuka masharti ya leseni zao akidai kuwa vitendo hivyo vitawaingiza hasara kubwa.



HABARI DODOMA

# Watakiwa kuimarisha mifumo uwajibikaji afya

**Na Mwandishi wetu,** BAHI

WARATIBU wa Timu za Usimamizi Huduma za Afya Mikoa (RHMT) na Halmashauri (CHMT) nchini, wametakiwa kuhakikisha wanaimarisha mifumo ya uwajibikaji ili kuleta mabadiliko katika sekta ya afya nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Dk. Dorothy Gwajima, katika ziara yake ya kikazi ya kukagua uwajibikaji wa timu hizo kwenye Kituo cha Afya cha Bahi.

Alisema watapimwa kwa uwajibikaji na kwa wale wote wasiopenda kubadilika watapangiwa majukumu mengine wanayoyamudu.

"Hakuna haja ya kila siku semina, warsha, mikutano halafu ukienda vituoni, mambo ya kawaida kabisa unakuta hayako vizuri wala takwimu hakuna na hakuna maelezo yoyote yenye mashiko kwa nini hali imekuwa hivyo ilivyo," alisema.

**Inasikitisha kuona baadhi ya waratibu wanahudhuria semina, mikutano na warsha mbalimbali lakini hakuna mabadiliko na wengine hukaa ofisini.**

Dk. Gwajima alisema pamoja na kazi nzuri zinazofanywa katika baadhi ya maeneo, yapo masuala ya msingi ambayo yanahitaji kusimamiwa vizuri zaidi na hayahitaji chochote cha ziada zaidi ya uwajibikaji imara wa viongozi waliopewa dhamana.

Alisema serikali haitavumilia kuwa na waratibu ambao hawaleti msukumo katika kuleta mabadiliko ya uwajibikaji na badala yake wamebaki kusafiri na kuhudhuria semina, warsha na mikutano ambayo haileti tija katika maeneo yao ya kazi.

"Inasikitisha kuona baadhi ya waratibu wanahudhuria semina, mikutano na warsha mbalimbali lakini hakuna mabadiliko na wengine hukaa ofisini."

Aliongeza; "Hata wanapoenda kutembelea vituo hawaoni upungufu na wakiyaona hawaandai mpangokazi wa kuboresha na wakiandaa mpangokazi hawafanyi ufuatiliaji bali wanafungia taarifa kwenye makabati katika utendaji kazi wa sasa."

Aidha, alisema waratibu ambao wanashindwa kwenda na kasi ya usimamizi unaotakiwa enzi hizi, wajipime mapema kabla ya kupimwa.

Gwajima aliwaagiza waratibu kufanya usimamizi na ufuatiliaji kwa weledi mkubwa ambapo kila mmoja atatakiwa kuonyesha ameona nini na mpangokazi ni upi na umefanikisha ufumbuzi wa changamoto ngapi, kama umekwama je, umechukua hatua gani za kuomba msaada.

Alitoa wito kwa timu za afya nchini kujifunza toka timu za Dodoma ambao kwa kutumia fursa ya kuwa karibu na wizara wameona kwa vitendo nini kinatakiwa ili nao waanze mara moja kuimarisha mifumo na kuanza mbio za mabadiliko kabla zoezi la tathmini ya wizara halijawafikia.



Kamishna Operesheni wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, Billy Mwakatage (kulia) na timu yake akiwa katika picha ya pamoja jana na Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya miundombinu, Ignace Mujwahuzi (kushoto), wakati alipotembelea Ofisi ya Mkoa wa Tabora. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Ndugai ataka ATCL isirudi nyuma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amelitaka Shirika la Ndege Tanzania(ATCL) kuhakikisha halirudi nyuma kiutendaji ili kuondokana na matatizo yaliyokuwapo siku za nyuma ikiwamo abiria kupata usumbufu.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua ofisi ya ATCL mkoani hapa.

Alisema Watanzania wanajivunia juhudi za kuimarisha shirika hilo na kupanua mtandao wa usafiri wa anga ndani na nje ya nchi.

"Tusirudi kule tuliko toka ATCL, na ni vizuri kuweka kumbukumbu ili kuonyesha tulikotoka kwenye dimbwi gani, nakumbuka kipindi kile mtu anaenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro(KIA), unapanda ndege nyingine unaenda ukirudi jioni unakutana na abiria wa ATCL wa tangu saa 12 asubuhi."

Aliongeza "Wakati mwingine abiria walikuwa wakipanda kwenye ndege na kushushwa bila kuambiwa kitu, unajikuta roho ipo juu ukiambiwa pandeni, unawaza sijui nipande au nishuke."

Pamoja na hayo, Ndugai aliwataka Watanzania wote kutumia huduma za ndege hizo ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kuinua usafiri wa shirika hilo ambalo kwa asilimia 100 ni mali ya Tanzania.

"Nitoe rai kwa wabunge, maofisa wa serikali, wafanyabiashara na wajasiriamali kutumia huduma za ATCL popote zilipo ndani na nje ya nchi ili kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ya kufufua na kulijengea uwezo shirika hilo,"alisema.

Aidha, alisema kwa kutumia usafiri huo wa ndani na nje ya nchi na katika nchi mbalimbali inakofika, ni uzalendo ambao hata mashirika ya ndege ya nje yanafanya hivyo, isipokuwa inapokuwa kuna sababu maalumu zinazochangia kutotumia usafiri huo.

"Pia niwaase mawakala 300 wa shirika kuzitangaza huduma nzuri na bora za ATCL popote zinapotolewa na kuzionyesha kwamba ni za ubora wa hali ya juu na za daraja la juu," alisema.

Spika alimpongeza Mmiliki wa Kiwanda cha Mvinyo, Archard Kato, kwa kuzalisha bidhaa ambazo zinatumika katika ndege za ATCL, kwa kuzitumia bidhaa hizo kunatangaza uzalishaji wa zao la zabibu ndani na nje ya nchi.

"Sisi kama Bunge tutaendelea kuunga mkono juhudi hizi za serikali za kufufua shirika hilo ambalo linalenga kupanua huduma zake ndani na nje ya nchi na kuwa miongoni mwa shirika kubwa zaidi barani Afrika la usafiri wa anga," alisema.

# Wakazi wa Nzuguni wamwangukia Lukuvi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI 127 wa mtaa wa Nzuguni 'A' jijini Dodoma wamemuomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuingilia kati mgogoro wa ardhi kati yao na halmashauri ya jiji hilo.

Mgogoro huo ambao unatokana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuchukua hekari 103 za wananchi kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa kisasa wa mpira wa miguu kwa ufadhili wa Serikali ya Morocco.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi hao walisema kuwa wamelalamika katika maeneo mbalimbali, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa huku serikali ikiwa katika hatua za mwisho kuanza ujenzi wa uwanja huo.

Yonah Mnofu, alisema kuwa wao hawapingi ujenzi wa uwanja huo kwa kuwa ni sehemu ya maendeleo bali wanacho kilalamikia ni haki itendeke juu ya maeneo yao.

Alisema kuwa eneo la uwanja ambalo lilikuwa limetengwa toka Utawala wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao (CDA), lakini wanashangaa hivi sasa kuona Halmashauri ya Jiji kuongeza eneo hadi katika mashamba yao.

"Sisi hatupingi ujenzi wa uwanja bali haki ifuatwe tupatiwe haki yetu, tulipwe fidia kama haiwezekani kulipwa fidia basi tupatiwe na sisi viwanja kama ambavyo wanataka kuwauzia wawekezaji," alisema.

Mnofu alisema kuwa eneo ambalo wanalilalamikia ni lile la hekari 103, ambalo Halmashauri ya Jiji imeliongeza kwa madai kuwa ni viwanja kwa ajili ya wawekezaji katika uwanja huo ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya watu 85,000.

Velian Heziron, alisema kuwa yeye ni mama mjanae mwenye watoto nane, eneo lake lililochukuliwa kwa ajili ya uwanja huo, alikuwa akilitumia kwa ajili ya kilimo ili kuweza kuendesha familia yake.

Alisema kuwa kutokana na Halmashauri ya Jiji kuchukua maeneo yao bila makubaliano yeyote hali hiyo itawaathiri kutokana na kutolipwa chochote.

"Tunaiomba serikali iangalie sana familia zetu haya mashamba tumekuwa tukiyategemea kwa ajili ya kilimo ili kuweza kulisha familia zetu, lakini sasa kama watayachukua halafu tusilipwe chochote tutakuwa hatujatendewa haki kabisa," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema kuwa, tayari alishapokea barua kutoka kwa wananchi hao wakilalamika kuchukuliwa maeneo hayo.

# RC ashauri kuweka mikakati kueneza Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, ameitaka Jumuiya ya Uendelezaji wa Lugha ya Kiswahili Zanzibar (JULUKIZA), kuhakikisha wanasimamia vyema mipango na malengo waliyojiwekea ili kuona lugha hiyo inakuwa na kuenea ndani na nje ya nchi kuimarisha utamaduni wa Mzanzibar usipotee.

Ayoub aliyasema hayo wakati wa ghafla maalum ya uzinduzi wa kitabu cha mtambue Chimbeni bin Kheir na kutimia kwa mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwa jumuiya hiyo ghafla ambayo ilifanyika katika ukumbi wa saana Rahaleo mjini Zanzibar.

Alisema jumuiya hiyo ina dhima kubwa ya kuhamasisha na kuongeza uelewa wa jamii juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili ili kulinda rasilimali ya lugha hiyo isipotee na kuharibiwa kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla kulingana na taaluma waliyonayo wajumbe wa jumuiya hiyo.

Aidha, Mkuu wa Mkoa huyo, alizitaka taasisi zingine za kiraia kuungana pamoja kuhakikisha lugha ya Kiswahili inalindwa na kukuzwa ili kuongeza ushindani wa matumizi bora ya lugha ulimwenguni pamoja na kutoa matunda ya upatikanaji wa ajira kwa Wazanzibar katika soko la dunia.

Ayoub aliipongeza jumuiya ya uendelezaji lugha ya Kiswahili kwa kutekeleza kwa vitendo malengo ya serikali ya kuanzishwa kwa jumiya za kiraia ambazo zinatekeleza shughuli mbalimbali kwa maslahi ya jamii.

Alisema jumuiya hiyo ina msaada mkubwa kwa wananchi katika kuipa kipaumbele lugha hiyo ili kuongeza wigo kwa warithi wa lugha hiyo, wakiwamo vijana na waweze kukiendeleza na kuzungumza kwa ufasaha kwa kuwa lugha hiyo ipo katika nafasi nzuri katika lugha zinazozungumzwa ulimwenguni.

Mkuu wa Mkoa huyo alizindua kitabu cha Chimbeni Bin Kheir na kuwataka wasanii nchini waendelee kutunza mila, silka na desturi ili kulinda utamaduni wakati wanapoigiza sanaa zao kwa lengo la kukikuza Kiswahili.

Mjumbe wa Jumuiya hiyo, Dhalha Mohammed Muhsini, akisoma risala yao, alisema harakati za kukikuza Kiswahili zinaendelezwa ikiwamo kuandaa majarida, kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wananchi wa mataifa mbalimbali pamoja na makongamano ili kusaidia jamii kuona umuhimu wa lugha hiyo.

# Mchanga wakwamisha ujenzi wa miradi Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

UHABA wa mchanga Zanzibar umekwamisha miradi ya ujenzi wa shule 14 zinazojengwa na serikali katika wilaya mbalimbali za Unguja.

Wakizungumza wakati Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majenzi Zanzibar, ilipotembelea majengo ya shule hizo, Mhandisi Makaazi wa mradi wa shule hizo, Nderema Shilima, alisema kuwa upungufu wa mchanga umekwamisha harakati za ujenzi huo.

Alisema kuwa mradi huo ni wa mwaka mmoja ambao ulianza Septemba mwaka jana na ulitarajiwa kumalizika Septemba mwaka huu, lakini hivi sasa umefikia asilimia 25.

Alisema kuwa kutokana na changamoto ya mchanga majengo hayo hayataweza kukamilika kwa muda wa mwaka mmoja kama ilivyotarajiwa.

**Yasije yakatokezea kama ujenzi wa majengo ya shule zilizopita ambapo majengo yake yana matatizo kutokana na kutokuwa na ubora.**

"Kwa muda wa mwezi mmoja sasa tumekosa raslimali ya mchanga hali ambayo imeathiri utendaji kazi wa ujenzi wa majengo ya shule hizi," alisema.

Naye mjumbe wa bodi hiyo, Ramadhan Mussa Bakari, alisema kuwa usimamizi wa majengo siyo mzuri kwa sababu wengi hawajasajiliwa katika bodi hiyo.

Alisema lazima wasimamizi wa majengo hayo walizingatie hilo kuhakikisha wahandisi wa majengo hayo wanajisajili ili kuweza kupata ujenzi bora na salama.

"Yasije yakatokezea kama ujenzi wa majengo ya shule zilizopita ambapo majengo yake yana matatizo kutokana na kutokuwa na ubora," alisema.

Aidha, alisema kuwa sio jambo la busara shule zote 14 kusimamiwa na mhandisi mmoja kwa upande wa mshauri elekezi kwa kuwa atashindwa kusimamia vigezo katika ujenzi huo.

Aliishauri serikali kuongeza mhandisi mshauri elekezi ili waweze kusimamia majengo hayo kuepusha matatizo mbalimbali ikiwamo kuporomoka.

"Wiki hii shule moja nchini Nigeria jengo limedondoka na masuala ya kudondoka majengo ulimwenguni yamekuwa yakitokea kila kipindi, hivyo tujikinge na masuala hayo kwa kuhakikisha wahandisi wanafuata ramani," alisema.

Kwa upande wake mrajisi wa bodi hiyo, Hawa Mzee, alisema katika ziara yao ya kutembelea majengo hayo wamegundua kasoro ndogo ndogo ikiwamo makandarasi wanaosimamia majengo hayo hawajajisajili katika bodi yao.



Wajumbe wa Bodi ya Wahandisi na Wakadiriaji Majengo Zanzibar, wakiangalia ujenzi wa karo katika Shule ya Mwanakwerekwe, wakati walipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa shule hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Dk. Shein atoa neno kwa watendaji

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wadau wanaotunza na kusimamia rasilimali za ardhi kufanya kazi kwa uzalendo na kuzingatia misingi ya uaminifu, uadilifu na uwajibikaji.

Dk. Shein aliyasema hayo wakati alipofunga semina kuhusu masuala ya ardhi na rasilimali zisizorejesheka.

Alisema ni muhimu kwa watendaji kufanya kazi zao kwa kuzingatia misingi ya uzalendo na kutambuwa kuwa rasilimali za ardhi na mali zisizorejesheka ni nyenzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa ustawi wa nchi. Alisema kuna umuhimu wa kukumbushana juu ya dhana ya uzalendo miongoni mwa Wazanzibari, kwa kuwa ni miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele tangu wakati wa Mapinduzi.

Aidha, Dk. Shein alisema njia sahihi katika kupata mafanikio ni lazima watendaji wa serikali kuimarisha umoja, mshikamano na kufanya kazi kwa nidhamu.

Akitoa mada katika semina hiyo ya watendaji wa serikali, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Jaji Mshibe Ali Bakari, alisema sheria zilizopo ni nzuri ila kinachokosekana kwa sasa ni uzalendo miongoni mwa watendaji na wasimamizi wa sheria za ardhi.

Alisema serikali ina dhima ya kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa kutunza na kusimamia sheria hizo na hatua hiyo itaifanya jamii kusimama kidete katika ulinzi wa rasilimali za ardhi.

"Tutoe elimu kwa wananchi ili tulete uzalendo, kama mchanga umechimbwa hauwezi kurudi tena na kama mwembe umekatwa hauwezi kurudi, tuwe wazalendo kulinda sheria zetu, tusikimbilie mahakamani, alisema.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Said Hassan Said, alisema changamoto zilizopo juu ya uharibifu wa raslimali ya ardhi zinatokana na serikali kushindwa kuchukuwa hatua za kisheria dhidi ya wakosaji kama zilivyobainishwa katika sheria na katiba ya nchi.

"Anayetakiwa kuilinda na kuihifadhi ardhi hii kwa mujibu wa sheria na katiba ni kila Mzanzibari," alisema.

Alisema endapo taratibu za kutambuliwa ardhi, kupimwa, kusajiliwa au kuhaulishwa kisheria zitafuatwa, hakuna sababu ya kuwapo kwa changamoto za ardhi nchini.

HABARI KIMATAIFA

# Watu 10 wafariki dunia kukosa chakula Kenya

**NAIROBI,** Kenya

ZAIDI ya watu 10 wamefariki kutokana na ukame katika Jimbo la Turkana nchini Kenya, huku zaidi ya watu 800,000 wakiendelea kuteseka kutokana na njaa na kiu.

Taarifa illiyotolewa jana na Wizara ya Kudhibiti Majanga na Utumishi wa Umma Jimbo la Turkana ilieleza kuwa eneo hilo limekuwa likikumbwa na ukame mara kwa mara.

Serikali ya Jimbo la Turkana wiki iliyopita iliwahakikishia wananchi wa eneo hilo kwamba imeidhinisha mpango wa usaidizi kuwakinga wakazi kutokana na madhara ya ukame uliopo.

Katika kijiji cha Kakwanyang' Turkana ya Kati, mizoga ya wanyama iliyotapakaa, na miti iliyokauka inaashiria hali ya ukame katika eneo hilo.

Wakazi wengi katika kijiji hicho hawajapata chakula chochote kwa muda wa siku tano zilizopita.

Kwa sasa wakazi wa eneo hilo wanalazimika kupunguza makali ya njaa kwa kula matunda ya mwituni yajulikanayo kama mkoma.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Moru Lomutan ambaye ni mama wa watoto sita analazimika kula tunda la mkoma ili liwe chakula kwake.

"Najaribu kuligonga hili tunda kwa mawe ili nile, kwa sababu sina hata nguvu ya kuliuma mdomoni, alisema mama huyo.

Taarifa zaidi kutoka eneo hilo zinaeleza kuwa katika bwawa la maji, watu walikuwa wamejaa, kinamama na watoto wakichota maji.

Aidha, karibu na bwawa hilo mizoga ya mbuzi na kondoo imetapakaa, ambao wengi walifariki kwa kukosa chakula na maji.

Anna Emaret ambaye ni mkazi wa eneo hilo alisema amepoteza mifugo yake 20.

Alisema amekuwa akigawana chakula na mifugo yake, lakini chakula kilipoisha, wakafa.

"Kondoo wangu wote wamekufa, mbuzi pia wamekufa. Sasa sina mifugo, sina chakula, serikali isipotusaidia, tutakufa tu kama mifugo yetu," alisema mama huyo.

Mariam Loolio ni ajuza mwenye umri wa miaka 85 alisema kwa muda wa siku tano hajala chochote.

"Nimekaa hapa nikiisubiri serikali ituletee chakula. Mnavyoniona mimi ni mzee, tena kipofu. Hakuna jinsi ninavyoweza kutafuta chakula, hakuna kabisa. Kwa hivyo nasubiri tu serikali ije iniokoe ili nisife njaa. Sina namna," alisema Mariam.

Ukame umekuwa ukilikumba eneo hilo mara kwa mara na pindi unapotokea wakazi na mifugo huwa hatarini.

Nchini Uganda katika Jimbo la Karamoja karibu na eneo hili la Turkana, Rais Yoweri Museveni alijenga bwawa ambalo hutumiwa na jamii ya Karamoja ambayo ni jamii ya wafugaji.

"Kwanini serikali ya jimbo na ile serikali kuu zisiungane pamoja na kutafutia wananchi suluhisho mwafaka na la kudumu kama ilivyofanywa na Rais Museveni upande ule mwingine? " Alihoji Paul Jaling'a, kiongozi wa vijana katika Jimbo la Turkana na kuongeza:

"Inapaswa sisi kama vijana tuelimishwe jinsi ya kufuga mifugo kwa manufaa ya biashara. Isiwe tu kwamba tunafuga mifugo kisha kiangazi kikianza, tunarudi kuwa maskini," alisema.

Alieleza kuwa kuuza mifugo wakati wa mvua na kuwekeza fedha ili kujinusuru wakati wa kiangazi itasaidia sana katika kuhakikisha kwamba ukame unasalia kuwa historia.

**BBC**



Wakazi mjini Beira Msumbiji wakiwa juu ya paa za nyumba baada ya kimbunga Idai kupiga mji huo na kusababisha mafuriko kwenye pwani ya Msumbiji na kuua watu zaidi ya 120. **PICHA AFP**

## Waandamanaji Ufaransa wachoma majengo, wapambana na polisi

**PARIS,** Ufaransa

JESHI la Polisi Ufaransa limelazimika kutumia mabomu ya machozi, mipira ya maji ya moto kuwasambaratisha waandamanaji wanaopinga serikali.

Waandamanaji hao waliovalia fulana za njano maarufu Yellow Vest walichoma moto tawi moja la benki na kuvunja maduka mjini Paris.

Tawi la benki ya Bangue Tarneaud liliwaka moto kabla ya wafanyakazi wa zimamoto kuwasili kwenye eneo la tukio, huku vituo viwili vya habari navyo vilishika moto ulipowashwa mitaani.

Hali hiyo iliwalazimu polisi mjini Paris kufyatua mabomu ya kutoa machozi na mipira ya maji ya moto kuwasambaratisha waandamanaji hao, ambapo baadhi yao walikuwa wakirushia mawe polisi wa kutuliza ghasia na kuwasha magari moto mbele ya eneo lenye mnara maarufu mjini Paris la Arc de Triomphe.

Hata hivyo, polisi waliwakamata waandamanaji zaidi ya 80 wakati wakijaribu kuvunja maduka yaliyopo mtaa wa Champs Elysees pamoja na mgahawa wa kifahari wa Fouquet.

**VOA**

## Ajali ya ndege Ethiopia yafananishwa Lion Air

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

MAOFISA wa Ethiopia wamesema maelezo yaliyonaswa katika visanduku vya mawasiliano ya ndege chapa Boeing 737 MAX nchini Ethiopia na Indonesia, yanafanana.

Waziri wa Usafiri wa Ethiopia, Dagmawit Moges, alisema uchunguzi wa kisanduku cha data za ndege ya shirika la ndege la nchi yao umedhihirisha kuna hali inayofanana na ile ya Lion Air ya Indonesia iliyotokea mwaka jana na kwamba hali hiyo itasababisha kufanyika uchunguzi zaidi.

Alisema ripoti ya awali, inatarajiwa kuwekwa wazi ndani baada ya siku 30 zijazo.

Kampuni la Boeing ya Marekani ilisema inatengeneza programu mpya ya kompyuta ili kuibadilisha ile inayokosolewa, huku shinikizo likizidi dhidi ya shirika la Marekani linalosimamia safari za ndege, baada ya kutangaza hapo awali kuwa usalama wa ndege hauna kasoro.

Ripoti zinaeleza kuwa shirika hilo linachunguzwa na idara ya usafiri.

Ndege zaidi ya 300 chapa Boeing Max 8 na Max 9 zimezuiliwa kuruka kote ulimwenguni kufuatia ajali mbili za ndege hizo zilizotokea katika kipindi cha miezi mitano nchini Ethiopia na Indonesia na kusababisha vifo vya watu watu 350.

Ndege zote zilizoanguka ni aina moja, Boeing 737 Max 8 na tayari uchunguzi unaendelea nchini Ufaransa, kubaini mawasiliano yaliyokuwapo kabla ya kuanguka ili kufahamu kilichosababisha ajali hiyo.

Wakati huo huo, uongozi wa Boeing kampuni iliyotengeneza ndege hiyo umesema unaunga mkono uchunguzi, ili kufahamu chanzo kilichotokea.

Juzi, jamaa, ndugu na marafiki wa abiria waliofariki katika ajali hiyo walikuwa na misa ya kuwakumbuka wapendwa wao katika makanisa ya Coptic jijini Addis Ababa na Nairobi nchini Kenya.

Serikali ya Ethiopia ilisema uchunguzi wa mabaki ya abiria waliofariki katika ajali hiyo utachukua miezi sita, lakini kwa familia zimepewa udongo kutoka eneo la ajali hiyo kuendelea na maziko. **RFI**



## New Zealand kuimarisha sheria ya umiliki bunduki

**WELLINGTON,** New Zealand

WAZIRI Mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern (pichani juu), amesema siku chache zijazo atatangaza sheria mpya kuhusu umiliki wa bunduki katika nchi hiyo, baada ya kutokea shambulizi kwenye misikiti miwili ambalo watu 50 waliuawa.

Akizungumza na waandishi wa habari, kuhusiana na shambulizi hilo, Ardern alisema katika muda wa siku 10 atakuwa ametangaza mabadiliko katika sheria ya umilikaji wa bunduki, ambayo itaifanya New Zealand kuwa salama zaidi.

Mkutano huo umefuatia kikao cha Baraza la Mawaziri kilichoongozwa na Ardern, ambapo mawaziri wote wamekubaliana kimsingi kuhusu mageuzi hayo.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Ardern alikuwa pamoja na naibu wake, Winston Peters, kiongozi wa chama cha New Zealand First ambacho ni mshirika katika serikali.

Siku za nyuma chama hicho kilipinga mabadiliko katika sheria ya bunduki, lakini wakati huu kimebadilisha mawazo.

Kiongozi wake, Winston Peters, alisema shambulizi la mwishoni mwa wiki limebadilisha hali ya mambo, na kwa hivyo sheria pia zinapaswa kubadilika.

Alisema sheria za New Zealand kuhusu umilikaji binafsi wa bunduki zilikuwa legevu sana, na raia wengi wamekuwa wakiitilia shaka kwa muda mrefu.

"Nimeeleza bayana kwamba wa-New Zealand wengi wamekuwa wakiuliza maswali kuhusu upatikanaji wa silaha za kivita mikononi mwa watu nchini. Hata hivyo, jibu kamili nitalitoa baada ya kuyashughulikia maamuzi ya baraza la mawaziri la leo. Bado yapo mambo ya msingi yanayopaswa kutazamwa kwa kina, nataka kufanya hivyo, haraka iwezekanavyo," alisema Ardern.

**DW**

# Kigogo OBC asomewa mashtaka mapya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa kampuni ya uwindaji ya Otterlo Business Corporation (OBC), Isack Mollel (59), iliyoko Loliondo, wilayani Ngorongoro, amepandishwa kizimbani kwa mara ya pili na kusomewa mashtaka 37 ya kuajiri raia wa kigeni kinyume cha sheria za nchi za kutoa ajira kwa wageni.

Kabla ya kusomewa mashtaka hayo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Mollel alifutiwa kesi namba moja ya mwaka huu, iliyokuwa inamkabili ya kuajiri raia 10 wa kigeni kinyume cha sheria za ajira.

Aidha, aliunganishwa kwenye kesi namba 74 ya mwaka huu, inayowahusu washtakiwa 10 waliokamatwa eneo la Loliondo kwa kufanya kazi bila vibali.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Niku Mwakatobe, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Martenus Marandu, akisaidiwa na Immanuel Mweta kutoka Idara ya Kazi Mkoa wa Arusha, aliiomba mahakama hiyo kuondoa kesi namba moja ya mwaka huu, inayomkabili Mollel akidai kuwa upande wa Jamhuri hauna nia ya kuendelea nayo na mahakama iliridhia ombi hilo.

"Mheshimiwa Hakimu, upande wa Jamhuri chini ya sheria namba 234(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai kifungu cha (20) kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, tunaomba kuiondoa kesi hii mahakamani kwa kuwa hatuna nia ya kuendelea nayo," alidai.

Baada ya ombi hilo kukubaliwa, Marandu aliendelea kuileza mahakama kuwa baada ya upelelezi kufanyika wa kesi namba 74 inayowakabili raia 10 wa kigeni, wameona kuna kila sababu ya kumwongeza Mollel na kuomba kubadilisha hati ya awali ya mashtaka na walikubaliwa na mahakama hiyo.

Raia hao ni pamoja na Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali.

Akimsomea mashtaka mapya 37 ya kuajiri raia wa kigeni bila kufuata sheria ya ajira kwa wageni, pamoja na kutokuwa na kibali cha msamaha, Wakili Mweta aliileza mahakama hiyo kuwa Mollel alitenda kosa hilo kati ya Novemba, mwaka jana na Januari mwaka huu, katika barabara ya Kanisa lililopo jijini hapo.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Mollel alikana mashtaka yote na kurejeshwa rumande, kutokana na kesi nyingine ya uhujumu uchumi ambayo haina dhamana, inayomkabili katika mahakama hiyo.

Mapema, Mollel alikuwa anakabiliwa na mashtaka 10 ya kuajiri raia hao wa kigeni, lakini upelelezi umeonyesha pia aliajiri raia wengine 27 wa kigeni kinyume cha taratibu za kisheria za kuajiri wageni na bila kuwa na kibali cha msamaha, ambao wameshaondoka hapa nchini, lakini vielelezo vyao vipo.

Wakati huo huo, kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mollel katika mahakama hiyo, mbele ya Hakimu Mwakatobe, iliahirishwa kutokana na upelelezi wa kesi hiyo kutokamilika.

Baada ya kesi zote mbili kumalizika, Mwakatobe aliahirisha hadi Aprili Mosi, mwaka huu. Aidha, raia hao 10 dhamana yao inaendelea na Mollel alirejeshwa mahabusu katika Gereza Kuu la Kisongo.

## Mtoto huyu anatafutwa



**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO Agnes Lucas (9), ambaye ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Tuangoma, jijini Dar es Salaam, anatafutwa na dada yake baada ya kutoweka nyumbani kwao.

Dada wa mtoto huyo, Ziada Saburi, aliiambia Nipashe jana kuwa mtoto huyo alitoweka nyumbani Tuangoma Machi 14, majira ya saa mbili usiku. Kabla ya kutoweka, mtoto huyo alikuwa anacheza na watoto wenzake.

"Tulifikisha taarifa za kutoweka kwa mdogo wangu Kituo cha Polisi Kongowe. Tumefungua jalada lenye namba KONG/RB/239/2019 na pia tumeshakwenda kwa ndugu na jamii, Hospitali za Temeke na Amana, huko kote hakuna taarifa zake," Saburi alisema.

Aliwaomba wasamaria wema watakaomwona mtoto huyo, watoe taarifa katika kituo chochote cha polisi na wawasiliane naye kupitia simu namba 0712-868301 au 0712-3933144.



Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Benki ya CRDB, Hilda Rweshane, akizungumza wakati wa kufunga mkutano kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kwenye Uwekezaji wa Soko la Mitaji na Dhamana ulioandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya maombi kutaifisha mali za DECI, Aprili Mosi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, imepanga kusikiliza maombi ya kutaifisha mali za Kampuni ya Development Entrepreneurship for Community Initiative (DECI), Aprili Mosi, mwaka huu, yaliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

DPP amefungua maombi hayo akitaka mahakama iamuru kutaifishwa mali za DECI ikiwamo magari ya kifahari, Sh. bilioni 14.1, nyumba na viwanja kuwa mali ya serikali.

Maombi hayo yalitajwa jana mbele ya Jaji Stephen Magoiga.

Upande wa mlalamikaji uliongozwa na DPP Biswalo Mganga, akisaidiana na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka (DDPP), Osward Tibabyekomya.

Upande wa walalamikiwa uliongozwa na Majura Magafu.

DPP alidai kuwa waliwasilisha kwa walalamikaji hati ya maombi Machi 7, mwaka huu na kwamba ofisi yake ilichapisha tangazo kupitia magazeti ya serikali, Habari Leo, Daily News na gazeti la Uhuru.

Alidai kuwa hata hivyo walalamikaji hawajawasilisha kwao hati kinzani na kwamba hawana majibu ya ushahidi dhidi yao.

Hata hivyo, upande wa walalamikiwa ukiongozwa na Wakili Magafu, uliomba mahakama impe muda kwa ajili ya kuwasilisha hati kinzani kwa sababu taarifa ya maombi hayo alipewa Ijumaa iliyopita.

Mahakama ilikubali ombi la walalamikiwa, imetoa siku saba wawasilishe kiapo kinzani Machi 25 na DPP kuwasilisha majibu Machi 26, mwaka huu. Aprili Mosi, mwaka huu maombi yatasikilizwa.

Katika maombi ya msingi, DPP Mganga, anaiomba mahakama hiyo itoe amri ya kutaifishwa mali za kampuni hiyo yakiwamo magari 11, nyumba, viwanja vinane na fedha kuwa mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Maombi hayo yaliyosajiliwa kwa namba 42/2019, walalamikiwa ni waliokuwa viongozi wa DECI, Jackson Mtares, Dominick Kigendi, Timotheo Ole Loitg'nye na Samwel Mtares.

DPP anaiomba mahakama hiyo kutoa amri ya kutaifishwa na kuwa mali ya serikali, nyumba namba UKMMD/1237 iliyoko Mwembe Madafu, Ukonga, Dar es Salaam, kiwanja namba 651, kitalu 'M' kilichopo Forest Area, Mbeya, nyumba iliyoko kiwanja namba 7, kitalu 'P' ikiwa na hati namba 033004/23 kilichoko mtaa wa Rufiji, Manispaa ya Mwanza.

Mali nyingine ni ardhi iliyoko katika kiwanja namba 2/283/2 kitalu "E" Mabibo, Kinondoni, Dar es Salaam, kipande cha ardhi ambacho hakijapimwa kilichoko Kijiji cha Manyinga, Turiani, Mvomero, Morogoro, kiwanja namba 467 kilichoko kitalu "H" kikiwa na hati ya usajili namba 48170, kilichoko eneo la Tegeta, Dar es Salaam, nyumba iliyoko kiwanja namba MM/19/P kilichoko Manzese karibu na Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam na nyumba iliyoko katika kiwanja namba KND/MXS/MNM/Z, ikiwa na leseni ya makazi namba KND 008337 Kinondoni, Dar es Salaam.

Magari ambayo DPP anaiomba mahakama kutoa amri ya kutaifishwa na kuwa mali ya serikali ni Toyota Premio, namba T 132 AWJ, Toyota Land Cruiser namba T 480 AUP, Toyota Rav 4 namba T 274 ATQ, Toyota Mark II, T 676 AYP, Subaru Legacy, T 682 AUT, Toyota Ipsum, T 850 AXY, Toyota Ipsum T455 ADM, Toyota Mark II, T 186 AYX, Mitsubishi Pajero T 852 AAV, Toyota Land Cruiser, T 789 AUX, Nissan Terrano, T 899 AYU.

Pia, DPP anaomba mahakama kutoa amri ya kutaifishwa kwa fedha zilizoko benki katika akaunti namba 22601601056 iliyoko National Microfinance Bank (NMB), tawi la Msasani ikiwa na Sh. 12,503,068,647.89.

Fedha nyingine taslimu ni zilizoko katika akaunti namba 0001201000000194/1 iliyoko Dar es Salaam Community Bank (DCB), tawi la Uhuru ikiwa na Sh. 1,457,700,462.49 na fedha taslimu zilizoko katika akaunti namba 021140019558 iliyoko Kenya Commercial Bank (KCB), tawi la Samora, Dar es Salaam, ikiwa na Sh. 57,933,304.10.

Kupitia maombi hayo, DPP anaiomba mahakama itoe amri nyingine itakayoona inafaaa.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WAFANYAKAZI WA HOTELINI**, Wanatakiwa wafanyakazi wa Usafi, Wahudumu, Wapishi na Meneja. Bagamoyo mjini, wawe na vyeti na uwezo wa kuongea Kingereza. kwa Mawasiliano piga namba: 023-2440004/0657, 233970/0768 296667


**NAFASI ZA KAZI UALIMU / CERTIFICATE** au diploma / english/mathematics na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311



## KUPOTEA KWA CHETI



**Tresphory Kisakali** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0443/0560** kilichotolewa na Baraza la Mitihani mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Meta. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi Polisi Taarifa: **NJ/RB/136/2019.**

115122202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Alan Aloyce Mhonzu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S4543-0125** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2014, katika shule ya sekondari Brilliant. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **URP/RB/1513/2019**

115123002

## KUPOTEA KWA CHETI



**Jullieth Kamala** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1689-0055** kilichitolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Peace. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KAS/RB/1734/2019**

115122702

**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA mjini**

**Usimamizi wa mirathi NA.19/2019**

**Ombi la DAVID SAMWEL LYIMO kuteuliwa Msimamiliz wa mirathi ya marehemu SAMWEL ELIYAPENDA**

**Kwa yeyote anayehusika Tanzania Bara**

Watu wote anaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 18/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa Tarehe




215123502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Hilda Dominic Mlelwa** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba **MC973 ADN** aina **TVS KING**, yenye chasis namba **MD6MI4PKOE4H9687**2. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **CID/TR/RB/584/2019**

215123702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**



Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
18/03/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 20/03/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **ARUSHA** kuelekea **DAR-ES-SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili: **T748 BBW T891ANB**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 24** |
| **Upana** | – | **mita 3.7** |
| **Kimo** | – | **mita ……..** |

3. Njia itakayotumika **ARUSHA** hadi **DAR-ES-SALAAM** kupitia BAGAMOYO gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215123802

## KADI YA TRAILER IMEPOTEA

**FLORIAN CHOGO SIMON**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Trailer lenye namba za usajili **T 724 CCB** Chassis **No. A244467** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**MZ/TR/RB/444/2019**

215123102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;66/2019**

**Ombi CATHERINE PETRO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BONIFACE GHATO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **07/03/2019.**



215122502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**


**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;78/2019**

**Ombi MUSA MOHAMED CHAKU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SELEMAN TORA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/03/2019.



215122402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Aisea Ibrahim Mboja** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba **T626 ABA** aina ya TOYOTA CORONA. Yenye chasis namba **ST1900058056,** Engine namba **4S1231023.** Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**WMB/RB/3215/2019**

115122602


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO



# SARRI:
## Tunaweza kumaliza 4-bora

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, amedai kwamba kikosi chake bado kinaweza kumaliza kwenye nne-bora licha ya kufungwa mabao 2-0 na Everton Jumapili.

'The Blues' hao walifungwa mabao mawili ya kipindi cha pili kupitia kwa Richarlison na Gylfi Sigurdsson kwenye dimba la Goodison Park juzi.

Wameshinda mchezo mmoja tu kati ya minne ya ugenini mwaka huu, hivyo wamejiweka kwenye hatari ya kushindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Sarri alielezea kukatishwa kwake tamaa baada ya kichapo hicho, lakini akasema bado wana changamoto ya kumaliza nafasi ya nne.

Akinukuliwa na tovuti ya klabu yake alisema: "Siyo rahisi, tunahitaji kujiimarisha na kupata pointi tatu.

"Hiyo haiwezekani katika mechi nane kama hatutaweza kujiimarisha zaidi, kama hatutaweza kujiimarisha zaidi kipindi cha pili kama tulivyofanya leo (juzi), uwezekano wa kumaliza kwenye nne-bora ni vigumu."

Kipigo hicho kimeifanya Chelsea kubakia nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, sehemu ambayo walikuwapo tangu walipofungwa mabao 6-0 na Manchester City mwanzoni mwa Februari.

# BARCELONA
## wajiandaa kumuuza Coutinho

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeripotiwa kwamba inajiandaa kumuuza Philippe Coutinho mwishoni mwa msimu huu, licha ya kuanza kuimarika kwa kiwango chake hivi sasa.

Baada ya kuondoka Liverpool kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 142 Januari mwaka jana, Coutinho amekuwa kwenye kiwango duni.

Amefunga mabao tisa tu katika mechi 40 alizocheza, huku akiwa amecheza kipindi cha miezi mitano kwenye La Liga bila kufunga bao, na mashabiki wengi wamekuwa wakimzomea raia huyo wa Brazil katika mechi kadhaa.

Philippe Coutinho hajafunga bao kwenye ligi au mashindano ya Ulaya tangu Oktoba mwaka 2018.

Barcelona sasa inataka kumuuza Coutinho kwa kuwa wanajiandaa kuachana naye kipindi cha majira ya joto hata kama kiwango chake kitaimarika, kwa mujibu wa Gazeti la Marca.

Kuumia kwa Ousmane Dembele kutampa nafasi kubwa Coutinho kujiimarisha mwenyewe mwezi ujao, lakini Gazeti la Marca limedai kwamba Barcelona haina mpango wa kuendelea na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.

Klabu za Chelsea na Manchester United zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Coutinho katika wiki za hivi karibuni, lakini watatakiwa kulipa karibia kiasi cha pauni milioni 142.

Gazeti la Marca limebainisha kwamba, Barcelona wanataka kumuuza mchezaji huyo kwa sababu tayari kuna Dembele na Malcom ambao wanaweza kumsaidia Lionel Messi na Luis Suarez.

Kumuuza Coutinho maana yake ni kutafuta fedha kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho, kwa kuwa wachezaji kadhaa wanatajwa kuwaniwa na Barcelona.

Wachezaji kama Paulo Dybala na Christian Eriksen wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutua hapo Camp Nou.

Barcelona inatajwa kwamba, kipindi cha majira ya joto inataka kukiimarisha zaidi kikosi chake kwa ajili ya michuano ya Ulaya na Ligi Kuu ya Hispania.

Barca kwa sasa wanaongoza msimamo wa La Liga, huku pia ikiwa imetinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na itaanza kucheza na Manchester United kwenye dimba la Old Trafford mwanzoni mwa Aprili mwaka huu.






# Nainggolan atoa sababu kuachana na AS Roma

**ROME,** Italia

KIUNGO wa Inter Milan, Radja Nainggolan, amebainisha kwamba ugomvi wake na mkurugenzi wa soka, Monchi ndio uliosababisha yeye kuondoka AS Roma kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Licha ya kuwa mmoja wa wachezaji wa kikosi cha kwanza cha Roma kwa miaka kadhaa, Nainggolan aliondoka kwenda pale San Siro kwa uhamisho uliowahusisha Davide Santon na Nicolo Zaniolo kwenda Roma.

Akizungumza na Gazeti la Eleven Sports la Ubelgiji, Nainggolan amefunguka kuhusu kuondoka kwake kwa 'Giallorossi' hao.

Alinukuliwa akisema: "Nilishindwa kuelewana na mkurugenzi wa soka (Monchi). Alikuwa anafanya mambo ya kipuuzi dhidi yangu.

"Alisema walitaka kuniuza, na mimi nikasema sawa. Lakini baadaye akataka kuniuza kwenda Uturuki bila ya kunijulisha.

"Nikaona kwamba, singeweza kuendelea kukaa pale. Jambo la msingi lilikuwa ni mimi kuondoka na kwenda sehemu nyingine."



## TOTTENHAM kufungua uwanja wake na Crystal Palace Aprili

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham imebainisha kwamba watacheza mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu kwenye uwanja wao mpya dhidi ya Crystal Palace Jumatano ya Aprili 3, mwaka huu.

Miamba hao wa London Kaskazini awali walipanga kuhamia kwenye uwanja wao mpya mwanzoni mwa msimu huu, lakini ilishindikana.

Taarifa rasmi katika tovuti ya klabu ya Tottenham imethibitisha kwamba mchezo wa kwanza kwenye uwanja wao huo mpya utapigwa mwanzoni mwa Aprili.

Aidha, taarifa hiyo imebainisha kwamba mchezo wa pili kuchezwa kwenye uwanja huo utakuwa dhidi ya Manchester City ukiwa ni wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Sasa tunaweza kuthibitisha kwamba, mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa uwanja wetu mpya utakuwa dhidi ya Crystal Palace Jumatano ya Aprili 3.

"Na utafuatia mchezo wa Jumanne ya Aprili 9 ambao utakuwa wa robo fainali dhidi ya Manchester City. Pia tutacheza dhidi ya Brighton kwenye Ligi Kuu kwenye uwanja wetu Aprili 23 au Jumatano Aprili 24."

Uwanja huo una uwezo wa kuchukua watazamaji 62,062.

# MARTIAL

## ajitoa kikosi cha Taifa Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

ANTHONY Martial amejiondoka kutoka kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ufaransa kinachojiandaa na michuano ya kufuzu michuano ya Euro 2020.

Winga huyo wa Manchester United alijumuishwa kwenye kikosi cha kocha, Didier Deschamps, licha ya kwamba kwa mara ya mwisho kuichezea nchi yake ilikuwa ni kwenye ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Urusi mwaka mmoja uliopita.

Hakujumuishwa kwenye kikosi kilichoshinda Kombe la Dunia na pia hakuwapo katika mechi dhidi ya Uholanzi na Uruguay Novemba mwaka jana, kutokana na majeraha.

Kwa mara nyingine tena, Martial hatakuwapo kwenye kikosi cha Ufaransa baada ya Shirikisho la Soka la Ufaransa kuthibitisha kwamba mchezaji huyo aliumia goti wakati akiichezea United dhidi ya Wolves kwenye Kombe la FA.

Madaktari wa pande zote mbili wamechukua maamuzi ya kukubali Martial abakie United ili aweze kuimarika afya yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hivi karibuni alirudi dimbani baada ya kupona nyonga ambapo aliumia kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16-bora dhidi ya Paris Saint-Germain.

Kwa mujibu wa mwandishi, Simon Peach, Martial sasa nafasi yake itachukuliwa na winga wa Atletico Madrid, Thomas Lemar, wakati Ufaransa ikijiandaa na mechi dhidi ya Iceland na Moldova.

Bado haijabainishwa ameumia kwa kiasi gani, lakini imedaiwa kuwa kocha wa muda wa United, Ole Gunnar Solskjaer ana matumaini Martial atakuwa fiti kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Watford mwishoni mwa mwezi huu.

Hadi sasa, Martial amefunga mabao 11 kwenye mashindano yote, ingawa amefunga mara tatu tangu Solskjaer achukue mikoba Desemba mwaka jana.

# Barcelona kusita kumsajili Gomez

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA huenda haitaendelea na mpango wake wa kutaka kumsajili mshambuliaji wa Celta Vigo, Maxi Gomez, kwa kuwa tayari wameshafikisha idadi ya wachezaji wanaotakiwa kuwapo kwenye kikosi chake ambao hawatoki Jumuiya ya Ulaya.

Gomez amekuwa kwenye kiwango cha kuridhisha kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, akiwa na Celta msimu huu, huku akifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho tano.

Na matokeo yake mchezaji huyo raia wa Uruguay amekuwa kwenye rada za klabu kubwa za Ulaya na inaonekana wazi kwamba, hataweza kukaa na Celta ambao wapo kwenye hatari ya kushuka daraja.

Barcelona imetajwa kuwa moja ya timu inayowania saini yake, kwa mujibu wa Gazeti la Marca.



Sheria za Hispania zinaruhusu klabu kuwa na wachezaji watatu tu ambao wanasajiliwa kwa wakati mmoja ambao hawatoki Jumuiya ya Ulaya.

Barcelona tayari wameshafikisha idadi hiyo ya wachezaji ambao ni Arturo Vidal, Arthur na Malcom.

Philippe Coutinho yeye sheria hiyo haimhusu kwa sababu ana uraia wa nchini mbili, Brazil na Ureno ambao ipo kwenye Jumuiya ya Ulaya.

Na sasa kama Barcelona watataka kumsajili Gomez watatakiwa kwanza kumuuza mmoja kati ya Vidal, Arthur au Malcom.

## KWA UFUPI

### GRIEZMANN ATAKA KUTUA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann, 27, amejutia kwa kutochagua kujiunga na Barcelona majira ya joto yaliyopita na anajaribu kuitafuta nafasi hiyo tena ya kutua Nou Camp. **(L'Equipe - in French)**

### ABRAMOVICH KUMTIMUA SARRI

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich, anaweza kutumia mapumziko haya ya kimataifa kumtimua kocha Maurizio Sarri baada ya kukatishwa tamaa na kipigo kutoka kwa Everton Jumapili. **(Express)**

### RODRIGUEZ KUTIMKA BAYERN

KIUNGO wa Bayern, Mcolombia James Rodriguez, 27, hataki kuendelea kubaki Munich baada ya mkataba wake wa mkopo akitokea Real Madrid, kumalizika mwishoni mwa msimu. **(Marca)**

### ERIKSEN AITAMANI MADRID

KIUNGO mshambuliaji wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen, 27, ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya London utamalizika majira ya joto 2020, anawindwa na Real Madrid na ana ndoto za kuichezea klabu hiyo ya Hispania tangu akiwa mdogo. **(Express)**

### KLOPP AITOLEA NJE BAYERN

KOCHA Jurgen Klopp ana nia ya kuendelea kuwapo Liverpool baada ya nahodha wa Ujerumani, Franz Beckenbauer, kumtaka kubeba majukumu ya kuinoa Bayern Munich. **(Liverpool Echo)**

### OVERMARS KUULA ARSENAL

ARSENAL itafikiria kuipata huduma ya mchezaji wao wa zamani Marc Overmars kama mkurugenzi wa ufundi baada ya waliyekuwa wakimuwinda, Monchi kuchagua kurudi Sevilla kufuatia kuachana na Roma. **(Telegraph)**

### JOTA AIKUNA TOTTENHAM

WASAKA vipaji wa Tottenham walivutiwa na straika kinda wa Benfica, Jota, 19, baada ya kumtazama Mreno huyo kwenye mechi ya Europa League dhidi ya Dinamo Zagreb. **(A Bola, via Sun)**

### HAZARD KUMBAKISHA HUDSON-ODOI

CHELSEA itaamua kutomuuza winga wa Muingereza Callum Hudson-Odoi, 18, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2020, kama watamuuza mshambuliaji Mbelgiji Eden Hazard, 28, kwa Real Madrid majira haya ya joto. **(Sun)**

### DAU KUIKIMBIZA MILAN

AC Milan inaweza kukatishwa tamaa na thamani ya pauni milioni 60 ambazo Everton inataka ili kumwachia mshambuliaji Mbrazil Richarlison, 21. **(Calciomercato)**

### UNITED, CHELSEA KWA FELIX

MSHAMBULIAJI wa Benfica, Mreno Joao Felix, 19, amesema ni mwenye furaha katika klabu hiyo licha ya kuwapo kwa taarifa za kuwindwa na Manchester United na Chelsea. Hivi karibuni Liverpool ilitoa ofa ya pauni milioni 61 ambazo zilikataliwa na klabu hiyo. **(Marca - in Spanish)**

### FERREIRA KUIGHARIMU LIVER

LIVERPOOL imewasiliana na Benfica kuhusu uwezekano wa kuweka rekodi ya dunia kumsajili beki wa kati Mreno Francisco Reis Ferreira, 21. **(Record, via Metro)**

### SPURS SOKONI KAMA KAWA

MWENYEKITI wa Spurs, Daniel Levy, amesema mipango ya usajili wa majira ya joto hauwezi kuathiriwa na gharama za ujenzi wa uwanja wao mpya. **(ESPN)**

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI APINDUA TENA REKODI BARCELONA

**BARCELONA,** Madrid

LICHA ya kuiongoza Barcelona kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 kwa kutupia hat-trick na kuzidi kuandika rekodi katika wasifu wake kisoka, Lionel Messi amewashukuru mashabiki wa Real Betis kwa kuonyesha kukunwa na uchezaji wake.

Hat-trick hiyo ni ya 51 kwa Messi katika wasifu wake kisoka, lakini kwa upande wa La Liga ni ya 33, ambapo kwenye mechi hiyo aliikamilisha kwa kuubetua mpira kilaini ambao ulimshinda mlinda mlango Pau Lopez na kufanya matokeo kuwa 4-1 katika dimba hilo la Benito Villamarin.

Aidha, kwa ushindi huo, Messi sasa ndiye mchezaji aliyeibuka na ushindi katika mechi nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote Barcelona, hivyo kumpiku Xavi aliyekuwa akishikilia rekodi hiyo.

Katika mechi hiyo ambayo ni 674 kwake kuichezea Barca, inamfanya kumfikia Andres Iniesta katika orodha ya wachezaji walioichezea klabu hiyo mechi nyingi zaidi, lakini Messi akishikilia rekodi ya kuibuka na ushindi katika mechi 477, ambapo sasa amempiku Xavi.

Nahodha huyo wa Barca alishindwa kuamini kwa namna mashabiki wa nyumbani, Real Betis ambao walionyesha shukrani yao kwa kuonyesha uchezaji wa kiwango cha juu.

"Ukweli ni kwamba sikumbuki hili [kutokea hapo kabla]," Messi aliiambia Movistar baada ya kufunga hat-trick yake ya 33 kwenye La Liga.

"Ni mwenye furaha kwa muitikio wa mashabiki. Kila tunapokuja katika uwanja huu wanatupa mapokezi mazuri, kwa furaha kubwa na ni furaha kwa ushindi huu, ambao ni muhimu sana.

"Mabao mazuri, lakini juu ya yote kilicho muhimu ni kuvuna pointi tatu. Ni fursa nzuri sana kuongeza wigo, tulijua matokeo ya Atletico Madrid na hatukuweza kuanguka."

Barca ilimiliki mpira kwa asilimia 43.9 tu, kiwango ambacho ni cha chini zaidi tangu kampuni ya kutunza takwimu michezoni ya Opta ilipoanza kuifanya kazi hiyo msimu wa 2004-05.

"Tulicheza dhidi ya timu ambayo inauchezea mpira vizuri," Messi aliongeza. "Kiufundi ilikuwa vizuri na hatukuhaha, kama wenzetu."

Kikosi hicho cha Ernesto Valverde kipo katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa baada ya kuongeza wigo wake wa pointi katika msimamo wa ligi na kuwa 10 zaidi.

Katika mechi hiyo iliyopigwa juzi, Jumapili bao lingine la Barca lilifungwa na Luis Suarez.

## HABARI MICHEZO




Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars, Paul Makonda (wa pili kulia), akizungumza jijini Dar es Salaam jana kuhamasisha mashabiki wa soka kujitokeza kwa wingi Jumapili kuishangilia Stars itakapokuwa ikicheza na Uganda. Wengine ni wajumbe wa kamati hiyo, Mhandisi Hersi Said (kulia), Philimon Ntalihaja (kushoto) na Athumani Nyamlani. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# MAKONDA, SPIKA WAFUNGUKA SIMBA INAVYOPAISHA UCHUMI

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa nyakati tofauti wameipongea Simba kwa kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku wakieleza kuwa mafanikio hayo licha ya kuitangaza Tanzania kimataifa, yataliongezea taifa pato la kiuchumi pindi wapinzani wa timu hiyo watakapokuja kucheza dhidi yao hapa nchini.

Simba iliyokuwa katika Kundi D imesonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuifunga AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kufikisha pointi tisa, huku kinara wa kundi hilo, Al Ahly ikimaliza na pointi 10.

Akizungumza jana jijini, Makonda alisema kuwa wafanyabiashara mbalimbali wakiwamo wenye hoteli, usafiri na chakula hufanya biashara kwa kuwahudumia wagezi (timu) wanaokuja nchini kwa ajili ya kucheza na Simba na hivyo pato la uchumi huongezeka.

Makonda alisema mafanikio yaliyofikiwa na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara watalifanya jina la Tanzania kuendelea kutajwa katika medani za kimataifa na wachezaji watapata nafasi ya kunadi vipaji vyao.

Pia aliwapongeza mashabiki wa Simba kwa kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao na kusema kwamba walitimiza jukumu lao la kuwa mchezaji wa 12 uwanjani.

"Hongera sana Simba, hongera wote walioshiriki kufanikisha ushindi ule, huu ni ujumbe mkubwa kwa serikali na Afrika kuwa mpira ni jadi yetu na tuna mahaba makubwa, " alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli kwa kuwekeza katika michezo na kuamua kujenga uwanja mwingine wa michezo wa kisasa ambao utakuwa na uwezo wa kuingiza mashabiki zaidi ya 100,000.

"Sasa Simba wameonyesha Tanzania sio Shamba la Bibi... wametupa matumaini mapya, tutajisikia hafari kupata uwanja huo mpya, ametupa deni," Makonda alisema.

Kwa upande wake Spika Ndugai mbali na kuipongeza Simba, wakati akizindua Ofisi ya Shirika la Ndege nchini(ATCL) jijini Dodoma jana, alisema kwa sasa nchi ya Congo na Misri wanaifahamu Tanzania na hivyo michezo hiyo itakuwa imetangaza ndege za ATCL.

"Tunapoendelea kuitangaza nchi yetu nitumie nafasi hii pia kuipongeza Klabu ya Simba kwa walichokifanya Jumamosi kwa kuifunga AS Vita, wapo watakaonuna, lakini nasema kwa dhati DRC Kongo nchi kubwa hakuna asiyejua neno Tanzania kupitia mpira ule,"alisema.

Alisema kwa mtu mpenda michezo hakuna ambaye atakuwa hajui nchi inayoitwa Tanzania kwa sababu imetangazwa sana na ATCL itakapotaka kuelekea eneo hilo ina faida za ziada kupata wateja.

"Vivyo hivyo mpenda mpira wa Misri, Al Ahly ambayo ni klabu namba moja kule imepigwa, inaijua Tanzania, Algeria hivyo hivyo, kwa hiyo kwa kupitia michezo imetangaza nchi kwa kiwango ambacho huwezi kuamini," alisema.

**Imeandaliwa na Somoe Ng'itu, DAR na Augusta Njoji, DODOMA**

# Ufaransa, Ubelgiji kutoana jasho Dar

**Na Salome Kitomari**

TIMU nane za nchi zinazozungumza Kifaransa zinatarajiwa kutoana jasho mwishoni mwa wiki ikiwa ni maadhimisho ya wiki ya umoja wa nchi zinazozungumza lugha hiyo duniani, huku mechi kali ikitarajiwa kuwa kati ya Ufaransa na Ubelgiji, imeelezwa.

**Mashindano hayo ambayo yataleta pamoja timu za nchi saba pamoja na timu ya umoja wa walimu wanaofundisha Kifaransa jijini Dar es Salaam (Dafta), yatafanyika katika viwanja vya Jakaya Kikwete (JKM Park), jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu michezo mbalimbali itakayofanyika wakati wa maadhimisho hayo, Balozi wa Ubelgiji nchini, Peter Van Acker, alisema kutakuwa na makundi manne ya timu ambazo zitacheza robo fainali, nusu fainali na baadaye fainali ili kupata mshindi.

Alizitaja timu hizo kuwa Kundi la Kwanza litaundwa na Uswisi na Morocco, Kundi la Pili litakuwa ni Canada na Rwanda, Kundi la Tatu ni Congo na Dafta, wakati Kundi la Nne likiwa ni Ufaransa na Ubelgiji.

"Timu zote zimefanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya kuukabili mchezo huo, na kila mmoja anataka kuwa mshindi katika mashindano hayo. Hatuishii kuzungumza lugha ya Kifaransa tu, bali tunafanya michezo mbalimbali kwa ajili ya afya zetu na kuleta pamoja zaidi," alisema.

Naye Rais wa Dafta, Patrick Shole, alisema timu ya walimu siku zote imekuwa mshindi kwenye mashindano hayo na mengine, na kwamba katika mchezo wa sasa wamejipanga kutunza rekodi ya ushindi kwenye mashindano hayo.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 30 | 8 | 11 | 11 | 27 | 35 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Wanawake Msimbazi kukutana keshokutwa

**Na Khadija Kalili**

WANACHAMA wanawake wa Simba wanatarajia kukutana katika kikao maalumu kitakachofanyika keshokutwa Alhamisi kwenye makao makuu ya klabu hiyo yaliyopo Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza jana jijini, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Asha Baraka 'Iron Lady' alisema kikao hicho kitafanyika kuanzia saa 5:00 asubuhi na malengo ya kuwakutanisha ni kupata nafasi ya kujadiliana mambo mbalimbali yatakayowaletea maendeleo.

Asha alisema moja ya agenda itakayozungumzwa ni namna ambayo wataipongeza klabu yao kwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na vilevile kuangalia fursa zinazopatikana katika mchezo huo wa soka hapa nchini.

"Huu utakuwa mkutano wa kwanza kufanyika na yote yatakayojadiliwa yatapelekwa katika Bodi ya Wakurugenzi wa Simba na pia yatapelekwa kwa Mwekezaji wetu, Mohammed Dewji," alisema Asha.

Aliongeza kuwa anaamini wanawake wanamchango hadi hapo klabu yao ilipofikia na wanataka kuongeza nguvu ili waweze kufanya vema zaidi katika hatua hiyo waliyofika na kutetea ubingwa wa ligi wanaoushikilia.

"Natolea mfano halisi ni kama katika mechi ya juzi, fursa za kibiashara zilianza tangu saa tatu asubuhi, hivyo wanawake wa Simba walitakiwa wafanye ujasiriamali wa kutosha na mwisho wa siku mwanachama anatoka akiwa na mfuko umejaa pesa kwa sababu Simba inapocheza wanaingia mashabiki karibu 50,000, sasa hapo inakuwaje mtu atoke mikono mitupu," Asha alisema.

Baada ya kumaliza majukumu ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba leo inatarajia kuivaa Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

# Michezo

Jumanne Machi 19, 2019

Nipashe


## Sarri: Tunaweza kumaliza 4-bora



HABARI UK. 28

KIJIJI!...



Lionel Messi akikitoka 'kijiji' cha mabeki wa Real Betis kwenye mechi ya La Liga iliyopigwa katika Uwanja wa Benito Villamarin juzi, na Barcelona kushinda kwa mabao 4-1. Messi alifunga hat-trick yake ya 33 La Liga kwenye mechi hiyo. **HABARI UK. 30**

# SIMBA KUISHUKIA RUVU KAMA VITA

## ●●● Yasema hakuna atakayebaki salama Ligi Kuu, Magori afuata droo robo fainali Caf Misri huku...

**Na Somoe Ng'itu**

TUMEREJEA! Baada ya kumaliza mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi cha Simba kimerejea kuendelea kusaka pointi tatu kwa kuwavaa Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam, huku ikieleza kuwa moto uliowalipua AS Vita ndio watakaoendelea nao.

Awali mechi hiyo ilitarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro lakini kutokana na baadhi ya wachezaji wa Simba kubanwa na kambi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars) na wengine wa nje kutakiwa kusafiri leo usiku, mchezo huo umelazimika kurejeshwa Uwanja wa Taifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema timu yake itaingia kwa kasi ile ile ya kusaka pointi tatu kama ilivyocheza katika mechi za mashindano ya kimataifa kwa sababu malengo yao ni kutetea taji hilo wanalolishikilia.

Rweyemamu alisema kuwa wachezaji wote ni wazima na jana asubuhi walifanya mazoezi isipokuwa nyota wake walioitwa katika kikosi cha Taifa Stars ambacho kinajiandaa kuikaribisha Uganda (Cranes) Jumapili.

"Vijana wako vizuri na tunamshukuru Mungu Jumamosi hatukupata majeruhi, wamefanya mazoezi leo (jana) asubuhi na kwa kifupi tuko tayari kwa mechi hiyo ya kesho (leo) ambayo itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku," alisema Rweyemamu.

Aliongeza kuwa kila mchezo ulioko mbele yao ni sawa na fainali na wanahitaji "kuwakimbiza" Yanga na Azam ambao wanapointi nyingi zaidi na wamejiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Naye kiungo wa kimataifa wa Simba Mnyarwanda, Haruna Niyonzima, aliliambia gazeti hili kuwa wamejipanga kuendelea kuwapa furaha mashabiki wa timu yao baada ya Jumamosi iliyopita kuweka historia kwa kuingia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Sio mimi tu, kila mchezaji wa Simba huwa yuko tayari kuisaidia timu na kufanya kile ambacho mwalimu ameelekeza, tunahitaji kushinda pia mechi zetu za Ligi Kuu ili kujihakikisha ubingwa kwa msimu wa pili, na kupata tena nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani," alisema kiungo huyo ambaye katika mechi dhidi ya AS Vita alionyesha kiwango cha juu.

Katika hatua nyingine, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alitarajiwa kuondoka leo kuelekea jijini Cairo, Misri tayari kushuhudia droo ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezeshwa kesho.

Kwa upande wa Ligi Kuu, Yanga ndio wanaongoza katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 67, lakini wamecheza mechi 28 wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 59 baada ya mechi 28 na Simba yenye pointi 51 ni ya tatu kufuatia kushuka dimbani mara 20.

Ruvu Shooting ambayo imecheza mechi 30, ina pointi 35 na iko katika nafasi ya 16 katika msimamo wa ligi, wakati African Lyon iliyocheza michezo 31 ina pointi 22 na inaburuza mkia.

## Mashabiki Yanga, Simba waitwa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa Simba, Yanga na klabu nyingine za soka hapa nchini wametakiwa kujitokeza kuishangilia Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) katika mechi ya kufuzu Fainali za Afrika itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini, Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars, ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alisema umefika wakati kwa mashabiki wote kuungana na kuishabiki timu hiyo ili iweze kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo.

Makonda alisema kuwa shabiki ni kiungo muhimu sana na anawaomba Watanzania wote kusimama na Taifa Stars kwa wakati huu.

"Ninawaomba watu wote tujitokeze kuiunga mkono Taifa Stars, tusimame na Stars, tuhakikishe tunaacha tofauti zetu, tuhakikishe kila mmoja anatimiza jukumu lake, tutumie fursa hii kuhakikisha Stars inashinda," alisema Makonda.

Alisema anahitaji kuona makundi yote yanajitokeza kuishangilia Taifa Stars na angetamani kuona Uwanja wa Taifa unajaa mara tatu ya walivyojitokeza mashabiki wa Simba katika mchezo wao dhidi ya AS Vita uliochezwa Jumamosi iliyopita.

"Sisi tunaunganishwa na Taifa Stars, tuitumie Stars kama sehemu ya kutuunganisha, AFCON 2019 ni zamu yetu," Makonda alisisitiza.

**NYONI AREJESHWA STARS**

Beki wa kati wa Simba, Erasto Nyoni aliyekuwa majeruhi tangu mapema Januari, mwaka huu, amerejeshwa katika kikosi cha Stars kilichoko chini ya Mnigeria, Emmanuel Amunike, baada ya kuonyesha kiwango kizuri wakati timu yake ikicheza na AS Vita ya DRC Jumamosi iliyopita.

Meneja wa Stars, Danny Msangi, alisema kuwa mchezaji huyo ameitwa kuziba nafasi ya beki wa Yanga, Andrew Vicent "Dante" ambaye ni majeruhi.

Msangi alisema tayari kikosi cha Stars kimeshaingia kambini tangu juzi kuanza mazoezi ya kujiwinda kuikabili Uganda, huku akiongeza kuwa nyota wanaocheza nje akiwamo mshambuliaji, Simon Msuva ameshawasili wakati nahodha, Mbwana Samatta anatarajiwa kutua nchini leo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002